# Nipashe

Jumanne Aprili 9, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579887

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## JPM awaonya mawaziri waliotelekeza viwanda

UKURASA 3




13

# Sakata la CAG moto bungeni



• **Mnyika**, Waziri Mhagama wabanana kwa vifungu, Naibu Spika atia neno, Chenge ataka sheria zizingatiwe...*Ukurasa 2*



MHAGAMA

MNYIKA

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MOI KUGAWA BURE MIGUU BANDIA 600**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) kwa kushirikiana na Taasisi ya BMVSS ya India...

UKURASA WA 3

**JELA MIAKA 60 KUMBAKA BINTIYE**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, imemhukumu kifungo cha miaka 60 jela Salim...

UKURASA WA 5

**POLISI WALIVYOUA MAJAMBAZI WATANO**

WATU watano wanaodhaniwa kuwa majambazi wameuawa na Jeshi la Polisi mkoani Tanga...

## Mfumuko wa bei wazidi kupaa

UKURASA 3



## Mbunge CCM ataka kusiwapo na uchaguzi wa Rais

UKURASA 2

**MICHEZO** MAZEMBE, SIMBA MAREFA KIMENUKA UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

## MOI kugawa bure miguu bandia 600

Na Mary Geofrey

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) kwa kushirikiana na Taasisi ya BMVSS ya India zinatarajiwa kuendesha upimaji na kutoa bure zaidi ya miguu bandia 600 kwa watakaohitaji.

Watu wenye uhitaji wa miguu hiyo, wametakiwa kufika MOI ndani ya mwezi huu kwa ajili ya vipimo na maelekezo mengine na kwamba ugawaji wa miguu hiyo utafanyika Mei, mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alitoa wito huo jana na kusema mpango huo ni sehemu ya mkakati wa MOI na serikali wa kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora kwa wakati kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi.

"Ni azima yetu MOI na serikali kuhakikisha huduma zote zinawafikia wananchi hususani wa kipato cha chini, hivyo miguu hii bandia itatolewa bure kwa watu wenye uhitaji. Tunafahamu wako Watanzania wengi ambao walishindwa kupata miguu hii bandia kutokana na kukosa fedha, hivyo tumeona ni vyema tukawaondolea changamoto hii," alisema Dk. Boniface.

Alisema wako Watanzania wengi ambao wameshindwa kuendelea na maisha yao ya kila siku ya uzalishaji kwa kukosa miguu bandia.

"Wapo wenzetu ambao walipoteza viungo na wakakata tamaa wakidhani huo ndio mwisho wa maisha yao. Sisi MOI pamoja na serikali tunawatia moyo kwamba wakipata miguu bandia wanaweza kurudi katika shughuli zao za uzalishaji kama kawaida, hivyo wajitokeze ili wapate miguu," alisema.

Aidha, alisema pamoja na kutoa miguu hiyo bandia, MOI iko kwenye mpango mkakati wa kuendelea kusogeza huduma kwa wananchi na katika kutekeleza hilo, imeweka kambi iliyoanza jana na itamalizika Aprili 12, mwaka huu.

Madaktari bingwa wa ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu wa MOI wamepiga kambi katika Hospitali ya Bugando jijini Mwanza na ambako watafanya upasuaji kwa wakazi wa Kanda ya Ziwa.

# Sakata la CAG moto bungeni

Na Sanula Athanas, DODOMA

SAKATA la utata wa uwasilishaji wa ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2017/18, limeendelea kuwa gumzo bungeni wakati Bunge la Bajeti likiingia katika wiki ya pili jana.

Mara tu baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali' bungeni jana asubuhi, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika (Chadema), alisimama na kuomba mwongozo wa Kiti cha Spika akitaka Bunge lielezwe tarehe ya kuwasilishwa kwa ripoti hiyo ya mwaka ya ukaguzi wa CAG.

Vilevile, Mnyika ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Tanzania Bara, alitaka Bunge lielezwe sababu za kutowasilishwa bungeni kwa ripoti hiyo hadi jana.

"Mapema leo (jana) asubuhi, tumekabidhiwa orodha ya shughuli za leo (jana) ambayo pamoja na mambo mengine hati ya kuwasilisha mezani.

"Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya nchi Ibara ya 143(4) inasema Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha kwa Rais kila taarifa itakayotoa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya pili.

"Baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais atawaagiza watu wanaohusika wakaiwasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla haijapita siku saba tangu siku iliyoanza kikao hicho.

"Endapo Rais hatachukua hatua ya kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Bunge au Naibu Spika ikiwa kiti cha Spika kiko wazi au ikiwa kwa sababu zozote Spika hawezi kutekeleza shughuli zake, basi ataiwasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge.

"Naomba mwongozo wako kwa sababu taarifa iliyotolewa na Ofisi ya CAG inaonyesha kwamba Machi 28, Rais alipokea ripoti za ukaguzi kutoka kwa CAG kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2018.

"Na kikao cha kwanza cha Bunge kilianza tarehe mbili ya mwezi huu na taarifa alizopokea Rais hazijawasilishwa na katiba imezungumzia siku saba, haijazungumzia siku za kazi au zisizokuwa za kazi.

"Naomba mwongozo wako ni kwanini katika orodha ya shughuli za leo (jana) hakuna ripoti ya CAG kwenye hati zilizowasilishwa mezani? Ni tarehe ngapi hasa Rais ataagiza wanaohusika walete ripoti ya CAG bungeni kabla haijapita siku saba ambazo Rais anatakiwa kwa mujibu wa katiba kuwasilisha ripoti bungeni?" Mnyika alihoji.

Hoja hiyo ya Mnyika ilimwinua kitini Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Ajira, Kazi na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, ambaye alisema Mnyika aliomba mwongozo kwa lengo la kuonyesha kwamba serikali haiwajibiki.

Mhagama ambaye pia ni Mnadhimu Mkuu wa Serikali bungeni, alikiomba kiti cha Spika kutoa tafsiri ya kisheria kuhusu hoja iliyoombewa mwongozo na mbunge huyo.


"Kwa kuwa kwa mujibu wa utaratibu wa shughuli za Bunge, katika mijadala iinayoendelea bungeni leo (jana), (Mnyika) ameonyesha

INAENDELEA UK 8



Rais John Pombe Magufuli akibonyeza kitufe kuwasha mitambo ya kuchakata mahindi baada ya kuzindua rasmi kiwanda cha kuchakata mahindi cha JKT Mlale, kilichopo mjini Songea, mkoani Ruvuma jana. **PICHA: IKULU**


## SHUKRANI



*Mzee William David Bocco*

Familia ya **Mzee Wiliam David Bocco.** Inatoa shukrani za zao za dhati kwa dhati kwa ndugu, jamaa na marafiki walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kumuuguza Baba yao mpendwa hadi kifo chake,

**Mzee William David Bocco** alifariki tarehe **30/03/2019** katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kuzikwa Tanga tarehe **01/04/2019.**

**Bwana ametoa na Bwana ametwaa Jina lake lihimidiwe. Ayubu 1:21**

115164802


# Mbunge ataka kusiwe na uchaguzi wa Rais 2020

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

MBUNGE wa Mtera, Livingstone Lusinde (CCM), ameliambia Bunge kuwa kuna haja ya kuweka kando matakwa ya kikatiba kwa kutofanya uchaguzi wa Rais katika uchaguzi mkuu wa mwakani ili Rais John Magufuli apite bila kupingwa.

Mbunge huyo alitoa kauli hiyo bungeni jijini Dodoma jana alipochangia hoja ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuhusu mwelekeo wa kazi za serikali na mapato na matumizi ya ofisi yake na Ofisi ya Bunge kwa mwaka ujao wa fedha.

Lusinde, maarufu Kibajaji, alisema anaweka mezani mjadala kwa wabunge na Watanzania wote kuangalia faida na hasara za kufanya uchaguzi wa Rais mwakani.

Mbunge huyo alisema haoni sababu ya kufanya uchaguzi wa Rais kwa kuwa ana uhakika hakuna mgombea kutoka vyama vya upinzani ambaye atamshinda Dk. Magufuli katika uchaguzi huo.

Lusinde pia alisema kuwa kwa kutofanya uchaguzi wa Rais, nchi itaokoa fedha nyingi ambazo itazielekeza katika utekelezaji wa miradi muhimu kwa wananchi.

"Katika hotuba ya Waziri Mkuu inaonyesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inategemea kuongeza vituo vya uchaguzi 858, jambo ambalo litaongeza gharama kubwa kwa wananchi wetu," mbunge huyo alisema na kueleza zaidi:

"Mimi nawaomba wabunge na Watanzania wote, hivi kwanini mwakani tusifanye uchaguzi wa madiwani na wabunge tu na Rais akapita bila kupingwa? Kwanini tusifanye hivyo? Kwanza, tutakuwa tumeokoa fedha nyingi sana na wakati Rais anaapishwa tumkabidhi cheki ya fedha ambazo taifa limeokoa ili aende kuzitumia kuondoa matatizo ya maji na barabara vijijini.

"Kuna faida gani kwenda kupoteza fedha kwa uchaguzi wa Rais ambaye hana mpinzani? Kwa faida gani? Naomba mitandao yote, wanazuoni wote hoja hii naiweka mezani, tuangalie faida ambayo nchi itapata kwa kufanya uchaguzi na hasara zake ili tupime. Sisi ni wabunge, tunaotokana na familia maskini tusijisahau.

"Watu maskini wanajinyima, badala ya kula milo mitatu wanakula mlo mmoja, kwanini na sisi tusijinyime kwa kula mlo wa madiwani, mlo wa wabunge na Rais apite bila kupingwa?"

Lusinde alisema kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Rais Magufuli kutatua changamoto za wananchi na kusimamia fedha za umma, hakuna chama kitakachosimamisha mgom-

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# Sababu za kupaa mfumuko bei hizi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MFUMUKO wa bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia Machi 2019 umeongezeka hadi asilimia 3.1 kutoka 3.0 kwa mwaka ulioishia Februari 2019.

Hali hiyo imetokana na bidhaa zisizo za vyakula kama vile mavazi na viatu, kodi ya pango, mafuta ya taa, mkaa, kuni, huduma za afya zimechangia kuongezeka kwa mfumuko huo.

Alizungumza jana kwa waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Sensa na Takwimu za Jamii wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ephrahim Kwesigabo, alisema hali hiyo inamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia Machi mwaka huu, imeongezeka kidogo ikilinganishwa na Februari.

"Kuongezeka kwa mfumuko wa bei wa Taifa kumechangiwa hasa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula kwa kipindi cha mwaka ulioishia Machi mwaka huu, ikilinganishwa na bei za Machi 2018," alisema.

Alitaja baadhi ya bidhaa hizo ni mavazi na viatu kwa asilimia 3.4, kodi ya pango kwa asilimia 4.7, mafuta ya taa kwa asilimia 8, mkaa kwa asilimia 13.1, kuni kwa asilimia 27.2, huduma za afya kwa asilimia 1.8, dizeli kwa asilimia 8.3, chakula na vinywaji kwenye migahawa kwa asilimia 4.6 na malazi kwenye hoteli kwa asilimia 5.7.

Aidha, alisema mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwezi Machi 2019, umepungua hadi asilimia 0.1 kutoka asilimia 0.5 kwa mwaka ulioishia Februari 2019.

Akizungumzia hali ya mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki, mkurugenzi huyo alisema nchi ya Uganda mfumuko kwa mwaka ulioishia mwezi Machi 2019 umebaki kuwa asilimia 3.0 kama ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Februari 2019.

"Kwa upande wa Kenya mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Machi 2019 umeongezeka hadi asilimia 4.35 kutoka asilimia 4.14 kwa mwaka ulioishia mwezi Februari 2019,"alisema.



Mhandisi kutoka Kampuni ya CRMBEG, Godwin Kambuga (kushoto), akifafanua jambo kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ujenzi wa daraja la muda kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa daraja jipya la Selander katika eneo la Seaview Upanga. **PICHA: JOHN BADI**

# JPM awaonya mawaziri walioteIekeza viwanda

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ameagiza watu wote walionunua viwanda wakati wa ubinafsishaji viwanda na kushindwa kuviendeleza hata kama ni mawaziri, wanyang'anywe na wakigoma wakamatwe na wafikishwe mahakamani kwa mashtaka ya uhujumu uchumi.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizindua kiwanda cha kuchakata mahindi cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kilichoko Mlale, mkoani Ruvuma ambacho ujenzi wake umegharimu Sh. milioni 444.77.

Akizungumza baada ya kuzindua kiwanda hicho, Rais Magufuli alisema alishatoa wito kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kuwa viwanda ambavyo vilibinafsishwa na havifanyi kazi, wakati umefika wa kuvirejesha na hakuna nafasi ya kuwabembeleza.

"Hata kama waliovichukua walikuwa mawaziri shughulikieni suala la kuwanyang'anya. Wakikataa wapelekeni mahakamani na mnaweza kuwapeleka kwa kuwashtaki kwa uhujumu uchumi," alisema.

Rais aliongeza kuwa: "Wamechelewesha ajira za Watanzania na mapato ni mara 10 wanaposhindwa huko, wapeni hawa ambao wanajua kuvitumia ili vijana wetu wapate ajira."

Alimshukuru Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Martin Msungu kwa kazi na mwelekeo mpya unaofanywa na jeshi hilo.

"Tangu JKT ianze haijawahi kutoa gawio. Leo (jana) mmetoa gawio la Sh. milioni 700. Hii hundi itafikishwa Wizara ya Fedha (na Mipango) ili itumike kwenye bajeti ya serikali.

Rais Magufuli pia aliyataka mashirika mengine ya umma yaliyobaki yajipange kutekeleza hilo.

"Ikiwa JKT imetoa gawio mliobaki, kama wanajeshi wametoa gawio halafu mashirika mengine mtaji ni wa serikali, watendaji wakuu mmekaa tu, kama ni mguu upande mguu sawa au mwili legeza, sasa muanze," alisema.

Rais Magufuli alizitaka Kamati za Bunge zinazohusika zichunguze mashirika ambayo hayatoi gawio lakini wahusika kazi yao ni kulipana mishahara mikubwa, posho nyingi na wanatengeneza vikao vingine nje ya nchi.

"Mtoe mapendekezo ndani ya serikali ili wahusika wote wakiwamo watendaji wakuu na bodi zao watupishe. Lazima ifike mahali tuelezane ukweli ili hizi fedha zijenge taifa," alisema.

INAENDELEA UK 26

# Jela miaka 60 kwa kumbaka bintiye

**Na Steven William, MUHEZA**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, imemhukumu kifungo cha miaka 60 jela Salim Iddi, baada ya kutiwa hatiani kwa makosa mawili ya kumbaka binti na mtoto wa jirani yake.

Iddi, ambaye ni mkazi wa kijiji cha Manyoni, Kata ya Misoswe wilayani hapa, alihukumiwa adhabu hiyo na Hakimu Mkazi Lillian Lutehangwa, kwa kitendo hicho dhidi ya watoto hao ambao ni wanafunzi.

Kabla ya hukumu hiyo, Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Turdo Bandiho, alidai kuwa mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo Oktoba 9, mwaka jana.

Alidai kuwa kutokana na kitendo hicho, wasamaria wema walipeleka polisi taarifa katika Kituo cha Polisi Muheza na binti yake alihojiwa na kueleza kufanyiwa hivyo.

Licha ya binti huyo, alidai kuwa mtuhumiwa pia alidaiwa kumfanyia kitendo kama hicho mtoto wa jirani yake Oktoba 6, mwaka jana ikiwa siku chache kabla ya kile alichofanya dhidi ya binti yake.

Baada ya uchunguzi, mwendesha mashtaka huyo alidai kuwa walimkamata mtuhumiwa na kumfikisha mahakamani na kusomewa mashtaka mawili ya ubakaji.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Lutahengwa alisema ushahidi pamoja na vielelezo vilivyotolewa mahakamani hapo, umethibitisha pasina shaka kuwa mtuhumiwa alifanya vitendo hivyo.

Kutokana na hali hiyo, Lutahengwa alisema mahakamana inamtia hatiani hivyo kumhukumu kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 60 katika Gereza la Maweni, jijini Tanga.


**MAJEMBE AUCTION MART LTD**
**(VIJANA WA KAZI)**

**MNADA WA HADHARA**

Kwa niaba ya **THAMINI UHAI LTD,** tutaendesha mnada wa hadhara wa kuuza magari na vifaa mbalimbali katika jiji la Dar es Salaam na Kigoma.

Mnada utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 13/04/2019 Dar es Salaam na Kigoma kuanzia saa 3:00 asubuhi.

DAR ES SALAAM - Mnada utafanyika yadi za Majembe Auction Mart Ltd, Mbezi Beach, Mwai Kibaki Road, karibu na Rainbow.

| NA. | GARI | HALI YAKE | NAMBA |
|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA LANDCRUISER HARD TOP | NZURI | T 801 BQK |
| 2 | TOYOTA LANDCRUISER LX | NZURI | T 166 DHH |
| 3 | TOYOTA LANDCRUISER LX | NZURI | T 226 BRG |
| 4 | VIFAA VYA OFISI MEZA VITI COMPUTER NK. | VIMETUMIKA | - |

**KIGOMA -** Mnada utafanyika ofisi za Thamini Uhai Jengo la NSSF, Kigoma Ujiji.

**VIFAA VYA OFISI KAMA MEZA, VITI, COMPUTER, PRINTERS, NK.**
**MASHARITI YA MNADA**

a) Ukaguzi unaruhusiwa siku tatu kabla ya tarehe ya mnada.
b ) Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (on the hammer), na salio la asilimia sabini na tano (75%) ni lazima lilipwe ndani ya kipindi cha siku 7 kutoka siku ya mnada.
c) Kiasi cha asilimia ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio asilimia sabini na tano (75%) katika kipindi cha siku saba toka tarehe ya mnada, na gari itauzwa tena.
d) Vifaa vya ofisi malipo ni taslimu.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa simu Na.**
**0786 444400, 0754 301930 na 0767 777727**

# STANBIC BANK TANZANIA

## Tariff Guide

### Effective as of 8th May 2019

| TRANSACTION/SERVICE | | LOCAL CURRENCY | FOREIGN CURRENCY | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **MONTHLY MANAGEMENT FEES** | **DESCRIPTION** | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Uhuru -Personal Current Account | Charged Monthly | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Hatua Account | Charged Monthly | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Pure Savings Account | NO management fee if minimum balance is maintained | NO management fees if balances is above TZS 50,000. Else, TZS 2,000 fee will apply. | NO management fees if balances is above $100. Else, $1.18 fee will apply. | NO management fees if balances is above EUR100. Else, EUR 1.18 fee will apply. | NO management fees if balances is above GBP 100. Else, GBP 1.18 fee will apply. | NO management fees if balances is above ZAR 300 Else, ZAR 17.7 fee will apply. |
| Cooperate and Investment banking | Charged Monthly | 48,000.00 | 20.00 | 18.01 | 16.00 | 290.01 |
| Commercial banking Tier 1 | Charged Monthly | 64,900.00 | 38.94 | 30.68 | 23.60 | 361.08 |
| Commercial banking Tier 2 | Charged Monthly | 35,400.00 | 21.24 | 16.99 | 12.74 | 196.82 |
| Biashara Direct | Charged Monthly | 15,000.01 | 10.62 | 8.26 | 7.08 | 97.94 |
| Private Banking | Charged Monthly PAYT | 29,500.00 | 17.70 | 14.16 | 10.62 | 164.02 |
| Private Banking | Charged Monthly BUNDLE | 53,100.00 | 31.86 | 24.78 | 18.88 | 295.00 |
| **TRANSACTION SERVICES** | | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Cash Withdrawal @ Branch Counter (Either With Cheque, Deposit Slip Etc.)- CURRENT ACCOUNT | Fee could be a % charge on withdrawal (with min charge per withdrawal) or lat charge per transaction. | 4,088 for amounts below 20M, 0.15 % of value max 125,000 for amount above 20M | For FCY withdrawals 1 % min 8 | For FCY withdrawals 1% min 14.16 | For FCY withdrawals 1% min 14.16 | For FCY withdrawals 1% min 141.6 |
| Cash Withdrawal @ Branch Counter (Either With Cheque, Deposit Slip Etc.) - PURE SAVE | One free cash withdraw per month, more than that charge will apply | 5,900 for amounts below 20M, 0.15 % of value max 118,000 for amount above 20M | For FCY withdrawals 1.18 % min 10.62 | For FCY withdrawals 1.18% min 21.24 | For FCY withdrawals 1.18% min 21.24 | For FCY withdrawals 1.18% min 212.4 |
| Cash Withdrawal @ Branch Counter (Either With Cheque, Deposit Slip Etc.) - HATUA ACCOUNT | One free cash withdraw per month, more than that charge will apply | 10,000 for amounts below 20M, 0.15 % of value max 118,000 for amount above 20M | For FCY withdrawals 1.18 % min 10 | NA | NA | NA |
| Cash Deposit Charge | Fee to be charged to notes below $50 | FREE | 1.77% of FCY currency below 50 note. Otherwise FREE. For all FCY currency. | FREE | FREE | FREE |
| Cheque payments to other banks | When our customer pays through Cheques to third party banks | 950.01 | 0.96 | 0.96 | 0.96 | 6.34 |
| Cheque Deposit | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Unpaid Cheque(Insuficient Fund) | Flat fee per unpaid item | 100,000.01 | 100.01 | 100.01 | 100.01 | 666.68 |
| Account Closure | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Cheque Book | | 450 | 0.46 | 0.46 | 0.46 | 3.01 |
| **CARDS AND ATM FEES** | | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Card expired | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Card New | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Card Not working | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Card compromised | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| POS Purchase ( Domestic) | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Annual card fees | UHURU BANKING | 10,000 | 10.01 | 10.01 | 10.01 | 66.67 |
| Annual card fees | PRIVATE BANKING | 30,000 | 30.01 | 30.01 | 30.01 | 200.01 |
| Secondary Card fee | | 25,000.01 | 25.00 | 25.00 | 25.00 | 166.68 |
| Card Damaged | | 25,000.01 | 25.00 | 25.00 | 25.00 | 166.68 |
| Card lost/Stolen | | 25,000.01 | 25.00 | 25.00 | 25.00 | 166.68 |
| Card Name Change | | 25,000.01 | 25.00 | 25.00 | 25.00 | 166.68 |
| Cash withdrawal @ other bank ATM (in another country) | | 8,000.01 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 53.34 |
| Internationa card access fee | | 8,000.01 | Tzs equivalent | Tzs equivalent | Tzs equivalent | Tzs equivalent |
| Uncollected cheque/CARDS fees ( Two month) | | 10,000 | 10.01 | 10.01 | 10.01 | 66.67 |
| POS Purchase ( International) | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Declined ATM cash withdrawal no funds - Stanbic/Standard Bank ATM (internationally) | | 2,500.01 | 2.50 | 2.50 | 2.50 | 16.67 |
| Cash withdrawal @ other bank ATM (in country) | | 1,000 - 400,000 = 2800<br>400,001-above=4000 | 1 - 170 = 2.8<br>171-above=4 | 1 - 170 = 2.8<br>171-above=4 | 1 - 170 = 2.8<br>171-above=4 | 1 - 2,000 = 28<br>2,001-above=40 |
| Declined ATM cash withdrawal no funds - other bank's ATM (in country) | | 1,000 | 1.00 | 1.00 | 1.00 | 6.67 |
| Balance enquiry on other Banks ATM/ CCC and at Branch | | 1,000 | 1.00 | 1.00 | 1.00 | 6.67 |
| Cash withdrawal @ own ATM (in country) | | 950.01 | 0.96 | 0.96 | 0.96 | 6.34 |
| Mini stat at own ATM | | 900.01 | 0.91 | 0.91 | 0.91 | 6.01 |
| Declined ATM cash withdrawal no funds (own ATM) | | 700.01 | 0.71 | 0.71 | 0.71 | 4.67 |
| Pin management | | 700.01 | 0.71 | 0.71 | 0.71 | 4.67 |
| Balance enquiry own ATM | | 300 | 0.31 | 0.31 | 0.31 | 2.01 |
| **USSD/WAP AND INTERNET BANKING** | | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Fee- Top-up Other | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Fee- Top-up Self | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Fee- Self Funds | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Biller Payment | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Fee-Monthly Subscription | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Bank To Wallet | | 1,000 - 25,000 =1500<br>25,001 - 100,000 = 2250<br>100,001 - 250,000 = 3000<br>250,001-500,000=3,750<br>500,000-1,000,000=4,500 | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent |
| Transfers Of Money Outside Stanbic(Express) | | 8,000.01 | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent |
| Transfers Of Money Outside Stanbic(Normal) | | 2,000.01 | 2.01 | 2.01 | 2.01 | 13.33 |
| Transfers Of Money 3rd party Within Stanbic | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Mini statement | | 500 | 0.51 | 0.51 | 0.51 | 3.34 |
| Balance Inquiry( wap and ussd charged) | | 350.01 | 0.35 | 0.35 | 0.35 | 2.34 |
| **OTHER FEES** | | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Statement (Monthly) OTC | | 1,000 | 1.00 | 1.00 | 1.00 | 6.67 |
| E statement | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| MT940 | Monthly Statement | 75,000.01 | 75.00 | 75.00 | 75.00 | 500.00 |
| Interim Statement (Over The Counter)( More Than One Month But Not Exceed 3 Month) | | 5,000 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 33.34 |
| Certificate of Balance | | 42,000.01 | 42.01 | 42.01 | 42.01 | 280.00 |
| Introduction letters (international banks) | | 55,000 | 55.01 | 55.01 | 55.01 | 366.67 |
| Certificate covering interest paid | | 55,000 | 55.01 | 55.01 | 55.01 | 366.67 |
| Certificate of Balance | | 42,000.01 | 42.01 | 42.01 | 42.01 | 280.00 |
| Confirmation Auditor List | | 130,000.01 | 130.00 | 130.00 | 130.00 | 866.67 |
| Search Fees For Copies | | 60,000 | 60.00 | 60.00 | 60.00 | 400.01 |
| Fee- OTC History Statements | | 60,000 | 60.00 | 60.00 | 60.00 | 400.01 |
| **PAYMENTS** | | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Salary Payments EFT - Manual | per person | 5,000 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 33.34 |
| Salary for TISS - Manual | per person | 10,000 | Tzs equivalent | Tzs equivalent | Tzs equivalent | Tzs equivalent |
| Fee- Standing Instruction | SI ESTABLISHMENT | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Fee-Standing Order Amendment | SI AMMENDMENT | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Basic Fee-Standing Instruction | SI THIRD PART ACCOUNT | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Basic Fee-Standing Instruction | SI -OTHER BANK ACCOUNT | 40,000.01 | 40.00 | 40.00 | 40.00 | 266.67 |
| Basic Fee-Standing Instruction | SI-OWN ACCOUNT | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Basic Fee-Standing Instruction | SI-UNPAID STANDING ORDER (FAILURE) | 50,000.01 | 50.01 | 50.01 | 50.01 | 333.34 |
| Stop Payment Orders | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Fee-Inter Account Transfer(3Rd Party) OTC | | 5,000 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 33.34 |
| Bank Cheque Issued | | 40,120 | 40.12 | 40.12 | 40.12 | 267.47 |
| Counter Cheque (OTC) | | 15,000 | 15.00 | 15.00 | 15.00 | 100.00 |

# Bosi LHRC awapa somo wabunge

**Na Salome Kitomari**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, amewashauri wabunge kutokufanya kazi kwa kuangalia mtazamo wa kisiasa bali athari ya jambo wanalolipitisha.

Akihojiwa na chombo kimoja cha habari kuhusu maoni yake kama mtetezi wa haki za binadamu, alisema hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ilipelekwa bungeni na baada ya kusomwa ilipigwa kura ya ndiyo na hapana.

"Najua ilipigiwa kura wakasema ndiyo kwa vile chama chetu kinaangalia hivi. Chama kimoja kina watu wengi bungeni, lakini athari ni kubwa mno, nia njema ya serikali kuondoa ufisadi itaondoka," alisema.

Alisema kwa mazingira hayo, watu watafanya ufisadi bila woga kwa kuwa anajua hakaguliwi na hata akikaguliwa taarifa haijadiliwi kwa uwazi kwa kuwa haiendi bunge.

"Fedha nyingi zitapotea kwa sababu hakuna uwajibikaji na nchi kwenda na Katiba na maana yake hakuna utawala wa sheria na kila mtu atafanya atakacho na tutarudi nyuma kimaendeleo na haki za binadamu hazitakuwapo," alisema.

Henga alisema kuna njia mbalimbali za kufanyika kama kwenda mahakamani kuhoji maamuzi ya wabunge au kuwaandikia wabunge kama wanakubaliana na uamuzi huo na kama wanajua athari zake.

Henga alisema kitendo cha kusema hatashirikiana na CAG, ni kugaragazwa kwa katiba ya nchi kwa kuwa nafasi hiyo ipo kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba.

"Kutakuwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo itakuwa na majukumu ya kusimamia fedha za wananchi zinazotolewa kutumika kwa mambo mbalimbali, na huyo CAG haripoti kwa bunge bali kwa Rais na anakwenda bungeni kuisoma, alafu bunge linaichambua na utekelezaji," alisema.

Kwa mujibu wa Henga, kusema hawafanyi kazi naye ni kuvunja muhimili wa serikali kusimamia fedha zake na wananchi waliowachagua wabunge ili wasimamie fedha zao na kuvunja haki za wananchi na kukwepa uwajibikaji.

Wiki iliyopita, Bunge lilipitisha uamuzi wa kutokufanyakazi na CAG kwa kuwa alihojiwa na mwandishi wa habari akiwa Marekani na kusema bunge ni dhaifu.

Siku chache baadaye, Spika Job Ndugai, alifafanua kuwa Bunge limekataa kufanyakazi na Prof. Mussa Assad na si ofisi ya CAG kwa kuwa amekataa kuondoa maneno dhaifu ambayo yanalidhalilisha bunge hilo.

## Polisi yaua majambazi watano Tanga

**Na Mwandishi Wetu**

WATU watano wanaodhaniwa kuwa majambazi wameuawa na Jeshi la Polisi mkoani Tanga, baada ya kutokea kwa majibizano ya risasi wilayani Korogwe.

Tukio hilo lilitokea jana wakati watu hao wakitaka kufanya uporaji kwenye mashamba ya mkonge ya Torotho.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo eneo la darajani kwenye mji mdogo wa Mombo.

Kamanda Bukombe alisema watuhumiwa hao pia walikutwa na tunguli ambazo walikuwa wakizitumia katika matukio hayo.

"Hizi ni tunguli ambazo tumekuta wamezivaa ambazo wao wanaamini zinawasaidia kujilinda ili wasiingie kwenye mikono ya vyombo vyetu vya dola," alisema Bukombe.

Aidha, katika tukio hilo polisi pia wamekamata silaha mbalimbali ikiwamo bunduki aina ya shotgun na bastola iliyotengenezwa kienyeji.

Kamanda Bukombe alisema miili ya watu hao imehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Korogwe mkoani humo.


| INTERNATIONAL BUSINESS CENTRE | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **INWARD PAYMENT** | | | | | | |
| Telegraphic Transfer/SWIFT | | $ 10 | $10 | | | |
| Drafts/Bills (Clean Bill Collection) | | $150 | $150 | | | |
| Bills and drafts negotiated and subsequently returned unpaid | | $150 | $150 | | | |
| **OUTWARD PAYMENTS** | | | | | | |
| SWIFT Charges for tracing remittances | | $50 | $50 | | | |
| Telegraphic Transfer/SWIFT | Oversee charge is charged depending on made of payment customer has choose. | 0.3% of Value Min $50, Max 150 (excluding oversee charge of $29.5) | 0.3% of Value Min $50, Max 150 (excluding oversee charge of $29.5) | | | |
| Cancellation of TT/Recall of funds | | $75 | $75 | | | |
| Amendment TT | | $75 | $75 | | | |
| Transfers though TISS | | TZS10 000 | Equiv 10 000 | | | |
| MT101 Issuance | | 10,000.00 | 1.18% of the amount min $59, Max $236 | 1.18% of the amount min 50, Max $200 | 1.18% of the amount min 40, Max 160 | 1.18% of the amount min 560, Max 2240 |
| Drafts/Bills/Cheques | | 1.18% of the amount min 100 000, Max 400,000 | 1.18% of the amount min $59, Max $236 | 1.18% of the amount min 50, Max $200 | 1.18% of the amount min 40, Max 160 | 1.18% of the amount min 560, Max 2240 |
| **BILLS FOR COLLECTION** | | | | | | |
| **OUTWARD** | | | | | | |
| Documentary Bills for collection (Payment) | | SWIFT charge $35 | SWIFT charge $35 | | | |
| Doc handling fee | | $150 | $150 | | | |
| Courier Services | | $50 | $50 | | | |
| Tracer Fees | | $50 | $50 | | | |
| Clean bills for collection | | $150 | $150 | | | |
| **INWARD** | | | | | | |
| Documentary Bills for collection (doc handling) | | $125 | $125 | | | |
| Clean bills for collection | | $125 | $125 | | | |
| Delivery of documents free of payments, in terms of remitting bank's instructions | | $50 | $50 | | | |
| Avalizing | | 1% min $150 however subject to adequate Security and approval | 1% min $150 however subject to adequate Security and approval | | | |
| Negotiation fee | | $50 | $50 | | | |
| Confirmation | | $50 | $50 | | | |
| Courier charges | | $50 | $50 | | | |
| **BOL** | | | | | | |
| Telegraphic Transfers | | 0.3% of Value Min 50.00, Max 150.00 | | | | |
| Local Transfers (RTGS / TISS) | BOL | 8,000.01 | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent |
| Local Transfers (EFT) | BOL | 2,000.01 | 2.01 | 2.01 | 2.01 | 13.33 |
| Internal Transfers | BOL | 1,000 | 1.00 | 1.00 | 1.00 | 6.67 |
| Payroll On-Us (Within Stanbic) | BOL | 1,000 | 1.00 | 1.00 | 1.00 | 6.67 |
| Payroll Off-Us - EFT | BOL | 2,000.01 | 2.01 | 2.01 | 2.01 | 13.33 |
| Payroll Off-Us - TISS | BOL | 8,000.01 | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent |
| Mobile Bulk Payments | BOL | 1,500.00 | 1.51 | 1.51 | 1.51 | 10.01 |
| BOL Monthly Fee | BOL | 24,000.01 | 24.00 | 24.00 | 24.00 | 160.01 |
| BOL Token Fee (One-Off) | BOL | 65,000.01 | 65.01 | 65.01 | 65.01 | 433.34 |
| Till to bank | Merchant Services | 1.8% | | | | |

Stanbic Bank Moving Forward™
A member of Standard Bank Group

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Udhibiti wizi viwanda madini uwe endelevu

**TAARIFA** kwamba Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, amevifungia viwanda vya uchenjuaji wa madini 15 vilivyopo wilayani Kahama mkoani Shinyanga, baada ya kubainika kuwapo wizi mpya wa madini kwa kutumia steel wire na kuikosesha serikali mapato, zinathibitisha kwamba bado kuna mianya ya wizi wa fedha za umma katika sekta ya madini.

Nyongo alivifungia viwanda hivyo mwishoni mwa wiki baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika viwanda hivyo na kukamata dhahabu gramu 102.9 ambayo ilikuwa katika mfumo usio rasmi.

Inaelezwa baadhi ya wamiliki wa viwanda hivyo huweka steel wire katika mabomba ya mashine za kuchujia kaboni na kuwaibia wateja wao.

Alibainisha baadhi ya watumishi wa ofisi za madini wilayani humo sio waaminifu na alibaini kuhusika kuwaibia wachimbaji wadogo katika upimaji wa dhahabu.

Uozo mwingine ambao aliubaini ni uwapo wa mizani ambazo hazijathibitishwa na Wakala wa Vipimo wa Serikali (WMA).

Kinachosikitisha ni taarifa kuwa Kaimu Meneja wa Madini Mkoa maalumu wa madini Kahama, amekuwa akikaa kimya bila kuchukua hatua dhidi ya baadhi ya wamiliki wa viwanda hivyo na kusababisha serikali kukosa mapato.

Haya yote yanathibitisha bado kuna safari ndefu katika kudhibiti wa wizi katika sekta ya madini, ambao unasababisha nchi yetu ikose mapato ya kuiletea maendeleo.

Vitendo vya wizi na udanganyifu katika viwanda vya kuchenjua madini na sekta ya madini kwa ujumla, kwa kiwango kikubwa vinachangiwa na usimamizi duni wa mamlaka zetu.

Pengine ndiyo maana Naibu Waziri Nyongo aliamua kuchukua hatua kwa kumsimamisha kazi Kaimu Meneja wa Madini Mkoa maalumu wa madini Kahama, baada ya kushindwa kusimamia vema viwanda vya uchenjuaji wa madini, hivyo kuwaibia wateja pamoja na kuikosesha kodi serikali.

Kuna umuhimu wa kuchukua hatua madhubuti na endelevu kwa lengo la kudhiti vitendo vyote vya wizi na udanganyifu katika migodi, ambavyo vinafanywa na baadhi ya wamiliki, hivyo kusababisha serikali ikose mapato yake.

Kwa kuwa vitendo hivyo pia vinawaathiri wateja wa madini wanaopeleka madini yao katika viwanda kuyauza, kwa kuwapunja madini yao, ni wakati mwafaka kuanzisha mfumo bora na wa kisasa kwa ajili ya kudhibiti shughuli za madini, ikiwamo biashara na malipo ya mapato kwa serikali.

Bila kuwekwa mfumo bora na wa kisasa katika viwanda vya kuchakata madini, serikali itaendelea kukosa mapato yake ambayo yangeiwezesha kujiendesha sambamba na kuchangia kuboresha huduma za msingi za jamii kama maji, elimu, afya na miundombinu.

Ikumbukwe kuwa viwanda vya kuchenjua madini kama havitawekewa udhibiti, hali hiyo inaweza kuwakimbiza wachimbaji wa madini wasiyapeleke huko badala yake kuyauza kwa njia ambazo zitaikosesha serikali mapato.

Tunawashauri wateja wa viwanda hivyo kuchukua hatua kwa kutoa taarifa mahali husika, wanapoona viwanda hivyo vinawaibia kwa kutumia njia za udanganyifu.

Hilo linawezekana kama mmoja wa wateja ambaye alisema baada ya kufikisha mzigo wake katika kiwanda kilichobainika kuweka steel wire, baada ya kupima kaboni zake matokeo yalionyesha atapata dhahabu nyingi, lakini baada ya kuichoma alipata kidogo na kutoa taarifa kwa maofisa wa serikali ambao waliyakata mabomba ya mashine hizo na kupata steel wire hizo zikiwa na dhahabu nyingi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com

**BUSARA**

**TUPONGEZE PANAPO PONGEZEKA**
**KUMPONGEZA MTU NI KUMPA SIFA KWA KAZI NJEMA ALIYOIFANYA. KIMSINGI MTU HAPONGEZWI KWA KUTENDA MABAYA BALI HULAANIWA. HATA HIVYO TUSIWE WACHOYO WA KUPONGEZA PALE PANAPOSTAHILI KUPONGEZA. KUPONGEZA NI KUTOA MOTISHA NA MWELEKEO WA DIRA NJEMA.** NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Raphael Kibiriti

# TRC, Polisi lisimamieni hili kuepusha janga la maafa

**KUNA** sekta nyingi zilizo muhimu kukuza uchumi wa mtu na taifa kwa ujumla wake.

Mojawapo ya sekta hizo ni ya usafiri ambayo huongeza tija katika uzalishaji na mifumo ya malighafi au masoko. Sekta hii inaundwa na usafiri wa nchi kavu, majini na angani.

Kwa upande wa nchi kavu, usafiri wa treni ndio ulio rahisi na salama kwa ajili ya kusafirisha abiria na mizigo kwenda maeneo tofauti, yawe ya mbali au ya karibu.

Hii ni kwa sababu pamoja na mambo mengine una njia isiyoingiliwa na vyombo vingine vya usafiri.

Na ndiyo maana katika maeneo ambayo kuna makutano ya barabara na reli, kuna geti ambalo hufungwa ili kuzuia magari na vyombo vingine vya usafiri wakati treni ikipita.

Aidha, treni hupiga honi kama tahadhari kwa sababu yenyewe haina utaratibu wa kufunga breki kupisha gari au chombo kingine cha usafiri.

Tuna matukio ambapo gari zimegonga treni kwa maana ya kugongwa na treni kwa sababu ya kupita kwenye makutano ya barabara na reli bila ya kusimama wakati treni ikipita.

Na matokeo yake tumeona kuwa gari hizo zimeshtakiwa kwa kugonga treni kisheria pamoja na kwamba ndizo zilizogongwa.

Hivyo nchi ambazo zimeboresha usafiri wa reli kama ilivyo katika mataifa kama ya Marekani, Ulaya na baadhi ya nchi za Asia, zina uchumi imara.

Katika mataifa hayo, watu wengi hutegemea kwa kiasi kikubwa usafiri wa reli kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Kuna treni za mwendokasi ambazo huchukua muda mfupi kusafiri umbali mrefu.

Na ndivyo itakavyokuwa kwa treni ya mwendokasi ya 'Dk. John Magufuli' baada ya kukamilika kwa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (standard gauge) kutoka Dar es Salaam hadi mwanza, itakayosafiri kilometa 160 kwa saa kwa taarifa zilizopo.

Pamoja na hilo, Jiji la Dar es Salaam tayari lina mtandao wa usafiri wa treni zinazosafirisha abiria unaosimamiwa na Shirika la Reli nchini (TRC).

Mtandao huo una treni zinazoanzia eneo la stesheni ama Kamata kwa hivi sasa kwenda Ubungo na Gongo la Mboto na Pugu.

Usafiri huu kwa kiasi kikubwa umekuwa mkombozi kwa wakazi wengi wa jiji wanaoishi katika maeneo ambayo treni hizo hupita.

Hata hivyo, wakati Muungwana akitoa pongezi kwa TRC kuwa na usafiri huu jijini ambao umesaidia wengi wakiwamo wanafunzi kwenda na kurudi shuleni, kuna mambo ya kurekebisha ambayo shirika linapaswa kuyafanyia kazi mara moja.

Mwanzoni mwa mwezi Machi mwaka huu, Muungwana alisafiri kwa treni akitokea Dar es Salaam kwenda Mpanda, mkoani Katavi.

Siku aliyokwenda kukata tiketi na siku aliyosafiri alishuhudia namna baadhi ya abiria wa treni hizi wakiwamo wanafunzi wasivyochukua tahadhari juu ya usalama wa maisha yao.

Aliona abiria waliokuwa wamekaa katikati ya reli pale stesheni Kamata wakisubiri kupanda treni hizi badala ya kukaa kwenye eneo maalumu la abiria wanaosubiri muda ufike wa kupanda treni hizo.

Lakini pia Muungwana alishuhudia abiria ambao kwa makusudi kabisa hawapandi kwenye treni hizo baada ya kutangaziwa kabla, muda wa treni kuondoka.

Na badala yake abiria hao walikimbilia kudandia kwenye treni hizi pale zilipoanza kuondoka.

Mbaya zaidi katika kundi hili walikuwapo pia wanafunzi, wakiwamo wa kike ambao Muungwana anaamini ni wazuri kwa kufuata maelekezo yanayotolewa tofauti na ilivyo kwa wengine.

Na kwa masikitiko makubwa ya Muungwana ni kwamba haya yalitendeka mbele ya macho ya maofisa wa TRC na polisi wanaosimamia usalama wa abiria na mali.

Ni maoni ya Muungwana kwa TRC na Jeshi la Polisi kusimamia kwa ukamilifu suala hili ambalo linaweza likasababisha majanga ya upotevu wa maisha kwa abiria wanaotumia usafiri huu, lakini pia wa mali.

# Sumatra yafungia mabasi ma3 kwa kuingilia mfumo

**Na Beatrice Moses**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (Sumatra) imeyafungia leseni za usafirishaji abiria mabasi matatu ya kampuni mbili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mhandisi Lameck Kamando kwa niaba ya Mkurugenzi wa Sumatra, imeeleza kuwa hatua hiyo imechukuliwa baada ya kubainika mabasi hayo yameingiliwa mfumo wa ufuatiliaji mwendo wa mabasi(VTS).

Kamando ameeleza katika taarifa hiyo kwamba leseni hizo zimesitishwa kwa muda wa siku 30, kwa kuwa walichokifanya ni kinyume na taratibu zilizowekwa.

"Adhabu hii imetolewa baada ya wahusika kupewa fursa ya kujieleza, lakini hawakutoa maelezo ya kujitosheleza."

Imeelezwa kuwa utekelezaji huo ni kwa mujibu wa kifungu namba 15 cha Sheria za Sumatra ya mwaka 2001 na namba 28(1)(b) ya Leseni za Usafirishaji (usafiri wa umma)2017.

Mabasi hayo yametajwa kuwa ni Super Sami T203 DHM, lingine ni lenye namba T204 DHM na basi la kampuni ya Sanlait Friends Uganda lenye namba UAZ 076 P.

Katika taarifa hiyo mamlaka hiyo imesisitiza kuwa inaendelea kuchukua hatua kwa wasafirishaji wanaokiuka masharti ya leseni na usafirishaji.

Adhabu nyingine ni pamoja na kufuta leseni kwa wanaofanya vitendo vinavyoweza kuhatarisha usalama wa abiria na watumiaji wengine wa barabara.

Akizungumza kuhusu hatua hiyo, Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa Sumatra, Salum Pazzi, alisema jumla ya mabasi 10 yamefungiwa tangu Januari hadi Machi mwaka huu.

"Kuingilia mfumo wa kufuatilia mwendo ni sawa na kujificha ili gari lisifuatiliwe, hivyo linaweza kuendeshwa kwa mwendo mkali unaoweza kusababisha ajali," alisema.

Alisema ajali za mabasi husika kwenda kasi zimesababisha watu kadhaa kupoteza maisha na wengine kujeruhiwa na kupata ulemavu wa maisha.



Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, akizungumza baada ya kipindi cha maswali na majibu kumalizika katika kikao cha tano Bunge la 15 jana, bungeni jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Repoa kukutanisha watafiti wa uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Utafiti ya Kuondoa Umaskini (Repoa), imeandaa mkutano wa 24 unaotarajia kuwakutanisha wataalamu wa masuala ya utafiti, maofisa wa serikali na wadau wa maendelea kujadili masuala mbalimbali yanayohusu serikali za mitaa.

Mkutano huo ambao unatarajia kufanyika kesho jijini Dar es Salaam, utahusisha watoa mada 11, ambazo zinalenga kujadili kwa kina masuala yanayohusu serikali za mitaa ikiwamo kupata uzoefu wa nchi zingine ambazo zimepiga hatua katika eneo hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Repoa, Dk. Donald Mmari, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, huku akisisitiza kuwa mwaka huu watajikita kuangalia mchango wa serikali za mitaa na fursa za uchumi na namna zinavyoweza kubadilisha maisha ya wananchi wa kawaida.

Alisema mkutano huo wa siku mbili utatoa fursa kwa wadau mbalimbali wakiwamo watunga sera kusikia wataalamu wa masuala ya uchumi.

"Tutajadili halmashauri zinavyoweza kusaidia kuboresha wananchi wa kawaida, uchumi wetu inaonekana unakuwa, maeneo mengi ikiwamo sekta ya mawasiliano inayokuwa bado imeajiri idadi ndogo ya wananchi," alisema.

Alisema washiriki watapendekeza namna bora ama njia nzuri ya kukuza uchumi kwa ngazi ya vijiji na kata.

**"Tutajadili halmashauri zinavyoweza kusaidia kuboresha wananchi wa kawaida, uchumi wetu inaonekana unakuwa, maeneo mengi ikiwamo sekta ya mawasiliano inayokuwa bado...**

# Jela miaka minne wizi bodaboda

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma imemhukumu mkazi wa Bangwe Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Francis Mugisha (32), kutumikia kifungo cha miaka minne jela kwa kosa la kuiba pikipiki.

Mbali na hukumu hiyo, imemwamuru Mugisha akimaliza kifungo chake, amlipe mlalamikaji, Emmanuel Mweta, Sh. milioni 2.4 ambazo ni thamani ya chombo hicho.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Frederick Shayo, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo bila shaka.

Hakimu Shayo alisema mahakama imatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na kwa vijana wengine wenye tabia ya wizi kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka hapo mahakamani mashahidi wanne na vielelezo vitatu ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa aliiba pikipiki hiyo.

Hakimu Shayo alisema baada ya kuangalia ushahidi wa pande zote, imeonyesha kuwa mshtakiwa aliiba pikipiki hiyo kwa makusudi kwa sababu mshtakiwa hawezi kulala sehemu nyingine na pikipiki sehemu nyingine tena kwenye nyumba ambayo mlango wake ni mbovu. Alisema yote hiyo ilikuwa njama ya kuiba pikipiki hiyo.

"Ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka umethibitisha bila kuwa na shaka, hivyo mahakama hii inakutia hatiani kwa kosa ulilosht akiwa nalo. Pia mahakama hii inakutaka ujitetee ili kukupunguzia adhabu," alisema Hakimu Shayo.

Baada ya kupewa nafasi hiyo, mshtakiwa alijitetea kuwa anaomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ana familia inamtegemea kisha akaangua kilio.

Hata hivyo, Hakimu Shayo alitupilia mbali utetezi huo na kusema: "Mshtakiwa kitendo ulichokifanya cha kuiba pikipiki ambayo umepewa ili ufanyie kazi kisha unaiba inaonyesha kuwa wewe ni mzoefu wa wizi, hivyo mahakama hii inakuhukumu kwenda jela miaka minne na ukimaliza kifungo chako hicho utamlipa mwenye pikipiki hiyo Sh. milioni 2.4. Hapo utakuwa umejifunza namna ya kuishi na jamii."

Awali, akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Edina Makala, alidai kuwa Januari 6, mwaka jana, majira ya asubuhi eneo la Bangwe Mji Mpya katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji, mshtakiwa aliiba pikipiki yenye namba za usajili MC 503 AXH aina ya Kinglion yenye thamani ya Sh. milioni 2.4 mali ya Emmanuel Mweta ambayo alimkabidhi kwa lengo la kufanyia biashara ya bodaboda.

# Mbunge ataka kusiwe na uchaguzi

INATOKA UK 2

bea na kumtikisa au kumshinda katika uchaguzi ujao.

"Mshindi namba mbili 'ulipo tupo' (akimaanisha Edward Lowassa) tayari yuko kulekule na wengine wamemfuata hukohuko, hivi kuna chama katika nchi hii kinaweza kumtengeneza mgombea urais ndani ya miezi tisa na akamshinda Rais Magufuli? Haiwezekani!

"Hakuna mtu atakayegombea 2020 si tu akamshinda, bali hata kumtikisa Rais Magufuli, badala yake tuje kushindana kwenye ubunge na udiwani. Amefanya kazi kubwa, tumpe heshima, hii ni Katiba ya kwetu, changamoto ni zetu, naruhusu mjadala wa hili," Lusinde alisema.

Mbunge wa Babati Mjini, Paulina Gekul (CCM), alisema alipokuwa upinzani alihoji Tanzania ni nchi ya aina gani ambayo haina hata ndege ya kuazima, lakini sasa kilio chake hicho kimesikika.

"Kwenye bajeti iliyopita nilikuwa mkali sana, miaka mitano iliyopita nikiwa mbunge wa viti maalum na nilivyokuwa mbunge wa jimbo, nimekuwa nikichangia sana suala la Tanzania kuwa na ndege zetu.

"Leo (jana) nitazungumza tofauti na nilivyokuwa naongea wakati nilipokuwa Ukanda wa Gaza. Kazi kubwa inayofanywa na serikali inayoongozwa na Rais Magufuli ya kuhakikisha taifa linakuwa na ndege, napongeza kwa sababu limetuletea heshima kama taifa. Watu hawasemi lakini kipato kinaongezeka na watalii wanaongezeka," alisema.

Mbunge huyo alisema Rais Magufuli pia ameonyesha uzalendo kutokana na uamuzi wake wa kubadili matumizi ya ndege iliyokuwa ikiwabeba viongozi kuwa ya abiria.

"Tuwe wakweli suala la barabara na madaraja ambayo hayajajengwa, barabara za kuunganisha mikoa na ukienda Dar es Salaam unakutana na ujenzi wa barabara ya njia nne kwenda, nne kurudi. Rais amekuwa anafanya mambo ambayo hayajafanyika, na tusipoyasema hata Mungu atatushangaa," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum, Gimbi Masaba (Chadema), alisema Serikali Kuu imeshindwa kukusanya mapato vizuri huku ikizitaka mamlaka ya serikali za mitaa kukusanya na kutumia mapato yao.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema haya kwa masikitiko makubwa sana kwa sababu wakati mapato yakikusanywa na halmashauri zenyewe zilikuwa na uwezo wa kujiendesha, halmashauri hizi leo zimeshindwa kujiendesha kwa sababu kwanza nyie wenyewe mmeingiza hasara kwenye ukusanyaji wa mapato," alisema.

Naomba na nasisitiza kweli kweli, serikali rudisheni makusanyo kwenye halmashauri zetu ili ziweze kujiendesha," Msaba alisema huku akiitaka serikali kuhakikisha inatoa fedha zinazotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji.

Katika mchango wake, Mbunge wa Sengerema, William Ngeleja (CCM), aliitaka serikali kuimarisha utungaji wa sheria ndogo ili kuepusha kuwaumiza wananchi katika utekelezaji wake.

"Kuna umuhimu mkubwa sana wa kuimarishwa utungwaji wa sheria ndogo, ushahidi uliopo ni kuwa asilimia 75 zina dosari na bila kuwa na jicho la Bunge, wananchi wengi wangeumia," alisema.

Ngeleja pia aliishauri serikali kuimarisha na kuipa nguvu sekta binafsi ili isaidie kuchangia ajira kwa Watanzania.

"Takwimu za sasa utaona sekta ya umma imechangia ajira kwa asilimia 66 na sekta binafsi wastani wa asilimia 34, lakini serikali ina miradi ambayo wakati mwingine inafikia ukomo, sasa uimarishwaji wa sekta binafsi utasaidia kuchochea ajira," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum, Lucy Owenya (Chadema), alisema serikali imekuwa ikilipa mara tatu ya gharama ya matengenezo ya magari yake kutokana na Wakala wa Ufundi na Umeme kukosa vifaa vya kisasa.

"Ili kupunguza matumizi, wahakikishe wanaweka vifaa vya kisasa. Tamesa wanapeleka kwenye gereji nyingine ambazo bili inakuwa mara tatu," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum, Grace Tendege (Chadema), aliitaka serikali kuchukua hatua kukabiliana na changamoto ya lishe na udumavu ili kuwa na taifa bora, akieleza kuwa changamoto hiyo hiyo ni kubwa nchini.

Mbunge huyo alisema hata wabunge hawajui wale nini ili kuwa na lishe bora, hivyo kuna haja elimu ya lishe itolewe kwa makundi yote.

Mbunge wa Bunda Vijijini, Boniphace Getere (CCM), alisema anaishangaa serikali kutenga Sh. bilioni tisa kwa ajili ya kuua viumbe na wanyama waharibifu wa mazao wakiwamo panya badala ya kusaka soko la wanyama hao nje ya nchi.

Alisema kuna soko la mende Brazil huku pia Malaysia ikinunua kwa wiki vipepeo, hivyo kuna haja serikali kuuza viumbe hai hao ughaibuni na kutengeneza ajira nchini.

Mbunge wa Wawi, Ahmes Juma Ngwali (CUF), alisema hali ya uwekezaji nchini ni mbaya kutokana na ugumu wa upatikanaji wa vibali vya kuwekeza na utitiri wa kodi.



Mkurugenzi Ofisi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) Zanzibar, Felix Wandwe, akiweka shada la maua kwenye kaburi la aliyekuwa mtumishi wa tume hiyo na mwanahabari marehemu Clarence Nanyaro, aliyezikwa kijijini kwao, Nkomaala, wilayani Meru mkoa wa Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEC**




## Sakata la CAG moto bungeni

INATOKA UK 2

kujua kutafsiri katiba, amekuja kunukuu vifungu vya Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini hakwenda mbali zaidi kusoma sheria zingine zinazoambatana na maagizo hayo ya kikatiba na sheria katika kufanya tafsiri za siku ambazo zimeandikwa kwenye katiba na sheria husika na uwasilishaji wa ripoti ya CAG na hasa Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

"Mheshimiwa mbunge anataka kuonyesha wazi kama serikali haitaki kuwajibika. Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako linapotokea jambo kama hili, kiti chako kipo tayari kumtafsiria Mnyika tafsiri ya sheria hizo zote ili asiendelee kulipotosha Bunge na akatuacha serikali tuendelee kujipanga kwa kuzingatia sheria na taratibu husika katika utekelezaji wa jambo hili?" Mhagama aliomba.

**KAULI YA CHENGE**

Katika mwongozo wake kwa wawili hao, Mwenyekiti wa Bunge, Andrew Chenge, aliyekuwa anaongoza kikao cha jana, alisema kuna haja sheria aliyoinukuu Mnyika bungeni isomwe kwa pamoja na sheria nyingine zenye uhusiano nayo.

Chenge ambaye aliwahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), alisema serikali haijakiuka katiba na sheria katika uwasilishaji wa ripoti ya ukaguzi wa CAG.

"Katiba kama ulivyoisoma, lazima uisome na sheria nyingine na moja inayotuongoza ni sheria ya tasfiri za maneno yote ambayo yametumika kwenye sheria, sura namba moja ndiyo inayotumika.

"Kwa hiyo, kwanza lenyewe halikutokea bungeni, 'order paper' (karatasi yenye orodha ya shughuli za kikao cha Bunge) hakuna kitu kama hicho.

"Nakusihi sana uende ukasome Sheria ya Tafsiri inapoeleza siku. Serikali haijaenda nje ya utaratibu unaotakiwa kwa mujibu wa katiba," Chenge alisema.

**KAULI YA NAIBU SPIKA**

Nje ya ukumbi wa Bunge, Nipashe ilizungumza na Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ambaye alisema hana taarifa za uwasilishwaji wa ripoti ya ukaguzi wa CAG kwa mwaka wa fedha 2017/18.

Nipashe ilihitaji kujua kama ripoti hiyo imeshawasilishwa bungeni kwa kuwa serikali inapaswa kufanya hivyo ndani ya siku saba ambazo zitakoma keshokutwa (Jumatano).

Jumanne iliyopita, Bunge liliazimia kutofanya kazi na CAG, Prof. Juma Assad, baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kumtia hatiani kwa kudharau, kudhalilisha na kushusha heshima na hadhi ya chombo hicho cha kutunga sheria kutokana na kauli yake ya mwanzoni mwaka huu Newyork, Marekani kwamba anafikiri "huo ni udhaifu wa Bunge".

Tangu kupitishwa kwa azimio hilo, kumekuwa na sintofahamu ya namna ambavyo ripoti ya ukaguzi wa CAG kwa mwaka 2017/18 itawasilishwa bungeni.

Hata hivyo, tayari Spika Job Ndugai imeshaweka wazi kuwa wako tayari kufanya kazi na maofisa wa CAG, lakini si mtu anayeitwa Prof. Mussa Assad, ambaye ndiye CAG na Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mujibu wa katiba.

# Mongella ataja viongozi wanaowafaa wanawake

**Na Mary Geofrey**

RAIS mstaafu wa Bunge la Afrika, Getrude Mongella, amesema kuelekea uchaguzi mkuu wa mwakani, Watanzania wanapaswa kuwachagua viongozi watakaotoa ajenda zinazowatambua na kuwathamini wanawake.

Amesema mgombea atakayewaona wanawake kama vitendea kazi ilhali ndio wachangiaji wa ukuzaji wa uchumi wa viwanda, hawatakiwi kupewa nafasi ya kuongoza nafasi yoyote nchini.

Mongella alitoa angalizo hilo Dar es Salaam wakati akizungumza katika utoaji tuzo za Malkia wa Nguvu, zilizoandaliwa na kutolewa na Clouds Media Group, jumla ya wanawake 20 walipewa tuzo za kutambua mchango wao ndani ya jamii.

Mongella alisema mataifa mengi duniani yamesonga mbele bila nguvu ya wanawake, lakini kwa Tanzania haiwezekani kwa sababu wanawake ndio washika uchumi na nguvu ya uzalishaji.

"Uchaguzi unakuja, ajenda zinazotolewa na wagombea lazima zitambue thamani na nafasi ya mwanamke ndani ya jamii. Kama mgombea ataona wanawake kama vitendea kazi huyu hatufai na hana sababu ya kuchaguliwa kwa sababu asilimia kubwa wanawake ndio wazalishaji wa uchumi wa taifa hili hivyo wanapaswa kutambuliwa," Mongella alisema.

Aidha, aliwasihi wanawake waliopewa tuzo za Malkia wa Nguvu, kuwa chachu ya kuwainua na kuwandaa wanawake wengi 10 kila mmoja katika kipengele cha tuzo yake.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alisema wanawake wanapita katika mapito magumu hata kufikia hatua ya kususiwa watoto na kuwataka wasikate tamaa kwa sababu mafanikio yao yapo njiani.

Makonda pia aliahidi kumpatia gari la kubeba wanafunzi, mshindi wa Tuzo ya Heshima ya Malkia wa Nguvu iliyochukuliwa na Robi Samwel ambaye analea na kuwasomesha watoto wa kike wanaokimbia kukeketwa mkoani Mara.

Akizungumzia ushindi wake, Robi alisema tuzo hiyo ameichukua kwa niaba ya mangariba walioacha kukeketa na wasichana wanaokataa na kupinga vitendo vya ukeketaji nchini.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya utengenezaji wa samani za ndani na maofisini ya Amorette, Jacqueline Mengi, aliwataka wanawake nchini kuiga mfano wa waliochukua tuzo hizo na kutokubali kukata tamaa.

Jacqueline ambaye alikabidhi tuzo ya Sayansi na Teknolojia kwa Mahinda Waziri na Sophia Abeil, aliwataka wanawake kuendelea kujituma na kujiamini.

Kwa upande wa tuzo ya Malkia anayetoa hamasa, ilichukuliwa na Faraja Kota, kupitia mradi wake wa Shule Direct, inayosambaza vitabu shuleni.

Tuzo ya kilimo na biashara ilienda kwa mfanyabiashara na mfugaji wa vifaranga, Elizabeth Swai. anayetotolesha vifaranga vya kuku 8,000 kwa siku.

Tuzo ya malkia ajaye ilienda kwa Jesca Mshama na tuzo ya burudani Lea Mwandamseke ambaye ni mwongozaji wa filamu na Asha Baraka ambaye ni mmiliki wa bendi ya Twanga Pepeta.

Kwa upande wa tuzo la biashara ya mauzo ya rejareja, ilichukuliwa na Leila Hassan na Mhandisi Anna Njavike; kipengele cha urembo na mitindo, zilichukuliwa na Miriam Odemba na Asia Idarusi.

Tuzo ya afya ilichukuliwa na Vicky Mtetema ambaye ni mwandishi mkongwe wa kwanza kuripoti wauaji wa watu wenye ualbino na Aunt Sadaka ambaye ni mshauri wa Saikolojia.



Gari likitoa msaada kwa kulivuta lililopata ajali na kuingia mtaroni baada ya kugongana katika eneo la Tangi Bovu jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mbaroni tuhuma wizi wa mtoto

**Na Ndalike Sonda, KAHAMA**

JESHI la Polisi wilayani Kahama mkoani Shinyanga linamshikilia mkazi wa Matejoo mkoani Arusha, Teddy Stephano (26), ambaye anatuhumiwa kuiba mtoto mwenye jinsi ya kiume anayekadiriwa kuwa na umri wa miezi sita.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Richard Abwao, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa juzi jioni na askari waliokuwa doria katika mtaa wa Igomelo na kwamba mtuhumiwa alikiri kosa hilo kwa kusema amefanya hivyo kutokana na tatizo la kupata mtoto.

Kamanda Abwao alisema mtoto huyo amepelekwa katika kituo cha kulelea watoto yatima Mjini Kahama kumsubiri mzazi wake na kwamba Jeshi la Polisi mkoani Arusha tayari limeshajulishwa ili kumchukua mtuhumiwa kwa hatua zaidi mkoani humo.

Aliwataka pia wananchi hasa wazazi kuwa waangalifu na watoto wao na wasiwaachie watoto wadogo kuwalea au kucheza nao.

## Majaliwa ahimiza amani, mshikamano

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania kudumisha amani, umoja na mshikamano ambavyo ni tunu walizoachiwa na waasisi wa Taifa.

Aliyasema hayo juzi katika kumbukumbu ya miaka 25 ya mauaji ya Kimbari iliyofanyika katika Jiji la Kigali nchini Rwanda. Waziri Mkuu ambaye amemwakilisha Rais John Magufuli katika kumbukumbu hizo, amewasisitiza Watanzania kudumisha amani na utulivu.

Awali Waziri Mkuu alijumuika na viongozi kutoka nchi mbalimbali kutoa heshima kwenye eneo la kumbukumbu ya mauaji hayo la Gisozi, jijini Kigali.

Baada ya kutoa heshima kwenye eneo la kumbukumbu za mauaji hayo, Rais wa Rwanda, Paul Kagame, alitoa maelezo ya kina kuhusu mauaji hayo yaliyotokea Rwanda 1994.

Viongozi wengine waliohudhuria kumbukumbu hizo ni pamoja na Rais mstaafu, Benjamin Mkapa na Rais mstaafu wa Nigeria, Ulusegun Obasanjo.

## TFS: Upandaji miti jukumu letu sote

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), umeitaka jamii kuondokana na dhana ya kuiachia serikali pekee jukumu la upandaji miti na utunzaji wa mazingira.

Kauli hiyo ilitolewa na Meneja wa TFS Wilaya ya Kinondoni, Dotto Ndumbikwa, wakati wa kupanda miti katika Chuo cha Ulinzi cha Taifa Kunduchi jijini Dar es Salaam, kazi iliyofanywa na wanachuo kwa kushirikiana na wakala huo.

Ndumbikwa alisema pamoja na juhudi mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanywa na serikali katika utunzaji mazingira, bado kumekuwapo na dhana potofu kwa jamii ya kutokuona umuhimu wa kutunza mazingira hayo. "Ipo dhana ambayo jamii bado imeendelea kuishikilia, kwamba suala la kutunza mazingira ni la serikali peke yake, tumekuwa tukijitahidi kutoa elimu, lakini bado hali hiyo ipo," alisema na kuongeza:

"Jamii haijui umuhimu wake na ndiyo maana hata miti inayopandwa na serikali watu huwa hawaoni shida kuikata. Ifike mahali Watanzania tubadilike, hali ya utunzaji wa mazingira haifurahishi na hii inatokana kwamba jukumu hilo ni la watu fulani."

Kanali Furahisha Ntahema ambaye ni Katibu wa Chuo hicho, alisema kazi ya kupanda miti na kutunza mazingira inatakiwa iwe endelevu si kwa taasisi za serikali pekee bali na kwa jamii nzima ili kuboresha mazingira katika nchi. Pia alitoa wito kwa Watanzania, kuachana na tabia ya kukata miti na badala yake kujijengea tabia ya kupanda na kutunza mazingira yanayowazunguka.

HABARI BUNGENI

## Julai Mosi mwisho mifuko ya plastiki

OFISI ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), imesema inawezekana Julai Mosi mwaka huu ndio mwisho wa matumizi ya mifuko ya plastiki.

Aidha, kanuni za utekelezaji wa sheria ya kuzuia mifuko hiyo zipo tayari zinasubiri kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Kauli hiyo ilitolewa bungeni jana na Waziri wa Wizara hiyo, January Makamba, alipokuwa akiongezea majibu ya maswali yaliyoulizwa na Mbunge wa Kaliua (CUF), Magdalena Sakaya, ambaye alihoji mkakati wa serikali wa kuzuia matumizi ya mifuko hiyo.

Waziri huyo alisema katika hotuba ya bajeti ya ofisi hiyo Aprili 16, mwaka huu, itatangaza hatua hiyo na ndani ya wiki hii ofisi hiyo itakutana na taasisi za serikali zinazohusika na jambo hilo ili kuweka utaratibu wa kupiga marufuku.

"Tumetengeneza kanuni zinangoja kuchapishwa kwenye gazeti la serikali na ni jambo tunalolichukulia kwa uzito mbadala upo na uwezekana," alisema.

Katika swali la msingi, Sakaya alihoji serikali ina mkakati gani wa kuondoa matumizi ya plastiki hapa nchini kwa kuwa yamekuwa na athari kubwa kwenye uharibifu wa mazingira.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri, Mussa Sima, alikiri kuwa matumizi ya mifuko hiyo yameongezeka hasa kutokana na mifuko hiyo kutolewa bure kwenye maduka, masoko, migahawa na maeneo mbalimbali.

Aidha, alisema kutokana na baadhi ya nchi jirani kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki na kuruhusu uzalishaji kwa ajili ya soko la nje ya nchi, kumekuwa na wimbi kubwa la uingizaji wa mifuko hiyo nchini.

Alisema serikali inadhamiria kusitisha uzalishaji na matumizi ya mifuko hiyo katika siku zijazo.

Hata hivyo alisema serikali kupitia ofisi hiyo imeanza kuchukua hatua za kuelekea upigaji marufuku wa matumizi ya mifuko hiyo.

Alisema imeendesha mikutano miwili ya wadau na wananchi walishauri serikali kuchukua hatua za haraka kudhibiti matumizi hayo na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika uzalishaji wa mifuko mbadala.

"Ninapenda kuchukua fursa hii, kwa mara nyingine kuhimiza viwanda vinavyozalisha mifuko ya plastiki na wadau wengine kujitayarisha kwa kubadili teknolojia na kutathmini fursa zinazojitokeza kwenye kuzalisha mifuko mbadala hasa kipindi hiki cha mpito," alisema.

# Bil. 6/- kutumika kupima, kupanga, kumilikisha ardhi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 6.4 kwenye mamlaka za serikali za mitaa 25 kwa ajili ya kupima, kupanga na kumilikisha ardhi.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Rhoda Kunchela.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema serikali iliahidi kumaliza migogoro ya ardhi kwa kupima maeneo ya wananchi mapema ili kuepuka bomoabomoa bila fidia.

"Je, ni lini jambo hili litafika mwisho?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Mabula alitaja halmashauri hizo kuwa ni Jiji la Mbeya, Manispaa ya Ilemela, Sumbawanga, Shinyanga na Iringa.

Zingine ni Halmashauri za mji ya Makambako, Njombe, Kondoa, Nzega, Kahama na Bariadi na Halmashauri za wilaya za Misungwi, Sengerema, Geita, Nzega, Bukombe, Magu, Chato, Ukerewe, Busega, Simanjiro, Gairo, Songea, Namtumbo na Itilima.

Aidha, alisema serikali inaendelea kutafuta fedha katika vyanzo mbalimbali ili jambo hilo lifikie mwisho.

Kadhalika, alisema wizara hiyo imenunua vifaa vya kisasa vya upimaji ambavyo vimesambazwa katika kanda nane na vinatumiwa na halmashauri zote ili kurahisisha na kuharakisha upimaji wa maeneo ya wananchi na kutoa hatimiliki za ardhi.

"Wizara inaendelea na utekelezaji wa mkakati wa kupima kila kipande cha ardhi nchini ambapo awamu ya kwanza ya mkakati huo itatekelezwa kupitia mradi wa majaribio wa kuwezesha umilikishaji wa ardhi," alisema.

Alieleza kuwa mradi huo unatekelezwa katika wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi mkoani Morogoro.

Sambamba na utekelezaji wa mkakati wa kupima kila kipande cha ardhi nchini, Mabula alisema wizara inaendelea na utekelezaji wa programu wa kurasimisha makazi yasiyopangwa katika maeneo mbalimbali nchini kwa kushirikiana na kampuni binafsi za kupanga na kupima ardhi zilizosajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema lengo ni kuhakikisha maeneo yote yanapangwa na kupimwa ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye na hivyo kuzuia uendelezaji holela ambao husababisha migogoro na adha kwa wananchi ikiwamo bomoa bomoa ya makazi yasiyo rasmi.



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima akijibu maswali bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Sababu za maeneo ya Dar kukosa maji zawekwa wazi

BUNGE limeelezwa kuwa baadhi ya maeneo ya Jiji la Dar es Salaam hayajapata maji kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ongezeko la watu na ukuaji wa jiji hilo.

Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Jumaa Aweso, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kibamba (Chadema), John Mnyika.

Katika swali lake, Mnyika alisema serikali ilisema ifikapo mwaka 2016 matatizo ya maji jiji hilo yatakuwa yamemalizika.

"Je, ni kwanini ahadi hiyo haijatekelezwa kwa wakati? Je, ni mitaa ipi katika Jimbo la Kibamba maji hayatoki na ni lini Dawasa itahakikisha maji yanatoka katika maeneo hayo?" Alihoji.

Pia, alihoji serikali iko tayari kuwasilisha katika mkutano wa Bunge taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini kama ilivyokubali katika Bunge la 10.

Akijibu swali hilo, Aweso alisema maeneo mengi ya jiji hilo yanapata maji kama serikali ilivyoahidi kupitia Bunge baada ya kukamilisha miradi mikubwa ya maji ambayo ilikamilika mwaka 2016.

"Serikali inatambua kuna baadhi ya maeneo ya jiji hilo hayajapata maji kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ongezeko la watu na ukuaji wa Jiji la Dar es Salaam pamoja na upatikanaji wa maeneo ya kupitisha miundombinu ya miradi," alisema.

Kadhalika, alisema asilimia 80 ya wakazi wa jimbo hilo wanapata huduma ya maji na maeneo ambayo hayapati maji kwa sasa ni maeneo ambayo yapo kwenye miinuko mikubwa.

"Ili kuhakikisha wananchi wote wa jimbo hili wanapata maji hasa wanaoishi maeneo yenye miinuko mikubwa, serikali inaendelea na ujenzi wa matangi katika eneo la Msakuzi Kusini na Maramba Mawili Juu," alisema.



**Na Augusta Njoji, DODOMA**

## Watoto wenye mahitaji maalum wakabidhiwa kadi za matibabu

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WATOTO wenye mahitaji maalumu kutoka vituo vya kulelea watoto yatima jijini Arusha, wamekabidhiwa kadi za afya 20, kwa lengo la kuwarahisishia njia ya kupata huduma za afya bila malipo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi kadi hizo, Msemaji wa Kundi la Friends of Batuli, Batuli Kisaya, alisema wamegawa kadi hizo kwa ajili wa kuboresha mazingira ya upatikanaji wa huduma za afya kwa watoto wenye mahitaji mbalimbali.

Aliongeza, kadi hizo wamezitoa kwa watoto yatima, walemavu na waliotoka katika mazingira magumu kutoka kwenye vituo mbalimbali vya kulelea watoto wenye mahitaji maalumu jijini Arusha.

Alisema kundi hilo walichangishana fedha hadi kufikia kiasi cha Sh. milioni moja ambazo walizitumia kukata kadi za matibabu ya watoto hao.

"Kupitia kikundi chetu tulichangishana na kupata fedha kiasi cha shilingi milioni moja na fedha hizo tumezitumika kukata kadi za watoto wenye mahitaji maalumu hivyo, tunaiomba jamii kujitolea kuyasaidia makundi haya bila kukata tamaa," alisema.

Hata hivyo, alisema licha ya kutoa kadi kwa watoto hao, pia wametoa msaada wa vyakula, mahindi gunia moja, ndoo ndogo moja ya mafuta ya kupikia, katoni moja ya sabuni ya kufuli na maji ya kunywa katoni tatu kwa wazee saba kutoka katika kituo cha Herototo kilichopo kata ya Moshono, jijini hapa.

Mgeni rasmi katika shughuli hiyo ya ugawaji wa kadi hizo, alikuwa mfanyabiashara, Filemon Mollel, ambapo alitoa rai kwa jamii kuwa mstari wa mbele kuwasaidi watu wanapopatwa na matatizo bila ya kujali hali yake, dini na kabila lake.

"Siri ya mafanikio katika maisha ni kuwasaidia watu wenye matatizo na mahitaji maalumu katika jamii, pia sijawahi kuona Mungu akiwaacha bure watu ambao ni watoaji wazuri wa sadaka zaidi amekuwa akiwazidishia mara dufu pale watoapo," aliongeza.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha DC, Dk. Wilson Mahera, alipongeza mpango huo, wakijitolea kuisaidia jamii na alisema mpango huo, unaendana na mpango wa serikali wa maendeleo ya afya ambao unahitaji kila mwananchi kuwa na afya nzuri kwa kupata matibabu na huduma bora ya afya. "Binafsi mimi niwapongeza kundi hili na niwaombe mpango huu uwe endelevu, pia katika kufikia malengo ya mpango wenu mimi nitachangia kadi mbili za watoto wawili," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii katika Jiji la Arusha, Mather George, alisema Jiji la Arusha kuna wazee 9307, kati ya hao, wazee 3307, wamepewa kada za afya na wanapatiwa huduma za afya bure katika hospitali, vituo vya afya na zahanati mbalimbali za Jiji la Arusha.

Kwa upande wa toto yatima, walemavu na wenye mahitaji maalumu alisema kuwa wapo 21,000 na wazee wenye ulemavu wapo 560, hivyo aliiomba jamii kujitokeza kulisaidia kundi hilo kutokana na kuwa na idadi kubwa ya watoto na wazee wenye mahitaji maalumu.

# AfCHPR yaamuru serikali kumlipa mfungwa fidia 300,000/-

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

MAHAKAMA ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, (AfCHPR), imetupilia mbali ombi la kuachiwa huru mfungwa Kenedy Ivan, anayeendelea na kifungo cha miaka 30 jela baada ya mahakama nchini kumkuta na hatia ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Hata hivyo, mahakama hiyo imeiamuru serikali kumlipa Ivan nafuu ya Sh. 300,000 kama fidia kutokana na madhara aliyopata baada ya kunyimwa msaada wa kisheria wakati wa kusikiliza mwenendo wa kesi yake katika mahakama za ndani.

Fedha hizo zinatakiwa zitolewa na mlalamikiwa ambaye ni serikali ndani ya miezi sita na bila kukatwa kodi.

Katika hukumu iliyotolewa na Rais wa Mahakama hiyo, Jaji Sylvain Ore, akiwa na Makamu Rais wake Jaji Ben Kioko, hivi karibuni, ilikataa kukubaliana na ombi la Ivan kwa maelezo kuwa hakutoa ushahidi aliotoa hakujitosheleza kuishawishi mahakama. Majaji wengine walikuwa na Ben Achour, Angelo Matusse, Suzanne Mengue, Therese Mukamuli, Tujilane Chizumila, Chafika Bensaoula, Blaise Tchikaya na Stella Anukam.

Aidha, mahakama hiyo haikuweza kuthibitisha kwamba kutendo cha kutiwa hatiani na kisha kuhukumiwa kifungo kilikuwa cha ukatili kwake na kwamba kuendelea kutumikia kifungo ni kinyume cha sheria.

Katika shauri lake, Ivan aliilalamikia serikali kwa kuvunja haki ya kusikilizwa kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 7 cha sheria iliyoanzisha mahakama hiyo.

Alidai kuwa alitiwa hatiani katika mazingira ambayo hayakuwa na msingi kisheria na kwamba hakimu aliyesikiliza shauri hilo alishindwa kuwaita mashahidi wake licha ya kuiomba mahakama na hakupata msaada wa kisheria.

Wakati Ivan alijiwakilisha mwenyewe, upande wa serikali katika kesi hiyo uliwakilishwa na Mkurugenzi wa Divisheni ya Masuala ya Katiba na Haki za Binadamu, Sarah Mwaipopo, Mkurugenzi wa Masuala ya Sheria kutoka Wizara ya Mambo ya Nje, Afrika Mashariki na Ushiriano wa Kimataifa, Baraka Luvanda.

Wengine ni wanasheria wakuu waandamizi wa serikali, Nkasori Sarakikya na Mark Mulwambo, Mwanasheria Mwandamizi wa Serikali, Abubakari Mrisha na Blandina Kasagama ambaye ni Ofisa Huduma wa Nje kutoka Wizara ya Mambo ya Nje.



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Arusha, Joseph Bukombe, akimvisha kizibao cha kung'aa mmoja wa madereva bodaboda katika stendi kuu ya mabasi jijini Arusha, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya unywaji kiistarabu inayoratibiwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) uliofanyika jijini humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madereva waonywa unywaji pombe wakati wa kazi

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

KAMPENI ya unywaji wa kistaarabu inayoendeshwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), imezinduliwa rasmi mkoani Arusha, huku madereva wa vyombo vya moto wakihimizwa kuzingatia sheria za barabarani ikiwamo kutotumia vilevi wakati wa kazi.

Kampeni hiyo maarufu kama 'Usinywe na Kuendesha Chombo cha Moto' imeenda sambamba na ugawaji wa makoti ya usalama kwa madereva bodaboda mkoani humo ikiwa ni mkakati wa kuhimiza matumizi ya vifaa hivyo kwa usalama wa watumiaji wa barabara.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo uliofanyika jana katika Makao Makuu ya Trafiki jijini hapa, Mkurugenzi wa Uhusiano wa SBL, John Wanyancha, alisema kampeni hiyo imelenga kutoa elimu kwa wateja wake nchini ili kupunguza matukio yanayoepukika kama ajali zitokanazo na unywaji wa pombe kupindukia.

"Pombe isipotumika kistaarabu inaweza kuleta madhara katika jamii na mojawapo ya madhara ni pale mtu anapokunywa pombe na akaendesha chombo cha moto ikasababisha ajali, jambo ambalo ni hatari kwa madereva na pia ni hasara kwa taifa," alisema.

Kampeni hiyo inashirikisha wadau mbalimbali ikiwamo Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (Sumatra), madereva bodaboda pamoja na jamii kwa ujumla ikilenga katika kupunguza ajali zitokanazo na ulevi wa kupindukia nchini.


Kwa upande wake, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Arusha (RTO) Joseph Bukombe, alisema kampeni hiyo itasaidia kupunguza ajali zinazosababishwa na ulevi, huku akiwataka madereva kuzingatia kuacha kutumia vilevi ili kujihakikishia usalama wawapo barabarani.

"Unywaji wa pombe kistaarabu ni suala muhimu sana kwa madereva kwa sababu madereva wakiwa kwenye hali ya ulevi ni moja ya chanzo cha ajali za barabarani, hivyo tunaipa kipaumbele kampeni hii hapa mkoani Arusha na tutaendelea kutilia mkazo suala hili," alisema.

Aliipongeza SBL kwa kuona umuhimu wa kuwalinda watumiaji wa barabara kwa kutoa elimu hiyo kwa madereva na umma kwa ujumla.

"Pamoja na kuwa wao (Serengeti) ni watengenezaji wa pombe lakini wameona wajibu wao wa kumlinda na kuleta usalama wa madereva na watumiaji wengine wa barabara," alisema.

Kwa mujibu wa ripoti za Jeshi la Polisi, mwaka 2018, ajali 876 za bodaboda ziliripotiwa kutokea na kusababisha vifo 366 na majeruhi 694. Ripoti zinaonyesha kupungua kwa ajali hizo ambapo kwa mwaka 2017 zilikuwa 1,459 zilizosababisha vifo 728.





# Ofisa Elimu ataka wazazi kutimiza majukumu yao

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

OFISA Elimu wa Sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Julius Kakyama, amewataka wazazi na walezi kutotumia kigezo cha serikali kutoa elimu bure kuacha kuwahudumia watoto wao mahitaji mengine muhimu ikiwamo chakula wawapo shuleni.

Kakyama ametoa rai hiyo jana, wakati akizungumza na wazazi wa wanafunzi wanaosoma katika Shule ya Sekondari Sawe iliyopo wilayani hapa.

Ofisa huyo alisema kuwa wazazi na walezi bado wanawajibu wa kuwahudumia watoto wao wakiwa shuleni ikiwamo chakula na sio kuwashindisha njaa kwa kisingizio cha elimu bure.

Alisema kuwa serikali imeamua kutoa elimu bure, lakini haijakataza wazazi au walezi kuwahudumia watoto wao mahitaji mengine kama vile sare za shule, chakula, ulinzi wa mtoto pamoja na kufuatilia maendeleo ya watoto wawapo shuleni.

Amefafanua kuwa wazazi na walezi wanapaswa kuhakikisha kuwa watoto wanapata chakula wawapo shule ili kuwawezesha kumudu vipindi vyote vya masomo darasani.

"Katika mpango wa elimu bila malipo wazazi na walezi wajitahidi kutimiza wajibu wao wa kuwahudumia watoto huduma zile muhimu ikiwamo kuwanunulia madaftari, sare za shule na kuhakikisha kuwa wanapata chakula shuleni," alisema Kakyama.

Kakyama alisema serikali ya awamu ya tano imefuta ada pamoja na michango mbalimbali iliyokuwa kero kwa wazazi na walezi, ili kila mtoto wa kitanzania apate elimu kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne bure, wazazi wanapaswa kuwahudumia watoto mahitaji mengine

"Kwa sasa wazazi hamlipi tena ada wala michango wajibu wenu ni kununua sare za shule na kununua mahitaji mengine kama kalamu, daftari na mabegi, serikali inaendelea kuhamasisha mtimize wajibu kwa kuwanunulia watoto wao sare hizo," alisema.Aidha, Kakyama amesema ni vema wazazi na walezi wakachangia chakula shuleni ili kuwafanya wanafunzi waweze kusoma kwa utulivu na umakini wanapokuwa shuleni na kuzuia utoro.

"Tunaomba pia mtimize wajibu wenu kuchangia chakula shuleni kwa sababu unapotoa chakula shuleni tunapunguza utoro, tunaongeza umakini na ufuatiliaji kwa wanafunzi pale wanapofundishwa, wanafunzi wengi wao wanatoroka pale wanapohisi njaa na wakiondoka baadhi yao hawarudi," alisema Ofisa Elimu huyo. Kakyama aliwataka wazazi kusimamia ipasavyo maadili ya watoto wao ili waweze kufanikiwa na kufikia malengo waliyojiwekea kitaaluma kwa kushirikiana na walimu katika kuhakikisha watoto wanakuwa na nidhamu ya kuridhisha katika jamii inayowazunguka.

Pia aliwataka walimu na wazazi kuhakikisha wanawasisitiza wanafunzi kutii sheria za shule kama vile uvaaji wa sare sahihi ya shule, kuheshimiana na utumiaji wa lugha nzuri.

# Hekta 60 zatengwa kupandisha NIT kuwa chuo kikuu

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

BAADA ya Benki ya Dunia na Jamhuri ya watu wa China kutoa ufadhili wa Dola za Marekani milioni 83.5 kwa ajili ya mpango wa kukipandisha hadhi Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kuwa Chuo Kikuu, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania imekabidhi eneo la hekta 60 kwa ajili ya mpango huo.

Akizungumza baada ya makabidhiano hayo yaliyofanyika jana katika Uwanja wa Ndege wa KIA, Mkuu wa chuo hicho, Profesa Zacharia Mganilwa, alisema chuo hicho kimepokea eneo hilo kwa ajili ya kujenga miundombinu ya 'College of Aerospace Sciences and Technology'.

Makabidhiano hayo yamefanywa baina ya Mkurugenzi wa Kampuni ya Uendeshaji na Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (Kadco) ambao ndio wasimamizi wa eneo hilo na Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji.

"Eneo hilo litatumika kufundishia wataalamu wa usafiri wa anga katika fani za urubani, uhandisi wa matengenezo ya ndege na uhudumu ndani ya ndege," alisema Profesa Mganilwa.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa NIT, Benki ya Dunia imetoa Dola za Marekani milioni 21.5 na Jumhuri ya Watu wa China imetoa ufadhili wa kiasi cha Dola za Marekani milioni 62.

Kwa mujibu wa Profesa Mganilwa gharama za kumsomesha rubani nje ya nchi ni zaidi ya Sh. milioni 200, hivyo ujio wa chuo hicho katika Mkoa wa Kilimanjaro utapunguza gharama hizo kubwa. "Tutakapoanza kufundisha hapa nchini wahandisi gharama zake ni kama shilingi milioni 30 ambao wameshaanza kuhitimu tayari. Kwa upande wa marubani mpaka ahitimu ada itakuwa ni kama shilingi milioni 72. Kwa hiyo mtaona hivi sasa tutaweza kufundisha marubani wengi zaidi kuliko ambavyo hali ilivyo hivi sasa.

Profesa Mganilwa ameeleza zaidi kuwa: "Rais John Magufuli aliahidi atakinunulia chuo hicho cha NIT, ndege mbili ambazo mchakato wake unaendelea. Vile vile serikali imekopa Benki ya Dunia na imepanga kununua ndege tatu mpya kwa hiyo ndio maana tunasema tutakuwa na ndege tano mpya."

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Prof. Bavo Nyichomba, alisema Tanzania tumekuwa tunatumia fedha nyingi sana huko nje, karibu mara 10 ya bei ambazo chuo chetu hapa kitatoza ada.

"Kwa hiyo tutaweza kuwafundisha wataalamu wetu hapa wa kitanzania na kwa kweli tunataka na sisi tuwe na Centre ya Afrika ya kuweza kukaribisha wanafunzi toka sehemu nyingine, nchi nyingine kwa bei nafuu," ameeleza Profesa Nyichomba.



Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara, Justin Nyari, akizungumzia changamoto na mafanikio ya wachimbaji madini ya tanzanite katika Mji Mdogo wa Mirerani, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wananchi wakataa Bodi ya Shule

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

WANANCHI wa Kata ya Masama Mashariki katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, wameikataa Bodi ya Shule na kutaka Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, aivunje kutokana na kushindwa kusimamia maadili ya wanafunzi na walimu wa shule hiyo.

Wananchi hao walifikia uamuzi huo jana na kumshauri Ofisa Elimu ya Sekondari wa Wilaya hiyo, Julius Kakyama, kumpelekea Ole Sabaya ujumbe huo kwamba hawaitaki bodi hiyo kuanzia sasa.

Akiwa Kakyama katika mkutano maalum uliowahusisha wazazi na viongozi wa idara hiyo ya elimu, wananchi wa kata hiyo walimlazimisha Kakyama kumwondoa Mkuu wa Shule hiyo, Cecilia Kulaya.

Mkuu wa shule hiyo, Kulaya, anatuhumiwa na wananchi hao kushindwa kusimamia walimu, hali iliyosababisha baadhi ya walimu kufika shuleni kusaini na kuondoka wakati wa muda wa masomo.

"Ofisa Elimu katika shule hii, walimu wanafanyabiashara ya kuuza maandazi kwa wanafunzi licha ya wazazi kukubaliana kuchangia fedha za chakula. Bodi pamoja na mkuu wa shule wamekuwa wakilifumbia macho, bodi hii imekuwa ikizuia kukamatwa kwa wahalifu wanaowapa wanafunzi mimba.

Zaidi aliongeza: "Walimu hao hao hawatoi taarifa katika ngazi za juu kwa ajili ya maamuzi na hatua za zaidi, hali inayosababisha watuhumiwa kukimbia baada ya kufanya makosa ya jinai."

Makamu Mkuu wa Shule hiyo anatuhumiwa kumbaka mwanafunzi wa kidato cha nne na kumpa ujauzito akiwa shuleni.

Alisema ni vyema serikali ikavunja bodi ya shule hiyo pamoja na kumwondoa mkuu wa shule kutokana na wazazi kukosa imani na bodi hiyo ambayo wajumbe wake wameshindwa kudhibiti nidhamu ya shule hiyo. "Kwa mfano kuna tukio la mwalimu Solomoni Sirikwa kumpa mimba mwanafunzi wa kidato cha tatu, mkuu huyo pamoja na bodi walishindwa kutoa taarifa mapema hali iliyosababisha mtuhumiwa kukimbia," alisema.

Akizungumzia madhaifu ya mkuu huyo wa shule mmoja wa wazazi hao alisema kuwa amekosa ushirikiano na walimu wengine hali iliyosababisha baadhi ya walimu kuhama na pia amekuwa akizuia vipindi vya masomo ya dini hali iliyopelekea mmomonyoko wa madili.

Kwa upande wake Elifinye Ndosa alisema bodi ya shule hiyo imekuwa ikishindwa kuchukua hatua za haraka pindi inatokea tatizo halo.

Akizungumza na wazazi hao, Ofisa Elimu wa wilaya hiyo, Kakyama, alisema suala uvunjaji wa bodi liko chini ya uongozi wa mkoa kwa kuwa waliteuliwa na mkoa baada ya majina kupendekeza na mkuu wa shule husika.

Kakyama alisema suala mkuu wa shule liko juu yake kuwataka wazazi kuwa na subira wakati ofisi yake ikiendelea kulifanyia kazi suala hilo la mkuu wa shule.

Nipashe
# TESA
TEKNOLOJIA . ELIMU . SAYANSI
Jumanne Aprili 9, 2019



Ukurasa 18

## JE, WAJUA?
AJIFUNGUA JUU YA MTI WAKATI WA MAFURIKO



## Idara ya Uhamiaji na mwarobaini janga wahamiaji haramu nchini

Ukurasa 15




# PROF. MSAMBICHAKA Mwamba uliokipaisha Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya

Ukurasa 16



# TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

## Magazeti hayana wanaodurusu?

'DURUSU' au 'darisi' ni kitendo cha kurudia somo ama kitabu. Soma kwa makini, pitia tena yale ambayo mtu ameyasoma.

Fanya mchakato wa kutoa toleo jipya la chapisho kwa kupitia maandishi, kupunguza au kuongeza taarifa.

Magazeti makini huwa na wasomaji maalumu wanaopitia habari na makala za waandishi kabla ya kuchapishwa.

Wajibu wao ni kusoma kwa makini kama kuna mtiririko mzuri wa lugha, sentensi zinazoeleweka.

Baada ya hapo wahariri wasaidizi nao hupitia kuangalia kama kuna habari zinazoweza kusababisha gazeti, redio au runinga kushtakiwa kutokana na lugha chafu au uchochezi. Yote hayo hufanywa ili kusahihisha.

Ili kuwa makini zaidi, wanaodurusu wanatakiwa kuwa mahiri wa lugha zinazotumiwa na vyombo husika. Vyumba vya habari vya magazeti, redio na runinga vyapaswa kuwa na kamusi mbalimbali za Kiswahili na Kiingereza kwa nchi zinazotumia lugha hizo ili kujiridhisha na maneno yanayoandikwa au kutumiwa na waandishi/watangazaji.

Yafaa nikumbushe tena kuwa maana ya neno 'lughawiya' ni taaluma inayoshughulikia uchambuzi wa lugha katika nyanja mbalimbali kama vile sarufi, maana, matamshi na matumizi.

Lugha ni mfumo wa mawasiliano, mtindo (wa kusema). Msemo, maneno, usemi, kauli, tamko. Hivyo watu wanapaswa kuwa makini sana wanapozungumza, kutangaza au kuandika.

Kuna neno linaloitwa 'visawe.' Maana yake ni maneno yenye maana zinazokaribiana. Kwa mfano, 'mtoto' na 'mwana' humaanisha kitu kimoja. Visawe hutumika ili kuwasilisha dhana ileile iliyokusudiwa bila kubadilisha maana.

Visawe hupamba lugha ama katika mazungumzo au katika uandishi wa namna mbalimbali. Kwa mfano: 'Mauzauza' ni kiinimacho, mizungu, mazingaombwe.

'Msichana' aweza kuitwa banati, binti, na mwari. 'Mvulana' aitwa ghulamu, janadume au barobaro. 'Weweseka' ni hohosa, babaika, kiakia, hangaika na riyariya.

'Vitawe' ni maneno yenye maana zaidi ya moja. Umoja wa vitawe ni 'kitawe.' Kwa hiyo 'vitawe' huchukua umbo au mofolojia (sarufi) moja yaani tawi la isimu linalohusika na uchambuzi na uchanganuzi wa kanuni na mifumo inayohusu upangaji wa maneno katika lugha lakini katika muktadha wa kimatumizi huenda kitawe kikawa na maana tofauti.

Katika matumizi ya vitawe mnenaji au mwandishi ni lazima awe makini ili kuondoa utata katika sentensi au usemi wake. Mfano: 'Kuba' ni dari ya nyumba iliyojengwa mfano wa tao au bakuli lililofudikizwa; kaburi lililojengewa ukuta mfano wa chumba.

Maneno yasiyokuwapo kwenye msamiati wa Kiswahili ndio yatumikayo sana nchini yakiwamo ya kihuni yazungumzwayo mitaani na vijiweni!

Sikushangaa niliposoma ujumbe mfupi wa simu niliotumiwa na mwandishi wa safu hii akisema: "Asante kwa kutusaidia tujifunze Kiswahili.

Kuna mwanahabari wa (akataja kituo cha redio) mara nyingi anapotoa ripoti huwa anatamka jina lake na humalizia kwa kuboronga jina la mkoa.

Badala ya kusema 'kutoka Kigoma huwa anasema kutoka Chigoma.' Aibu kwa chombo cha umma."

Maneno yatumiwayo sana na waandishi/watangazaji ni 'mzuka', 'balaa', 'buana/bana', 'mihela/mahela', 'madogo', 'nyavu' n.k.

Sasa tuone maana halisi ya maneno hayo: 'Mzuka' ni kiumbe kisichoonekana ila hudhaniwa kuwa kinaishi na kumtokea mtu; pepo, zimwi, kivuli, rununu.

Gazeti maarufu la michezo liliandika: "Kwa sasa iko nafasi ya tano nyuma kidogo ya Simba, huku ikisaka nafasi ya kuweka heshima, kwani mastaa wake wanapatwa na mzuka kinoma." Je, 'mzuka' linaakisi (toa picha, dokezo, ishara au fununu kuhusu jambo) sentensi ya mwandishi?

'Balaa' ni jambo, kitu au mtu anayefikiriwa kuleta maafa, mkosi au hasara; kisirani, nuksi. Jambo lenye kuleta hali ya kutoelewana; kizaazaa, mtafaruku, beluwa.

Kiswahili sahihi hakina neno 'buana' kama linavyoandikwa na waandishi wetu wakiwa na maana ya 'bwana'!

Wengine huandika 'bana' ambalo maana yake ni kuweka kitu katikati ya mikono na kutumia nguvu kukisonga pande zote; gandamiza, fyanda. Shika kwa nguvu kama mtego; nasa, kamata. Funga: bana mlango, bana kufuli. Pia tumia kwa uangalifu.

Aidha, waandishi huandika 'mihela' au 'mahela' wakiwa na maana ya fedha nyingi! 'Hela' ni sarafu au noti iliyoidhinishwa na serikali kuwa malipo halali kwa ajili ya kubadilishana na bidhaa zinazonunuliwa: fedha, faranga, pesa, fulusi, senti.

Pia ni tamko la kumfanya mtu awe na hadhari; tahadhari! angalia!

Upotoshaji mwingine: "Pawasa: Madogo mbona wamepita. Kocha wa viungo wa timu ya taifa ya Tanzania yenye umri chini ya miaka 20 'Ngorongoro Heroes', Boniface Pawasa ametoa nafasi kwa timu ya vijana wenye umri chini ya miaka 17 'Serengeti Boys' kushiriki michuano ya Kombe la Dunia nchini Brazil."

Je, ni sahihi vijana wenye umri chini ya miaka 20 kuitwa 'madogo'? Tena sentensi haikuandikwa itakiwavyo badala yake imeborongwa! Pawasa ana wadhifa gani hata aseme Serengeti Boys itashiriki michuano na Kombe la Dunia nchini Brazil? Yeye amebashiri kuwa huenda timu hiyo ikashiriki michuano hiyo baada ya kuona mchezo wa vijana hao.

'Nyavu' ni wingi wa wavu na hutengenezwa kwa nyuzi au nyaya zilizosukwa na kufanya utandu wenye tundu ndogondogo unaotumiwa kwa shughuli mbalimbali kama vile uvuvi, kutegea wanyama, kufunga kwenye magoli ya kandanda; kimia.

Pamoja na uhalisia huu, waandishi na watangazaji huandika na kusema, kwa mfano, "Kagere ametikisa nyavu za timu pinzani kwa kuiandikia Simba bao la kuongoza." Ukweli ni kwamba ametikisa 'wavu' wa timu pinzani. Hata kama amefunga zaidi ya bao moja huwa ametikisa wavu (sio 'nyavu') mara ya pili, tatu n.k. au ametikisa tena wavu wa wapinzani.

**Methali: Mwenda kasi mngojee achoke.**

***marobarnabas@yahoo.com***
***0715/0784 33 40 96***

# ELIMU KUTOKA POLISI




Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), Maria Nzuki. **PICHA: MTANDAO**

## WAZAZI MSIWAACHE WATOTO WAJILEE WENYEWE

KABLA sijaanza kuandika makala haya, ningependa wasomaji wangu wapate ufahamu kuhusu neno kubaka pamoja na neno kulawiti.

Kubaka ni kitendo cha kumwingilia mtoto aliye chini ya miaka 18 kimapenzi, iwe kwa hiari yake au bila hiari yake.

Kwa watu walio na miaka 18 na kuendelea ni kitendo cha kumlazimisha mwanamke kufanya mapenzi kwa kutumia nguvu.

Miongoni mwa sababu zinazopelekea kutokea kwa matendo hayo ni wazazi kuwa mbali na watoto wao, jambo ambalo husababisha watoto kujilea wenyewe na kujiingiza katika makundi mabaya ambayo hujihusisha na matendo ya ubakaji na wakati mwingine watoto wa kiume kulawitiwa.

Kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2017, jumla ya watu wa rika mbalimbali waliofanyiwa vitendo vya ubakaji ni 8039, ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2018 ambapo matukio ya ubakaji yaliyoripotiwa ni 7,617.

Hiyo ni sawa na upungufu wa matukio 422, yaani asilimia 5.2.

Aidha, takwimu za Jeshi la Polisi kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2017, zinaonyesha kwamba jumla ya watu waliofanyiwa vitendo vya ulawiti ni 1184, ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2018, ambapo matukio ya ulawiti yaliyoripotiwa ni 1201, sawa na ongezeko la matukio 17, yaani asilimia 1.4.

Kuongezeka kwa matukio haya, kunatokana na wazazi na jamii kwa ujumla kutotimiza wajibu wao wa malezi na kufumbia macho vitendo hivyo vya unyanyasaji.

Hiyo ni pamoja na kusuluhisha matukio hayo kinyume na sheria au kifamilia, jambo ambalo linasababisha kuongezeka kwa vitendo vya ubakaji na ulawiti.

Kimsingi, vitendo hivyo vimesababisha kuongezeka kwa mmomonyoko mkubwa wa maadili hususani mimba za utotoni, kuongezeka kwa watoto wa mitaani, maambukizi ya magonjwa ya zinaa na zaidi kuwaathiri kisaikolojia watu wanaofanyiwa vitendo hivyo.

Wakati mwingine mwaathirika anaweza kupata maumivu makali wakati wa kitendo na kusababisha majeraha na hata kupoteza maisha.

Wazazi na walezi kwa ujumla, wanatakiwa kujenga utamaduni wa kuwa na muda wa kuwa karibu na watoto wao, kuwafuatilia, pamoja na kuchunguza mienendo yao.

Aidha, wanatakiwa kuhakikisha wanawakagua watoto wao mara kwa mara ili kujua mapema kama wamefanyiwa kitendo chochote cha ukatili na hasa kuzungumza nao kirafiki ili iwapo wanaweza kusema ukweli bila uwoga wafanye hivyo.

Iwapo atabainika kutokea kwa kitendo hicho mzazi au mlezi ana jukumu la kuripoti haraka katika kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi ya mtuhumiwa.

Pia, mzazi ama mlezi hatakiwi kumuosha au kumsafisha mtoto aliyefanyiwa kitendo cha ubakaji muda mfupi baada ya tendo hilo, lengo ni kuhifadhi ushahidi usipotee na kurahisisha upelelezi wa kesi mahakamani.

Katika kukabiliana na matukio ya ubakaji na vitendo mbalimbali vya unyanyasaji, Jeshi la Polisi nchini, linayo madawati ya jinsia na watoto kuanzia ngazi za wilaya hadi Makao Makuu ya Polisi kote nchini, ambayo yana mafunzo maalumu ya kushughulikia matukio hayo.

Akizungumza na mwandishi wa makala haya, Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) Maria Nzuki alisema, kuwa jumla ya madawati 417 yameanzishwa nchi nzima katika vituo vya Polisi vya madaraja ya A, B na C.

Miongoni mwa majukumu ya Dawati la Jinsia na Watoto katika vituo vya Polisi ni kushughulikia makosa yote ya udhalilishaji wa kijinsia hususani matukio ya ubakaji na ulawiti.

Aliongeza kuwa, katika kukabiliana na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia hususani vitendo vya ubakaji, Jeshi la Polisi nchini kupitia madawati ya jinsia na watoto, linaendelea kutoa elimu ya uelewa.

Elimu kwa masuala yahusuyo ukatili wa kijinsia kwa wananchi kupitia vyombo vya habari, makongamano, mikutano ya wazi, sanaa pamoja na maonyesho mbalimbali.

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Uhusiano,**
**Makao Makuu ya Polisi,**
**S.L.P 9141**
**Dar es Salaam.**
**Baruapepe:habariphq@yahoo.com**
**habari.phq@tpf.go.tz**

ELIMU

NA ANTHONY GERVAS, MARA

# Idara ya Uhamiaji na mwarobaini janga wahamiaji haramu nchini

■ Yaanzisha kitengo maalum cha utawala wa mipaka na operesheni
■ Udhibiti wa mipaka kuwa kozi inayotolewa katika Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda Moshi
■ Yaja na daftari maalum la kuandikisha wageni mikoa mbalimbali

IDARA ya Uhamiaji Tanzania inakabiliana na changamoto nyingi katika mipaka, hasa za wahamiaji haramu wanaoingia nchini bila vibali vya kuishi, kinyume cha sheria.

Hili ni tatizo pia la kimataifa ambalo linayakumba mataifa mengi katika dhima nzima ya kupambana vilivyo na wahamiaji haramu, hali ambayo imekuwa ikichagiza uhalifu, jambo linaloathiri vilevile hata uchumi wa nchi.

Kwa hivi sasa suala la wahamiaji haramu ni ajenda ya kitaifa na kimataifa, kutokana na ongezeko la wimbi hilo katika maeneo mbalimbali nchini na hata kwenye uga wa kimataifa.

Msemaji Mkuu wa Idara ya Uhamiaji nchini, Ally Mtanda, anafafanua zaidi juu ya janga hili.

Anaanza kwa kusema kwamba, mhamiaji haramu ni raia wa kigeni anayeingia nchini na kuendelea kuishi kinyume cha sheria za uhamiaji.

Anabainisha zaidi kwamba anaweza kuwa anayeingia nchini kwa mujibu wa sheria za uhamiaji, lakini akaendelea kuishi nchini kinyume na sheria, kanuni na taratibu husika.

**KINACHOCHANGIA WAHAMIAJI HARAMU NCHINI**

"Kihistoria Tanzania kwa muda mrefu imekuwa ni kimbilio la wageni wengi wanaotafuta hifadhi ya ukimbizi kutokana na machafuko ya kisiasa na kijamii katika nchi zao," anabainisha msemaji huyu.

Anafafanua kuwa baadhi ya wageni hao wamekuwa hawafuati taratibu za kuishi nchini kama wakimbizi na hivyo kuishi kama wahamiaji haramu.

"Wengine wakikwepa zoezi la kurejea kwao kwa hiari, huku wakiwa hawajahalalisha ukaazi wao nchini, hivyo kuendelea kuishi kinyume cha sheria," anasema.

**JIOGRAFIA**

Mtanda anasema kuwa kijiografia, Tanzania inakadiriwa kuwa na eneo la kilometa za mraba 954,087 na inapakana na nchi nane tofauti.

Anasema eneo lote hilo limezungukwa na mipaka ya alama za mawe (Beacons), bahari, maziwa, mito na vilima ambavyo havina uzio, hivyo kutumika kama vipenyo kwa wahamiaji haramu kuingia nchini na kuishi.

**UCHUMI**

Anataja sababu nyingine inayovutia ongezeko la wahamiaji haramu kuwa ni suala la uchumi, ambapo Tanzania imebadili mfumo wake wa uchumi hodhi na kufuata mfumo wa soko huria.

"Mabadiliko hayo yamewavutia watu wengi kuja kutafuta maslahi zaidi ya kimaisha, na hivyo kusababisha ongezeko la wageni nchini wakiwamo wahamiaji haramu," anasema.

Mtanda anabainisha kuwa ukuaji wa teknolojia na mfumo wa utandawazi, vimeleta changamoto ya watu wanaotafuta kazi na wanaojihusisha na vitendo viovu kama vya uuzaji wa dawa za kulevya.



Baadhi ya wahamiaji haramu walionaswa na moja ya operesheni zilizofanywa na Idara ya Uhamiaji kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama. **PICHA: MTANDAO**

> "Tunaendelea kuweka mtandao wa kompyuta katika ofisi mbalimbali ili kuunganisha vituo vyote na makao makuu... mpango huo ukikamilika utarahisisha kuboresha mawasiliano kati ya vituo vya mipakani, wilaya, mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar."



Msemaji Mkuu wa Uhamiaji Tanzania, Ally Mtanda, akizungumza katika mkutano wa ujirani mwema na wananchi wa Sirari mkoani Mara na wa Isibania nchini Kenya, kuhusu vita dhidi ya wahamiaji haramu, ulioanza Machi 19 na kumalizika Machi 21. **PICHA: ANTHONY GERVAS, MARA**

"Pia usafirishaji haramu wa binadamu, uingizaji wa silaha nchini kinyume cha sheria, utapeli na vitendo vingine vya kihalifu," anasema.

**SIASA**

Msemaji anataja amani na utulivu nchini kuwa sababu nyingine ya raia wa nchi jirani na nyingine ambazo zimekuwa zikikumbwa na matatizo ya ndani, kama vita vya wenyewe kwa wenyewe kukimbilia Tanzania.

"Na baadhi yao kuishi nchini kinyume cha sheria, mfano wimbi la Wasomali na wa-Ethiopia wanaokamatwa mara kwa mara, kwa kuingia nchini kinyume cha sheria," anasema.

**KIJAMII**

Aidha, Mtanda anabainisha sababu nyingine kuwa ni ile ya kuwapo kwa uhusiano wa kijamii kwenye maeneo ya mipakani, yanayoambatana na ndoa kati ya Watanzania na raia wa nchi jirani.

"Wapo baadhi ya Watanzania na wageni vilevile wenye imani potofu kwamba kuoa au kuolewa tu na Mtanzania na kupata cheti cha ndoa kunampa mgeni uhalali wa kuishi nchini bila hati yoyote kutoka Idara ya Uhamiaji," anasema.

**IDARA INAVYOKABILI TATIZO HILI**

Katika kukabiliana na tatizo hili Mtanda anasema Idara ya Uhamiaji imeanzisha kitengo maalum cha utawala wa mipaka na operesheni ili kuimarisha mipaka, misako, doria na shughuli za operesheni.

"Aidha, imefanya udhibiti wa mipaka kuwa moja ya kozi zinazotolewa katika Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda kilichopo Moshi mkoani Kilimanjaro," anasema na kuongeza:

"Pia tumeanzisha daftari maalum la kuandikisha wageni mikoa mbalimbali, hususani ya mipakani."

Anasema, idara imekuwa ikitoa elimu kwa umma kuwaelimisha wananchi madhara ya kukumbatia wageni ambao hawana vibali vya kuishi nchini.

"Maofisa wetu wamekuwa wakishiriki vikao kuanzia ngazi ya kata ili kuwapa wananchi elimu juu ya masuala yahusuyo uraia na haki zitokanazo na uraia huo, hivyo kuwajengea uzalendo wa kufichua wasio raia wasinufaike na haki zisizo wastahili," anasema.

**USHIRIKIANO**

Msemaji huyu anabainisha kwamba Idara imekuwa ikifanya misako na doria za mara kwa mara kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama pamoja na wananchi.

"Kupitia misako na doria hizo, wageni kadhaa wamekuwa wakikamatwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria," anasema na kuongeza:

"Tunaendelea kuweka mtandao wa kompyuta katika ofisi mbalimbali ili kuunganisha vituo vyote na makao makuu...mpango huo ukikamilika utarahisisha kuboresha mawasiliano kati ya vituo vya mipakani, wilaya, mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar."

**CHANGAMOTO**

Pamoja na jitihada nzuri zinazofanywa na idara hiyo kuhakikisha inadhibiti wahamiaji haramu, Mtanda anataja changamoto mbalimbali zinazofanya udhibiti huo kutofanikiwa kikamilifu.

"Hizo ni pamoja na ukubwa wa uwazi wa mipaka, wananchi kuwa na tabia ya kuhifadhi au kusafirisha wageni kwa manufaa yao, wananchi kutokuwa na vitambulisho vya Taifa ili kuweza kupambanua nani ni raia na asiye raia," anasema.

**ATHARI ZA WAHAMIAJI HARAMU KWA TAIFA**

Mtanda anataja athari hizo kuwa ni pamoja na kuhatarisha usalama wa wananchi, ongezeko la uhalifu kama vile ujambazi, uuzaji na utumiaji wa dawa za kulevya, ugaidi, ukahaba, utapeli, kupungua kwa nafasi za ajira pamoja na huduma nyingine kwa wananchi.

"Hiyo inatokana na Taifa kubeba mzigo mkubwa wa watu wanaohitaji huduma hizo wakiwamo wahamiaji haramu, lakini pia kuingiza utamaduni wa kigeni unaoweza kufuta mila na utamaduni wa kitanzania," anasema.

**ITAENDELEA WIKI IJAYO AMBAPO MTANDA ATAFAFANUA AINA ZA URAIA**

## TEKNOLOJIA

NA NEBART MSOKWA, MBEYA

# MIAKA 12 YA PROF. MSAMBICHAKA

## Mwamba uliokipaisha Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya

- Taasisi ufundi imegeuka chuo kikuu bora
- Wanafunzi 700 - 4,630; wanawake 33 - 884
- Kozi nne hadi 21; kampasi mpya Rukwa
- Aleta taaluma ngeni ya uhandisi vifaa tiba

FEBRUARI 27 mwaka huu, Jumuiya ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (Must), ilifanya hafla maalumu ya kumuaga aliyekuwa Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Joseph Msambichaka, ambaye anastaafu kutumikia wadhifa huo.

Aidha, katika hafla hiyo Profesa Aloys Mvuma, alikaribishwa na kusimikwa rasmi kurithi nafasi ya Profesa Msambichaka, hata kuandika historia ya kuwa mtu wa pili kushika wadhifa huo tangu chuo hicho kilipopandishwa hadhi na serikali mwaka 2012 kuwa chuo kikuu, kutoka iliyokuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya (Must).

Historia inaonyesha kuwa Prof. Msambichaka ndiye kiongozi wa chuo hicho aliyedumu kwa muda mrefu zaidi madarakani tangu chuo hicho kilipoanzishwa ambapo ametumikia nafasi za juu za chuo hicho kwa muda wa miaka 12.

Prof. Msambichaka, mtaalamu wa uhandisi, alianza kukiongoza chuo hicho mwaka 2007, wakati huo kikiwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya, alikohudumu katika nafasi ya mkuu wa chuo.

Mwaka 2012 baada ya taasisi hiyo kupandishwa hadhi na kuwa Chuo Kikuu, Prof. Msambichaka aliteuliwa kuwa Makamu Mkuu wa Chuo wa kwanza kutumikia wadhifa huo, aliyodumu nao kwa miaka saba.

> "Lengo lingine ni kuipunguzia serikali, gharama za uagizaji wa wataalamu wa vifaa tiba kutoka nje kwa ajili ya kuja kututengenezea vifaa tiba vyetu na hii programu ni muhimu sana, hasa kipindi hiki ambacho serikali inaimarisha huduma za afya,"

**MAFANIKIO**

Inaelezwa, uongozi wa Prof. Msambichaka umekipaisha kuingia katika orodha ya vyuo bora nchini, kutokana na elimu inayotolewa na wataalamu waliozalishwa, hasa wa eneo la teknolojia.

Baadhi ya yanayotajwa katika mafanikio chuoni ni ongezeko la watumishi walioelimishwa na chuo kwa nyakati na ngazi tofauti za elimu.

Kwa mujibu wa takwimu za chuoni, wakati anaanza kukiongoza, aliwakuta watumishi 109, lakini amestaafu wakiwa idadi yao 503 ambao wana viwango tofauti vya elimu na wengine bado wanaendelezwa.

Baraza la wafanyakazi wa chuo hich kupitia mwenyekiti wake, Dk. Lw Mwakalukwa, linaeleza alama n bali ambazo Prof. Msambichaka ameziacha katika chuo hicho na kukifanya king'ae.

Dk. Mwakalukwa anasema, wakati Prof. Msambichaka anaanza kazi mwaka 2007, chuo kilikuwa kinadahili wanafunzi 700 wa ngazi ya stashahada katika fani nne pekee, lakini mpaka anastaafu, udahili umefikia wanafunzi 4,630.

Anasema idadi hiyo ya wanafunzi, inajumuisha wanaosoma stashahada na shahada ya kwanza. Pia kozi zimeongezeka kutoka nne za wakati huo mpaka 21; yaani 15 za stashahada na sita za shahada ya kwanza.



Makamu Mkuu mstaafu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (Must), Prof. Joseph Msambichaka (kushoto), akipokea cheti maalumu cha kutambua mchango wake kwa chuo hicho, kutoka kwa Mkuu wa Chuo hicho, Pius Msekwa. Kulia ni Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Zakia Meghji. **PICHA: NEBART MSOKWA**



Pia, anasema mkuu huyo wa chuo, amesaidia ongezeko la udahili wa wanafunzi wa kike kutoka 33 wa mwaka 2007 hadi 884, wanaosoma fani mbalimbali za sayansi, zikiwamo za uhandisi.

"Prof. Msambichaka alianzisha kampeni maalumu ambayo chuo kinaendesha kila mwaka kwenye shule mbalimbali za sekondari, kwa ajili ya kutoa hamasa kwa watoto wa kike kupenda masomo ya sayansi na hisabati. Kampeni hii imechangia ongezeko la wanafunzi wa kike," anasema Dk. Mwakalukwa.

**KITENGO CHA USHAURI**

Dk. Mwakalukwa anasema, Prof. Msambichaka alibuni kitengo cha ushauri elekezi, kinachoitwa 'Mist Consultancy Bureau' (MCB), ambacho kinatoa ushauri kwenye miradi mbalimbali ya serikali, kampuni na watu binafsi.

Anasema mbali na kuwa chanzo cha mapato ya chuo, pia kinasaidia kuwajengea uwezo wataalamu wa chuo na wanafunzi, kupitia miradi inayotekelezwa na kitengo hicho katika maeneo mbalimbali.

"Katika uongozi wa Prof. Msambichaka hapa chuoni, MCB imechangia shilingi bilioni 1.6 kwenye mapato ya chuo na tunatarajia mapato hayo kuendelea kuongezeka kwa miaka ijayo," anasema Dk. Mwakalukwa.

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, anasema pamoja na kuwapo kitengo hicho cha ushauri elekezi, pia Prof. Msambichaka aliwezesha kuanzishwa kampuni ya ujenzi ijulikanayo Mist Engineering Contractors Ltd (Misteco).

Ni kampuni hiyo iliyoanzishwa mara tu baada ya kuingia madarakani na imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na Dk. Mwakalukwa anasema, lengo la kuanzishwa kampuni hiyo, ilikuwa kuwajengea uwezo wataalamu wa chuo na wanafunzi.

**UHANDISI VIFAA TIBA**

Dk. Mwakalukwa anaeleza, baada ya kubaini Tanzania inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa wataalamu wa vifaa tiba, aliamua kuanzisha programu maalumu ya uhandisi vifaa tiba, ili kuzalisha wataalamu hao.

Anasema programu hiyo imeanza kutolewa kwa mara ya kwanza katika mwaka wa masomo 2018/2019 na kwamba pamoja na uchanga wake, lakini hamasa iliyotolewa imeifanya kupata mwitikio mkubwa wa wanafunzi kujiunga.

Anasema, programu inatolewa katika ngazi ya stashahada na kwamba wanafunzi waliodahiliwa mpaka sasa wapo 173, huku kikiwa ndicho chuo cha kwanza nchini kutoa mafunzo ya aina hiyo.

Kwa mujibu wa Dk. Mwakalukwa, moja ya malengo ya Prof. Msambichaka kuanzisha programu hiyo, ilikuwa kuhakikisha chuo kinazalisha wataalamu wa kutosha watakaotengeneza na kukarabati vifaa tiba, ili kuepuka kukwama kwa utoaji huduma bora za afya kwa wananchi.

"Lengo lingine ni kuipunguzia serikali, gharama za uagizaji wa wataalamu wa vifaa tiba kutoka nje kwa ajili ya kuja kututengenezea vifaa tiba vyetu na hii programu ni muhimu sana, hasa kipindi hiki ambacho serikali inaimarisha huduma za afya," anasema Dk. Mwakalukwa.

**UPANUZI WA CHUO**

Dk. Mwakalukwa anamsifu Prof. Msambichaka, kwamba wakati wa uongozi wake, alifanikisha kuandaa mipango ya kukipanua chuo hicho, kwa kuongeza majengo ndani ya makao makuu kampasi ya Mbeya na kuanzisha kampasi nyingine mkoani Rukwa.

Anafafanua kuwa, kampasi hiyo ya Rukwa, itaanza shughuli za masomo rasmi baada ya ithibati na kwamba inatarajiwa kutoa mafunzo katika fani za: Uhandisi, Kilimo, Afya, Ualimu, Uchumi na Sayansi ya Jamii.

Kuhusu maendeleo ya kampasi ya Mbeya, Mwenyekiti wa Baraza la Must, anataja upanuzi wake ni ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800.

Vilevile anasema, mtaalamu huyo aliwezesha kujengwa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia watumiaji 2,500 kwa wakati mmoja na kwamba, kukamilika kwa jengo hilo, kunatarajiwa kusaidia kupunguza changamoto ya uhaba wa nafasi.

Dk. Mwakalukwa anasema, katika maktaba iliyopo sasa, ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 150 pekee, hali ambayo ni changamoto kwa idadi kubwa kwa mahitaji ya wanafunzi waliopo sasa.

"Amewezesha, pia ujenzi wa maabara nne hapa chuoni, pia ameandaa mpango kabambe wa upanuzi wa chuo (master plan), ambao unakusudia kujenga majengo mbalimbali, zikiwamo nyumba za watumishi, karakana, maabara, vyumba vya mihadhara na hosteli za wanafunzi," anaeleza Dk. Mwakalukwa.

Anasema, kukamilika kwa mpango huo, kutaongeza uwezo wa chuo hicho kudahili wanafunzi na kufikia wanafunzi 15,000 wa fani mbalimbali zinazotolewa.

**MSEKWA AMPONGEZA.**

Mkuu wa Chuo cha Must, Pius Msekwa, anampongeza Prof. Msambichaka kwa mchango mkubwa alioutoa kwa Taifa, kupitia kazi aliyoifanya, ikiwAmo uzalishaji wa wataalamu.

Msekwa, ni Spika mstaafu wa Bunge na kabla ya hapo, aliwahi kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Dar es Salaam, anasema serikali inatambua mchango wa kiongozi huyo chuoni Must, kuanzia alipokipandisha hadhi kutoka kuwa taasisi mpaka ilipokuwa chuo kikuu, hali inayokipa hadhi kubwa nchini.

Katika kipindi kirefu cha utumishi wa kitaaluma, Profesa Msambichaka, amekuwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kuhusu dira ya chuo, Msekwa anasema, makusudio yaliyoko ni kukiongezea ubora kiwe juu katika ushindani wa ukanda wa Afrika Mashariki.

"Tunampongeza sana Prof. Msambichaka kwa utendaji wake uliotukuka. Lengo letu ni kukifanya chuo hiki kuwa chachu ya ongezeko la matumizi ya sayansi na teknolojia hapa nchini," anasema Msekwa.

Anaongeza: "Hivyo, tunamuomba mwenzetu Msambichaka, tutakapohitaji msaada wake, awe tayari kutusaidia tukikwama."

**MWENYEKITI BARAZA**

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo cha Must, Zakia Meghji, anasema wasifu wa Prof. Msambichaka ni mzuri na ndio maana alifanya vizuri wakati wa uongozi wake chuoni, katika kipindi chote alichotumikia.

Anampongeza kwa kustaafu kwa mujibu wa sheria na sio kwa sababu ya kashfa ya aina yoyote, kama ambavyo huwa inatokea kwa baadhi ya viongozi nchini.

Meghji anamsifu Prof. Msambichaka kwa ubunifu uliosaidia chuo kukua kwa haraka na kuwa miongoni mwa taasisi za elimu ya juu, zenye sifa nzuri ikiwamo kutoa hamasa kwa watoto wa kike kujiunga na masomo ya sayansi.

"Mimi baada ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hiki, Prof. Msambichaka, alinipigia simu akanipongeza kwa kuteuliwa na akanikaribisha kwenye chuo hiki. Hivyo nami nampongeza kwa kustaafu kwa mujibu wa sheria na sio kutumbuliwa," anasema Meghji.

**ATOA YA MOYONI**

Akiagana na Jumuiya ya Chuo Kikuu Must, Prof. Msambichaka anasema kilichomfanya aonekane amefanya vizuri katika utendaji wake ndani ya chuo hicho, ni ushirikiano alioupata kutoka kwa wasaidizi wake mbalimbali.

Anawataka watumishi waliobaki kuendelea kuwa waadilifu na kumpatia ushirikiano Makamu Mkuu mpya wa chuo hicho, Prof. Mvuma, kama walivyompatia yeye, Must iendelee kustawi.

Pia, anawaasa watumishi hao kutambua dhamana waliyopewa na serikali katika chuo hicho, hivyo anawataka waendelee kulinda jina na heshima ya chuo katika uzalishaji wa wataalamu wa uhandisi na teknolojia nchini.

"Tuendelee kuijenga Must yetu, huku tukiongeza ubunifu kazini na kushirikiana na wadau wetu mbalimbali, ambao ni nguzo muhimu katika kukamilisha malengo yetu na hivyo kuchochea maendeleo ya taifa zima," anasema Profesa Msambichaka.

Pia, anawaasa wanafunzi kuutumia muda mfupi wanaokuwa nao chuoni, kujiepusha na vitendo viovu vinavyoweza kuharibu mipango yao ya maisha.

**MRITHI WAKE**

Mrithi wa Prof. Msambichaka katika nafasi ya Makamu Mkuu wa Chuo cha Must, Prof. Mvuma, anaahidi kuendelea kuhakikisha anakisimamia chuo kiendelee kuwa bora.

Anasema kitu pekee kitakachomsaidia kufanikisha suala hilo, ni kufanya maamuzi yenye busara ya ngazi ya juu, ambayo yatakuwa na tija kwa chuo na taifa kwa ujumla.

Anampongeza Prof. Msambichaka kwa kazi nzuri aliyoifanya wakati wa uongozi wake na kwamba yeye ataendelea kutekeleza majukumu hayo, kuanzia pale alipoishia mwenzake, huku akijifunza mbinu zilizokuwa zinatumika.

Mbali na kuking'arisha Chuo cha Must, pia Prof. Msambichaka, alama za nyayo zake zinatajwa katika miradi kama vile ujenzi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam, ambayo ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na timu ya wajumbe wabunifu wa uanzishwaji Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom).

## JIELIMISHE



Mwanamke akiwa ndani ya pango Israel. **PICHA: MTANDAO**

## Pango refu zaidi duniani la chumvi lagunduliwa Israel

WATAFITI nchini Israel wanasema, wamegundua pango refu zaidi duniani la chumvi.

Njia na vichochoro vyenye urefu wa kilometa 10 ndani ya pango la Malham, linaloelekea katika bahari ya chumvi inayopakana na Jordan upande wa mashariki na Israel, na ukingo wa magharibi, upande wa magharibi, vilivyowekwa kwenye ramani miaka miwili iliyopita.

Eneo hilo jangwani ni karibu na eneo ambako kwa mujibu wa Biblia, mkewe Lutu aligeuzwa kuwa nguzo ya chumvi.

Wataalamu wanasema wanatarajia mvua kulirefusha pango hilo zaidi kadri muda unavyosogea.

Hili hufanyika wakati maji ya mvua yanapotiririka ndani ya upenyo wa pango hilo na kuyeyusha chumvi na kuunda njia zenye mlalo nusu, zinazotiririka na kuelekea kwenye bahari ya chumvi.

Sehemu ya pango hilo la Malham linalopitia Mlima wa Sodom, tayari lilikuwa limewekwa kwenye ramani katika miaka ya 1980.

Miaka miwili iliyopita, Yoav Negev kutoka kundi la watafiti wa mapango Israel aliamua kukamilisha uchunguzi huo na kuidhinisha kikosi cha watafiti na wataalamu wa masuala ya mapango.

Kwa wakati mmoja walipokuwa wakipumua ndani ya pango hilo, Boaz Langford kutoka Chuo Kikuu cha Hebrew mjini Jerusalem, alisema wachunguzi hao walihisi kana kwamba chakula chao kimekosa kiungo.

"Basi tulikata chumvi kutoka mojawapo ya mawe na tukaitumia," alisema.

Malham imechukua rekodi ya miaka 13 inayoshikiliwa tangu mnamo mwaka 2006 na pango lingine la chumvi lijulikanalo kama Cave of the Three Nudes, lenye urefu wa kilometa 6.85 katika kisiwa cha Qeshm nchini Iran, watafiti wameongeza.

**BBC**

TAKWIMU

# Idadi ya wazee yapiku ile ya watoto duniani

KWA mara ya kwanza katika historia, kuna wazee wengi duniani kuliko watoto, kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN).

Takwimu zinaonyesha kuwa, watu wenye umri wa miaka 65 ni wengi zikilinganishwa na za wale walio chini ya miaka mitano kufikia mwishoni mwa mwaka 2018.

Kwa sasa kuna watu takriban milioni 705 wenye miaka zaidi ya 65 duniani, wakati wale wenye umri kati ya miaka 0-4 ni takriban milioni 680.

**WATOTO WACHACHE**

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti na Tathmini ya Masuala ya Afya wa Chuo Kikuu cha Washington, Christopher Murray, ameiambia BBC kwamba kutakuwa na watoto wachache sana na watu wengi walio na umri wa miaka zaidi ya 65, hali itakayowia vigumu kwa dunia kuendelea.

"Fikiria kuhusu athari za kisosholojia na kiuchumi kwa jamii yenye watu wenye umri mkubwa wengi kuliko watoto," anasema.

Mwaka 1960, uwiano wa uzao ulikuwa karibu watoto watano kwa mwanamke mmoja, kwa mujibu wa Benki ya Dunia (WB).

Karibu miaka 60 baadaye, uwiano huo umeongezeka kwa 2:4 tu.

**IDADI YA WAZEE**

Tatizo la uwepo wa wazee wengi ni kubwa katika nchi zilizoendelea.



Jamii za kiafrika huzaa sana lakini zina vifo vingi vya watoto. **PICHA: MTANDAO**

Kuna kasi ndogo ya kuzaliwa watoto kwa sababu kadhaa ikiwamo sababu za kiuchumi, idadi ya vifo vya watoto kuwa ndogo, njia za kupanga uzazi kupatikana kwa urahisi na ni gharama kulea watoto.

Katika nchi hizo, wanawake hupata watoto wakiwa na umri mkubwa, hivyo kuwafanya kuwa na watoto wachache.

Mazingira mazuri ya maisha yao yanamaanisha kuwa watu 'huishi maisha marefu' kwenye nchi zilizoendelea.

Mfano Japan, watu huishi mpaka karibu miaka 84 (umri mkubwa zaidi duniani).

Hali hii imeiogopesha Japan kwa miongo kadhaa na mwaka jana serikali ilitangaza ongezeko la umri wa kustaafu kutoka miaka 65 mpaka 70.

Ikiwa suala hili litapitishwa, wafanyakazi nchini Japan, watachelewa kustaafu kuliko sehemu nyingine yeyote duniani.

Nchini China watoto wa umri wa chini ya miaka mitano ni chini ya asilimia 6 ya watu wote.

**AFRIKA**

Nchi za kiafrika ni miongoni mwa nchi ambazo ziko kwenye njia panda kuhusu masuala ya uzazi.

Viwango vya uzazi viko juu mno na hakuna uwiano kati ya idadi ya watu na ubora, Niger ikiwa moja ya nchi hizo.

Hata hivyo, nchi hizo hizo zina idadi kubwa ya vifo vya watoto. Niger ikiwa na vifo 85 vya watoto katika kila watoto 1000, idadi kubwa duniani.

**ATHARI ZA KIUCHUMI**

Kuwa na idadi kubwa ya wazee kuna maana nguvu kazi ndogo, ambapo kunaweza kusababisha kushuka kwa uchumi wa nchi.

Mwezi Novemba mwaka jana, Shirika la Fedha Duniani (IMF) lilitahadharisha kuwa uchumi wa Japan unaweza kushuka kwa kiasi cha zaidi ya asilimia 25 katika kipindi cha miaka 40 ijayo, kutokana na uwepo wa idadi kubwa ya wazee.

Je, teknolojia inasaidia kupunguza madhara ya kiuchumi ya watu wenye umri mkubwa?

**SERA NA SIASA**

Kuna makubaliano, kuwa serikali zinapaswa kuchukua hatua kupambana na hali hii na zimekuwa zikijaribu kufanya hivyo.

China ilipitia tena sera yake ya 'mtoto mmoja' mwaka 2015 na mwaka 2018 ilitangaza kuachana na sera hiyo ifikapo mwakani.

Nchini China walizaliwa watoto milioni 15.2 mwaka 2018, idadi ndogo katika kipindi cha zaidi ya miaka 60.

Wasomi nchini China wameeleza kupungua kwa wanawake wenye umri wa kuzaa na familia kuacha mipango ya kuwa na watoto kwa sababu za kifedha, haswa katika familia zenye wanawake wengi walio wasomi ambao hukataa kuwa walezi wakuu.

Wataalamu wa masuala ya idadi ya watu wanasema kuwa sera zinazozingatia afya za wazee zinapaswa kutumika kupunguza madhara.

Hoja ni kuwa watu walio na afya njema wana uwezo zaidi wa kufanya kazi kwa muda mrefu na nguvu zaidi, hali ambayo itapunguza gharama za matibabu.

Nchi zenye ushirikishaji wa nguvu kazi kubwa kwa wanawake, uchumi wake huwa hauporomoki mara kwa mara kwa sababu nguvu kazi yenye wanawake wengi huwakilisha chombo chenye nguvu cha kupambana na umaskini.

**BBC**

JE, WAJUA?

# Ajifungua juu ya mti wakati wa mafuriko

MWANAMKE mmoja amejifungua mtoto juu ya mti wa mwembe alipokuwa akiyakwepa mafuriko katika eneo la kati nchini Msumbiji, yaliyosababishwa na kimbunga Idai.

Mama huyo afahamikaye kwa jina la Amélia alijifungua mtoto wa kike, Sara, alipokuwa juu ya mti pamoja na mtoto wake wa kiume, mwenye umri wa miaka miwili.

Familia yao iliweza kuokolewa siku mbili baadaye na majirani, kufuatia dhoruba ambayo imeua watu 700 nchini mwake.

Tukio hili linakuja takribani miongo miwili baada ya mtoto mwingine kuzaliwa katika mazingira kama hayo.

Mtoto huyo, Rosita Mabuiango alizaliwa wakati wa mafuriko yaliyokumba maeneo ya Kusini mwa Msumbiji.

"Nilikuwa nyumbani na mwanangu wa kiume mwenye umri wa miaka miwili ambapo ghafla, bila onyo lolote, maji yalipoanza kuingia ndani ya nyumba yetu," Amélia aliliambia Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF).

"Sikuwa na njia nyingine ila kukwea mti... nilikuwa peke yangu na mtoto wangu wa kiume," aliongeza:

Amélia na familia yake kwa sasa wanaishi katika makazi ya muda ya msaada karibu na Dombe na wanaarifiwa kuwa katika afya nzuri.

Rosita Mabuiango, ambaye sasa ana umri wa miaka 19, aligonga vichwa vya habari za kimataifa baada ya yeye na mama yake Sofia, kuokolewa na helikopta kutoka kwenye mti uliokuwa umezingirwa na maji ya mafuriko.

Akizungumza na magazeti nchini humo Mail na Guardian, Sofia alisema kuwa alikuwa na uchungu 'mkali, mkali sana.'

"Nilikuwa najaribu kulia, kupiga mayowe. Wakati mwingine nilifikiri mtoto alikuwa anatoka, lakini wakati mwingine nikafikiri ilikuwa ni kwa sababu ya njaa," alisema.

Aliongeza kuwa: "Watu wengi walipoteza kila kitu katika mafuriko, lakini walau nilipata kitu."

Lakini katika mazungumzo na BBC, Rosita alisema kuwa ahadi za serikali ya Msumbiji za kumlipia masomo na ahadi ya kumlipia gharama ya safari ya Marekani iliyotolewa na serikali ya Marekani zote hazijatimizwa.

"Masomo yangu yamekuwa wakati wote yakigharimiwa na mama yangu, sijapokea chochote kutoka kwa serikali," alisema Rosita na kuongeza:

"Sawa, nyumba tulijengewa na serikali lakini kwa sasa haiko katika hali nzuri, mvua inaponyesha nyumba inavuja... Walau wangesaidia kuikarabati." **BBC**



Amélia aliyejifungua wakati wa dhoruba iliyoua watu zaidi ya 700 nchini Msumbiji, kufuatia kimbunga Idai, akiwa na binti yake, Sara. **PICHA: MTANDAO**

# UCHAMBUZI WA KITABU

## NA DK. RAYMOND NUSURA MGENI

HABARI rafiki upendaye maarifa na mwenye shauku ya kufanikiwa.

Kitu kikubwa kinachowatofautisha waliofanikiwa kwa viwango vya juu na wengine kuwa chini ni namna ya kufikiri na namna ya kutenda au kufanya mambo.

Hiki ndicho ambacho kilimsukuma mwandishi Scot Anderson atuandikie kitabu hiki cha namna ya kufikiri kama bilionea na kuwa bilionea.

Idadi ya watu ambao wamefikia ngazi ya ubilionea ni ndogo ukilinganisha na idadi yote ya watu duniani, ambayo ni zaidi ya bilioni 7.

'Vile mtu aonavyo nafsini mwake ndivyo alivyo ni moja ya nukuu maarufu.' Ni dhahiri kabisa kuwa mawazo huchangia ufanyikaji wa kitu.

Ufanyikaji wa kitu kuwa bora huwa ni zao la fikra bora. Na hili ndilo linaweza kufanya watu wengine wafanikiwe na wengine washindwe kufanikiwa.

Msingi wa kufanikiwa ni kufikiri na kutenda sawa na ulivyofikiri. Lazima pawepo na msawazo wa kile unachokifikiri na kile utakachoenda kukifanya.

Vile watu watakavyo na kutaka siku wawe mabilionea lazima kuanza kufikiri kibilionea na kutenda kama watendavyo mabilionea.

Kuna mambo 7 ya jinsi mabilionea hufikiri na kutenda tofauti na watu wengine wanavyoyafanya.

Mambo haya tukiyafanyia kazi kuanzia kufikiri kwetu hadi kwenda kutenda, basi tuna nafasi kubwa ya kufanikiwa kama mabilionea walivyoweza kufanikiwa.

Eneo la kwanza ni juu ya kuifikiria fedha kama njia ya kupata vitu vingine, ndipo ulipo utofauti na mabilionea wafikiriavyo pale wao wanapoona fedha ni zana ya kiuwekezaji.

Kwa kila fedha wanayopata wanafikiri namna ya kuiwekeza ili iwatengenezee utele baadaye wa kupata chochote wakitakacho. Ili ufanikiwe zaidi kila fedha utakayopata fikiri namna ya kuiwekeza na kuizidisha, utapata mafanikio makubwa.



Ni utofauti wa kufikiri ili kuwa na mafanikio katika maisha. **PICHA: MTANDAO**

# THINK LIKE A BILLIONARE BECOME A BILLIONARE

## Fikiri kama bilionea kuwa bilionea

**UWEKEZAJI**

Eneo la pili ni uwekezaji. Uwekezaji kwa wengine hufikiri kama njia ya kuwa na fedha ya kutosha baada ya kustaafu na huku waliofanikiwa na kufikia ngazi za juu za mafanikio kwao uwekezaji ni kipaumbele cha kwanza cha kuwatengenezea utele.

Kuanzia kusoma vitabu, kulipia semina, afya zao na uhusiano.

Uwekezaji wao wanaofanya kwao una lengo la kuwatengenezea utele na fursa tele sasa na siku zijazo na hii hufanya fursa zibishe hodi kwao bila kikomo.

**AJIRA**


Eneo la tatu ni ajira au kazi. Huku wengine wakifikiri kuwa wakipata kazi nzuri au ajira itakuwa njia ya kuwa na utajiri, wao wanafikiri kazi kama njia ya uwekezaji uzalishao uzoefu, ujuzi na maarifa kwa ajili ya kutengeneza thamani kubwa zaidi sasa na baadaye.

Kazi kwao ni mbegu ya wao kupata uzoefu ambao utakuwa mtaji kwa siku za baadaye za kufanya makubwa, sababu ya kutumia kazi kama njia ya uwekezaji.

HATARI

Eneo la nne ni hatari. Wengine wanakimbia kuchukua hatua katika maisha kwa hofu ya kushindwa au kufikiri watu watawaonaje, na huku waliofanikiwa wanaona hatari zaidi kukaa bila kuchukua hatua katika maisha.

> "Hivyo kipaumbele chao cha kusimamia muda ni kikubwa tofauti na watu wengine ambao wako tayari kupoteza muda na hawahisi kama wamepoteza raslimali muhimu kwa maisha yao.




Kadri wao wanavyoweza kuchukua hatua nyingi na kukutana na kufeli ndivyo wanavyojitengenezea nafasi kubwa ya kufanikiwa.

Wao kila siku kwao ni fursa ya kuziendea hatari maana wanaamini ndizo zilizobeba mafanikio yao.

**CHANGAMOTO**

Eneo la tano ni matatizo. Waliofanikiwa katika maisha yao wanaamini kuwa kupitia matatizo au changamoto ndipo ilipo njia ya mafanikio.

Maana kwa kutatua matatizo ya jamii, ndivyo wanavyokuza thamani zao na kupata wakitakacho kwa kuwa huwapa watu wakitakacho kwa kuwatatulia matatizo yao.

Siku zote huwa wanakimbilia kuona fursa zinazoletwa na matatizo kama fursa ya wao kupiga hatua kubwa zaidi.

**MAANDALIZI**

Eneo la sita ni maandalizi. Wao wanaamini kadri unavyojiandaa mapema katika maisha, ndivyo itakavyokuwa bahati kwako kwamba kila fursa itakayokuja itakukuta uko tayari na utaweza kupiga hatua.

Wao kila siku wanatumia na kufikiria namna ya kutengeneza ijayo wakiwa bado hawajaifikia.

Kutengeneza mapema nafasi kwao ndiko kunakofanya wengine wawaone watu wenye bahati...wasijue wakati wengine walipokuwa wanapoteza siku bila kujiandaa wao walikuwa wakijiandaa kwa kukaribisha mafanikio katika kesho zao.

Maarifa kwa watu waliofanikiwa, wanaamini ndio mhimili mkuu katika mambo yote.

Ndio maana wanawekeza fedha zao kwenye maandalizi, muda, katika kupata maarifa ya kutosha kufanya wafanikiwe na kupiga hatua za juu.

Hii ni tabia ambayo utaiona kwa mabilionea wengi, kuwa fikra zao ni bora sababu ya uwekezaji kwenye maarifa na hekima kama mwanga wa mafanikio yao.

**MUDA**

Eneo la saba ni muda. Wanaamini kuwa fedha ikipotea wana uwezo wa kuzipata na kuzidi maana wanayo mifumo inayojiendesha ya kufanya wao wafanikiwe.

Ila kwao muda wanaupa uzito, wakijua unapopotea hakuna namna ya kuweza kuuzidisha tena.

Hivyo kipaumbele chao cha kusimamia muda ni kikubwa tofauti na watu wengine ambao wako tayari kupoteza muda na hawahisi kama wamepoteza raslimali muhimu kwa maisha yao.

Haya ni mambo 7 ambayo tukibadili kufikiri na kutenda kama wanavyofanya waliofanikiwa, basi nasi kuna siku tutafika walipo wao na kusogea hatua zaidi.

Chukua kila eneo na ona kitu cha kufanyia kazi na maisha yako hayatakuwa kama yalivyo sasa.

Inawezekana kama tukibadilika, kwa kufikiri kama mabilionea na kuwa kama mabilionea kwa kutenda.

**Na Dk. Raymond Nusura Mgeni, mchambuzi wa vitabu, anapatikana kwa namba 2019 +255 676 559 211 raymondpoet@yahoo.com**



WADAU **SABATO KASIKA**

# SERIKALI imeruhusu wanafunzi waliofaulu kidato cha nne 2018 na wanaotegemea kujiunga na kidato cha tano na vyuo mwaka huu, kubadilisha tahsusi (Combination) kulingana na ufaulu wao.

Wadau wanasemaje?



**SAMSON NTOKE MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM**

KWANZA ninaipongeza serikali kwa fursa hiyo iliyotoa kwa wanafunzi, kwani wapo baadhi yao walikuwa wakishindwa kutimiza ndoto zao kutokana na kupangiwa moja kwa moja michepuo kati ya chaguo zao tatu walizokuwa wanachagua.

Kuna wengine walikuwa wakijikuta wakipangiwa mchepuo katika chaguo lao la tatu na siyo walivyotarajia.

Pamoja na fursa hiyo, ambayo serikali imetoa, kwa upande mwingine itawafanya baadhi ya wanafunzi kushindwa kutimiza malengo yao, kwani kwa kufuata ufaulu, wapo watakaolazimika kuchagua mchepuo fulani ambao hawakuupenda, kwa kuwa mchepuo huo umetokea kwa bahati tu wakafanya vizuri na kujikuta hawana namna ya kukwepa kuchagua michepuo wanayoipenda, kwa hofu ya kukosa nafasi, kwasababu ya ufaulu hafifu wa masomo ya mchepuo wanaoupenda.

Changamoto nyingine inayoweza kutokea katika fursa hii ni pale ambapo serikali itajikuta inapata ugumu wa kuweka uwiano wa michepuo iwapo wanafunzi wengi watafaulu na kuchagua michepuo inayofanana.

Hivyo ninashauri serikali iangalie uwezekano wa kuweka vigezo zaidi ili kufanikisha mpango huu unaolenga kuwasaidia wanafunzi kutimiza ndoto zao.



**LOYCE KABUCHE (MWANAFUNZI CHUO KIKUU MZUMBE, MOROGORO)**

HATUA iliyochukuliwa na serikali ni sahihi kabisa inafaa kuungwa mkono, kwa sababu itamsaidia mwanafunzi kuchagua tahasusi anayoipenda, pia itampa nafasi ya kufikia kusomea kile anachokipenda na siyo kwa kuchaguliwa na hivyo kulifanya taifa kuwa na wasomi wengi wenye taaluma kwa kile wanachokipenda katika maisha yao au kutimiza ndoto zao.

Siyo kusomea sayansi tu na kujikuta waliosomea upande huo wanakuwa ni wengi hadi kukosa ajira kabisa, wakati sekta ya biashara hutakiwa watu wengi, lakini wanakosekana kutokana na kutokuwapo kwa wasomi kwenye sekta hiyo.

Lakini bahati nzuri serikali imetoa fursa ambayo wanafunzi hawana budi kuichangamkia kwa kuangalia upya ni namna gani wanaweza kujipanga katika elimu ili waweze kufanikiwa.

Ninaamini kwamba kila mmoja atarekebisha uchaguzi wake wa awali kulingana na jinsi alivyofaulu katika matokeo ya kidato cha nne mwaka jana ili apambane upya na hali yake na hatimaye kutimiza ndoto yake aliyojipangia kwa ajili ya maisha yake ya baadaye.



**MARCELINA MGUTU (MHITIMU WA KIDATO CHA NNE MWAKA 2018)**

MIMI kama mhitimu wa kidato cha nne, nimefurahishwa na kile ambacho kimefanywa na serikali yetu, kwani imetupatia fursa zaidi sisi wahitimu kuchagua kile kinachoendana na uwezo wetu zaidi, kwasababu baada ya matokeo ndipo mhitimu anajua mwelekeo wake kuliko hata pale ambapo hajauona mtihani halafu anatakiwa kuchagua.

Hivyo kwa asilimia kubwa ninaipongeza serikali kwa hatua hii ambayo itasaidia wanafunzi wengi kuendelea kutimiza ndoto zao katika elimu na kuibadilisha Tanzania kuwa ya wasomi wengi zaidi watakaochangia katika maendeleo.

Ikumbukwe kwamba hakuna nchi inayoweza kuendelea bila kuwa na wasomi, hivyo kwa jinsi ambavyo serikali imeamua, ni wazi hapo baadaye nchi hii itakuwa na maendeleo makubwa, kwa sababu itakuwa na wasomi wengi kwa maana ya wataalamu wa fani mbalimbali kuliko ilivyo sasa.

Niwahimize wanafunzi wenzangu tuliohitimu kidato cha nne mwaka 2018 tusipoteze fursa hii, ambayo serikali imetoa kwa ajili yetu.

Kila mmoja wetu anajua amepata alama gani kwenye mtihani wa kidato cha nne, amepewa nafasi ya kubadili tahasusi.



**SAID AMRAN (MWALIMU MBEZI HIGH SCHOOL DAR ES SALAAM)**

MAONI yangu ni kwamba uamuzi huo wa serikali ni sahihi kabisa na inaonyesha ni jinsi gani inavyodhamiria kumsaidia kielimu mtoto wa Kitanzania.

Kilichofanyika ni kuhakikisha wale wote wenye sifa (credit 3) wapate nafasi ya kuendelea na masomo ya kidato cha tano bila kukwazwa na machaguo yao ya awali, jambo ambalo siku za nyuma lilisababisha baadhi ya shule za serikali kukosa wanafunzi na kubaki wazi, hali ambayo kwa sasa haitatokea tena.

Kwa hiyo ninachukua nafasi hii kuipongeza serikali kwa uamuzi huo wa busara.

Tunaomba uamuzi huu uendane na ongezeko la walimu katika shule, yaani wasiajiriwe walimu wa sayansi tu bali na wa masomo mengine, kwani sasa wahitimu wanajipanga upya kwa ajili kubadili machaguo yao ya awali.

Kama watabaini hawakufanya vizuri kwenye baadhi ya masomo watajikita zaidi katika masomo ya fani ambayo itawaandaa kuwa na wataalamu wazuri katika maisha yao ya baadaye kwa jinsi walivyojipangia katika ndoto zao.



**DOMICA BALAMA (MWALIMU GENESIS SCHOOLS DAR ES SALAAM)**

HII ni fursa nzuri sana tena sana, kwani mara nyingi watoto hawa huwa hawapewi nafasi ya kuchagua nini cha kusoma zaidi ya kupangiwa na walimu kulingana na ufaulu.

Wapo ambao wangependa kusoma sayansi, lakini wanaambiwa hawawezi badala ya kusaidiwa ili waweze na hivyo kutupwa kwenye michepuo mingine.

Kwa hiyo fursa hii itawapa wao nafasi ya kuchagua wanachokipenda. Lakini pamoja na uzuri wa fursa, bado kuna changamoto ninayoiona, kwani siyo wote watakaonufaika nayo.

Watoto wa vijijini ambao kompyuta wanaziona kwenye michoro watakuwa na uwezo wa kufanya chaguzi hizi? Je, ni jitihada zipi zimefanywa kuhakikisha kila mhusika ananufaika na fursa hii nzuri?

Changamoto nyingine ninayoiona ni kwamba fursa hii inaweza kutumiwa vibaya na baadhi ya wazazi na walezi wanaotaka watoto wao wasome kitu fulani. Serikali ifanye kila njia kuhakikisha kila mtoto ananufaika na fursa hii bila kuingiliwa.

Wazazi na walezi wakae pembeni na pia kwa upande wa wanafunzi wa vijijini, wasaidiwe kwa namna yoyote ya kuweza kufanikisha malengo yao kulingana na mazingira wanayoishi.





# RC Chalamila sasa atangaza vita wanaopuuza malalamiko

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ametishia kuwafukuza kazi watumishi watakaobainika kuwazuia wananchi wanaofika katika Ofisi za Mkoa kwa lengo la kuwasilisha kero mbalimbali zinazowakabili.

Chalamila alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ambapo alieleza kuwa vitendo hivyo vimekuwa vikikwamisha jitihada za serikali za kusikiliza na kuzitafutia ufumbuzi kero zinazowakabili wananchi.

Alisema serikali haitawavumilia watumishi wenye tabia ya kuwazuia wananchi kutoa kero zao kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa sababu zao binafsi.

"Ole wake mtumishi yeyote atakayebainika kuwazuia wananchi kuonana na mimi ili wasitoe kero zao, atafukuzwa kazi muda huo huo hatuwezi kuwavumilia watu wa namna hiyo kama mtu hajiamini na utendaji kazi wake akae pembeni," alisema Chalamila.

Baadhi ya wananchi kutoka Stendi ya Kabwe jijini Mbeya, walimweleza Mkuu huyo kuwa baadhi ya watumishi wamekuwa wakizuia kutoa kero zao katika Ofisi ya Mkoa, huku wakitoa sababu mbalimbali kwamba Chalamila katingwa na kazi.

Miongoni mwa wananchi hao Lupakisyo Mathias alieleza kuwa kitendo cha watumishi hao kutowaruhusu wananchi kuonana na Mkuu wa Mkoa kwa ajili ya kutoa kero zao kinawakatisha tamaa na kuona mkuu huyo hawatumikii wananchi kama anavyodai kwenye mikutano yake ya hadhara.

Alisema kutokana na changamoto wanazozipata wakifika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, wameona wametengwa na hawezi kusaidia shida zao na matokeo yake kumuona mkuu huyo atimizi wajibu wake ipasavyo.

"Mkuu wa Mkoa anaangushwa na baadhi ya watumishi katika ofisi yake hawako tayari kutoa ushirikiano kwa wananchi wanaowasilisha kero zao kwenye Ofisi ya Mkoa, ndio maana hata wengine wanatafuta njia mbadala za kufikisha dukuduku zao kwa viongozi wa kitaifa wakifika, tunaomba Mkuu wa Mkoa atumbue majipu ndani ya ofisi yake," alisema Lupakisyo.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Mkoa wa Mbeya amepiga marufuku kwa taasisi zote zinazohusika na ukusanyaji kodi na ushuru kuacha tabia ya kuwatoza kodi madereva bajaji na bodaboda ambao tayari wanavitambulisho vya wajasiriamali.

Alisema wajasiriamali hao wasitozwe kodi au ushuru wa aina yoyote kwa kuwa tayari wamekwisha toa fedha ya vitambulisho vya ujasiriamali kwa mujibu wa maelekezo ya Rais Dk. John Magufuli na kwamba wako huru kufanya kazi zao.



Mbunge wa Rorya mkoani Mara, Lameck Airo, akizungumza katika harambee ya kuchangia Sh. milioni 360 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika shule za sekondari za tarafa ya Suba jimboni humo, iliyofanyika jijini Dar Salaam juzi, ambapo aliahidi kuchangia shilingi milioni tano. Kulia ni Katibu wa Kamati ya maandalizi ya harambee, Pilly Marwa na Mwenyekiti, Chacha Nshoya. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Serikali yaanza kutoa elimu wanufaika Tasaf

**Na Grace Mwakalinga, KYELA**

SERIKALI Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya kupitia mpango wa kuzinusuru kaya maskini (TASAF), imeanza kutoa elimu ya matumizi bora ya fedha ili walengwa 4,764 waweze kunufaika kwa kuanzisha shughuli za ujasiriamali na kilimo.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia Kitta, alisema lengo la kutoa elimu ya matumizi bora ya fedha limezaa matunda kwa kuwa tayari walengwa kupitia fedha hizo wameanzisha shughuli mbalimbali za kujiingizia kipato ikiwamo ujasiriamali na kilimo.

Claudia alisema wataalamu wa wilaya hiyo, wameweka utaratibu kutoa elimu ya matumizi bora ya fedha kwa wanufaika kupitia kila dirisha la malipo linapofunguliwa.

Alisema TASAF imeongeza nguvu katika ukusanyaji wa mapato kwa kuwa kila kundi linaloishi katika mazingira magumu limekuwa mstari wa mbele kiingiza katika shughuli za uzalishaji.

"Mfuko huu umewagusa hata wananchi ambao ni waathirika wa VVU, ambao walikuwa hawana uwezo wowote wa kujipatia chakula na sasa wameongeza uzalishaji na kubakisha akiba ya vyakula tunamshukuru Rais Magufuli kwa kuzisaidia kaya maskini ambazo sasa zinafanya shughuli ndogondogo za kimaendeleo na kuinua kipato chao," alisema Claudia.

Mbali na wilaya hiyo kuendelea kutoa elimu ya matumizi bora ya fedha kwa kaya maskini kupitia TASAF, wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo watendaji kuchelewa kufika katika eneo la malipo kwa ajili ya walengwa.

Alisema changamoto hiyo inasababisha usalama mdogo wa fedha za walengwa, hivyo Mkuu wa Wilaya aliwataka watendaji wote wa TASAF kuwahi kufika eneo la malipo ili kuondoa changamoto ya usalama kwa wapokeaji wa fedha hizo.

Baadhi ya kaya ambazo zimeunda vikundi walidai kunufaika kwani kupitia fedha hizo wameweza kukopeshana.

Miongoni mwa vikundi vya wanufaika wa TASAF ni Kikundi cha Mwamko kilichopo katika Kijiji cha Kilombero Kata ya Mababu ambacho hadi sasa kimefanikiwa kukusanya fedha kiasi cha shilingi milioni 1,500,000 kwa wanachama 20.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Essah Ijande, alisema elimu ya matumizi bora kupitia mpango wa kuzinusuru kaya maskini wa TASAF, uliwasaidia kuunda kikundi ili wajitegemee na kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi zinazopatikana katika wilaya hiyo.

Alisema lengo la kikundi hicho kwa baadaye ni kununua mashine ya kusaga na kukoboa nafaka, kununua shamba lao la kudumu, kufungua akaunti benki pamoja na kupata usafiri wa baiskeli ya kikundi.

# Waomba kuboresha miundombinu ya elimu

**Na Mwandishi Wetu, MBEYA**

WALIMU mkoani Mbeya wameiomba serikali kuboresha mindombinu ya elimu ikiwamo vyumba vya madarasa, vifaa vya kujifunzia na kufundishia pamoja na maslahi ya walimu.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Mkoa Mbeya, Anthon Mwaselela, wakati akizungumzia maandalizi ya sherehe za Mei Mosi ambazo kitaifa zitafanyika mkoani Mbeya.

Mwaselela alisema walimu wanakutana na changamoto mbalimbali wanapotimiza majukumu yao kama vile kutumia umbali mrefu kufuata huduma za kijamii ikiwamo hospitali, taasisi za kifedha na maji pamoja na uhaba wa nyumba za walimu.

Alisema kada ya walimu ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya taifa haithaminiwi kwa sababu wadau na serikali imeshindwa kuboresha miundombinu ya elimu na kusababisha walimu kutimiza majukumu yake kwenye mazingira magumu.

"Mazingira yetu ya kazi ni magumu kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa, vitendea kazi pamoja na nyumba za walimu hali inayosababisha tushindwe kutumiza majukumu ipasavyo tunaiomba serikali iboresha miundombinu ikiwamo kuongeza vifaa vya kufundishia katika kila shule za sekondari na msingi," alisema Mwaselela.

Aidha, Mwaselela aliiomba serikali kuwatazama kwa jicho la tatu walimu wanaofanya kazi vijiji kwa sababu wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo mrundikano wa wanafunzi kwenye darasa moja ukilinganisha na idadi ya walimu pamoja na madarasa yalipo.

Aliomba kuongeza kasi ya upandishaji madaraja na mishahara walimu hasa wanaotoka kumaliza masomo itasaidia kuongeza motisha kwa wafanyakazi na kufanya kazi kwa bidii.

Amesema baadhi ya walimu wanaomaliza masomo hawaongezewi mishahara na kupandwa madaraja kama walivyokuwa wanatarajia hali inayoshusha morali na ubunifu na kusababisha walimu kufanya kazi kwa manung'uniko.

Baadhi ya walimu mkoani Mbeya walisema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni kutolipwa stahiki zao kwa wakati na baada ya kumaliza masomo hawarekebishiwi madaraja yao ya awali.

**"Mazingira yetu ya kazi ni magumu kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa, vitendea kazi pamoja na nyumba za walimu hali inayosababisha tushindwe kutumiza majukumu ipasavyo tunaiomba serikali iboresha miundombinu ikiwamo kuongeza vifaa vya kufundishia katika kila shule za sekondari na msingi," alisema Mwaselela.**





# Kamanda Muroto atangaza kuchakaza watakaoandamana

Na Paul Mabeja, DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma limepiga marufuku maandamano yaliyopangwa kufanywa leo na vijana wa Chama cha ACT- Wazalendo kwa kushirikiana na vyama vingine vya siasa vikiwamo NCCR-Mageuzi, Chauma na UPDP.

Aidha, jeshi hilo limesisitiza kuwa kwa yeyote atakaye kaidi na kufanya maandamano hayo atapigwa hadi atachakaa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema kuwa kuna taarifa ambazo zimewafikia kuwa leo vijana wa ACT- Wazalendo kwa kushirikiana na vyama vingine vya siasa.

"Wanatarajia kufanya maandamano siku ya Jumanne ya tarehe 9 mwezi huu, waliyoyapa jina kuwa ni maandamano ya amani wakiwa na lengo la kushinikiza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza mambo yafuatayo," alisema Muroto.

Aliyataja mambo hayo kuwa ni pamoja na kumshinikiza Spika wa Bunge kufuta azimio la Bunge kutofanya kazi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Profesa Mussa Assad na kuweka kwenye shughuli za Bunge (Oder Paper) upokeaji wa taarifa za CAG ikiwa na saini yake ifikapo tarehe 10 mwezi huu saa 3 asubuhi.

Alisema kutokana na taarifa hizo zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii, jeshi hilo Mkoa wa Dodoma limetangaza marufuku ya maandamano hayo kufanyika kwa kuwa hayana kibali.

"Tunapenda kuwatahadharisha wananchi kuepuka kujiingiza katika mkumbo wa uhamasishaji wa maandamano haya kwani wasije wakaingia katika mikono ya serikali kutokana na kuvunja sheria za nchi," alisema Kamanda Muroto.

Alisema kuwa mtu yeyote asijaribu wala kuthubutu kujitokeza kufanya maandamano kwani atakayejitokeza kwa maandamano hayo atapigwa hadi atachakaa.

"Tutambue kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni muhimili unaojitegemea na hautakiwi kuhojiwa nje ya Bunge, kwa kuwa wanaohoji mipango na maazimio ya Bunge wamo ndani ya Bunge ambao ni wabunge wenyewe walichaguliwa na wananchi ili kuwawakilisha," alisema.

Aliongeza kuwa vijana wanatakiwa kujitambua na kuelewa kuwa wao ni nguvu kazi ya taifa wanaotegemewa katika kuinua uchumi wa nchi badala ya kutumika kama zulia kwa kupoteza muda mwingi katika kushawishi na kuhamasisha maandamano ambalo ni kosa la jinai.

Muroto alisema kuwa jeshi hilo linawaondoa wasiwasi wananchi wanaoendelea na shuguli zao kutokuwa na hofu, kwa kuwa wataendelea kupata ulinzi kama ilivyo kawaida.



Wafanyakazi wa Shirika la Reli wakilibomoa jengo la kanisa la The Gospel Ministry Church (GMC) kwenye zoezi linaloendelea la kuyaondoa majengo yote yaliyojengwa kwenye hifadhi ya barabara ya reli jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wananchi walalamikia kukosa fursa ya ajira

Na Paul Mabeja, CHAMWINO

WAKAZI wa Kata ya Mlowa, wilayani Chamwino mkoani Dodoma, wamelalamikia kutokujumuishwa katika fursa za ajira za ujenzi wa hospitali ya wilaya inayojengwa katika eneo hilo na badala yake wamepewa watu kutoka nje ya eneo lao.

Aidha, wamesema hata kinamama wanaopata vibarua katika mradi huo wamekuwa wakipewa malipo kidogo ambayo hayakidhi mahitaji ya kila siku licha ya kazi kubwa wanayoifanya.

Wakazi hao waliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Utekelezaji ya Jumuiya ya Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Dodoma, waliotembelea mradi huo ikiwa ni sehemu ya kuangalia utekelezaji wa Ilani ya chama hicho katika Wilaya ya Chamwino.

Mmoja wa wakazi hao, Paulina Mapuga, alisema kuwa hawapati fursa ya kupata ajira katika mradi huo kwani wengi waliopata ni kutoka katika maeneo ya mbali.

"Ni kweli tumepata fursa ya hospitali ya wilaya kujengwa katika eneo letu tunaishukuru sana serikali, lakini wenyeji wa hapa hawapati ajira katika ujenzi huo hususani vijana wetu," alisema.

"Hata sisi kinamama tunaopata vibarua katika ujenzi huu hatupati kipato kizuri kwa siku tunalipwa 2,000 hadi 2,500 kwa wiki tunapata 10,000 hadi 12,000 hizi hazitutoshi tutajikwamua vipi na umaskini kwa namna hii tunaomba tusaidiwe kwa hilo, " alisema Mapuga.

Akitolea ufafanuzi kuhusu sula hilo kwa uongozi wa UVCCM, diwani wa kata hiyo ambaye ni mwenyekiti wa kamati ya ujenzi wa hospitali hiyo, Allani Matewa, alisema tatizo kubwa linalosababisha ni mafundi wanaotekeleza mradi huo kutokuwa na uwezo kiuchumi na wakati mwingine kutokana na matakwa ya mikataba ambayo hutolewa na serikali.

"Tatizo kubwa lipo katika mikataba hii na ukizingatia mafundi wanaotumiwa ni hawa tunao waita 'local fundi' ambao hawana uwezo katika masuala ya fedha, hivyo ndio husababisha haya yote," alisema.

**"Hata sisi kinamama tunaopata vibarua katika ujenzi huu hatupati kipato kizuri kwa siku tunalipwa 2,000 hadi 2,500 kwa wiki tunapata 10,000 hadi 12,000 hizi hazitutoshi tutajikwamua vipi na umaskini kwa namna hii tunaomba tusaidiwe kwa hilo, " alisema Mapuga.**

# Wananchi watinga bungeni kumsaka Lukuvi

Na Paul Mabeja, DODOMA

WAKAZI wa Kitongoji cha Kalugwebe Kata ya Iteera wilayani Kyerwa, mkoani Kagera, wametinga jijini hapa kumuona Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi.

Akizungumzia lengo la safari yao kutoka Kagera kuja jijini Dodoma kwa niaba ya wenzake 250, Augustina Augustine mkazi wa kitongoji hicho alisema wameamua kumfuata Lukuvi ili awasaidie kutatua mgogoro huo.

Augustine alisema mgogoro huo kati yao na wafugaji ulianza mwaka 2009, ambapo walilazimika kwenda mahakamani na ilipofika 2017 walishinda kesi na kukabidhiwa mashamba yao ambayo walikuwa wanayatumia kwa ajili ya kilimo.

Alisema wakati wakiendelea na shughuli zao kama ilivyo kawaida walishangaa kuona polisi wakija pamoja na mgambo kuwaondoa na kuanza kufyeka mazao yao ambayo walikuwa wameshalima.

"Polisi walituondoa wakidai yale ni maeneo ya wafugaji, lakini kimsingi sisi tulishashinda kesi mahakamani na kupatiwa haki ya kumiliki yale maeneo, lakini tunashangaa kuona kuwa tunaondolewa bila sababu yoyote," alisema.

Alisema hivi sasa familia zao zinapata shida kutokana na kukosa vyakula kufuatia kufyekwa kwa mimea yao ambayo walikuwa wanaitegemea kwa ajili ya chakula na biashara.

"Walifyeka mashamba yetu ya ndizi, pamoja na mikahawa, hivi sasa hali yetu ni mbaya sana ndiyo maana tumeamua kuja Dodoma kumuona Waziri Lukuvi ili atusaidie," alisema.

Alieleza kuwa wamekuja Dodoma kutokana na kutoa taarifa zao kwa Mkuu wa Wilaya yao pamoja na mkoa, lakini hakuna hatua zilizochukuliwa hali iliyowalazimu kufunga safari kuja bungeni ili kumuona Lukuvi.

"Waziri Lukuvi aliwahi kufika katika kitongoji chetu miaka ya nyuma na mgogoro ule anaufahamu na aliagiza ofisi ya mkoa iushughulikie, lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea ndiyo maana tumeamua kuja Dodoma ili kusaidiwa," alisema.

Alisema walifanikiwa kuonana na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, badala ya Lukuvi kwa madai kwamba alikuwa ziarani.

Mabula, aliwasikiliza wananchi hao na kumpigia simu Kamishna wa Ardhi katika eneo hilo kushughulikia mgogoro huo haraka iwezekanavyo.



# Jaji Makungu atoa neno kesi udhalilishaji, dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

JAJI Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, amesema kuwa malalamiko ya ucheleweshwaji wa kesi zinazohusu dawa za kulevya na udhalilishaji, yamepungua mahakamani.

Jaji Makungu alitoa kauli hiyo wakati akifungua mkutano wa 12 wa Chama cha Maofisa wa Makahama Zanzibar (ZAJOA), uliofanyika Taasisi ya Utalii ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

Alisema utendaji wa kazi mwaka uliopita ulikuwa mzuri na kuwapongeza watendaji wote wa mahakama kwa utendaji mzuri walioonyesha na mafanikio yaliyopatikana.

Aliongeza kwamba wajibu wa msingi wa mahakama ni kusikiliza mashauri na kuyatolea maamuzi kwa haki na haraka licha ya kuwapo changamoto mbalimbali, lakini umalizaji wa kesi ulikuwa mzuri kwa asilimia 84 mpaka Desemba 2018.

"Tumeongeza idadi ya mahakimu wa mahakama ya mwanzo, wilaya na mkoa, pamoja na kuwapadisha mahakimu mbalimbali, hivyo nawapongeza wale wote waliopata nafasi hizo na kuwataka kuwa watendaji wazuri na kuwajibika katika kazi zao," alisema.

Aliwataka wale ambao hawakupata nafasi ya kupandishwa madaraja, kutovunjika moyo kwa kuwa nafasi bado zipo na kuwataka kufanya kazi kwa juhudi ili mara nyingine na wao wapandishwe.

Kwa upande wake, Rais wa Chama cha Maofisa wa Mahakama Zanzibar, Salum Hassan Bakar, alisema chama chao hufanya mkutano kila mwaka kwa lengo la kufanya tathmini ya kazi za mwaka uliopita na kuzungumzia changamoto na mfanikio yaliyopatikana.

Alisema jumuiya yao inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa fedha, kwani hadi sasa wanategemea mapato yanayotokana na michango ya wanachama, hivyo bado wanahitaji misaada na wapo katika mikakati ya kutafuta vyanzo vingine vya mapato.



Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya NBC, Neema Singo (kushoto) akizungumza na baadhi ya wanafunzi 63 wa vyuo vikuu wanaosoma kwa kupitia Mpango wa Ufadhili wa NBC wakati wa mafunzo yaliyoandaliwa na benki hiyo kwa ushirikiano wa taasisi ya Elevate Education ya Afrika Kusini, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakumbushwa kufuatilia mahudhurio ya watoto

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

FAMILIA za watoto wanaoishi katika mazingira magumu zilizomo katika mradi wa kuimarisha familia unaotekelezwa na Shirika la Kulelea Watoto Yatima (SOS), zimetakiwa kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kufuatilia mahudhurio ya watoto wao shuleni.

Hayo yalielezwa na Mratibu wa SOS Pemba, Ghalib Abdalla Hamad, alipokuwa akizungumza na kinamama wa chama cha ushirika Zaonia katika sherehe ya kuadhimisha Siku ya Walengwa wa Mradi, iliyofanyika Maziwang'ombe Wilaya ya Micheweni, Pemba.

Alisema SOS imewawezesha kinamama kiuchumi kwa lengo la kuwalinda watoto, kuwapatia haki zao za msingi sambamba na kusaidia kuimarisha makazi yao.

"SOS katika kipindi chote hicho tulikuwa tunajengeana uwezo namna gani tutaweza tukafanikisha kufikia maendeleo ya familia zetu, katika masuala ya matunzo na malezi ya watoto wetu kupitia mbinu mbalimbali ikiwamo kuanzisha vikundi vya ushirika," alisema.

Alieleza SOS kwa kushirikiana na familia hizo wamebaini maendeleo yaliyofikiwa ikiwamo kuwarudisha watoto shule, huku wengine wakipatiwa elimu ya ufundi kama ushoni, uchoraji wa makawa na picha.

Naye Ofisa Miradi kutoka SOS Pemba, Abdalla Omar Kidimu, alisema juhudi za pamoja na ushirikiano ndio zilizowapatia maendeleo kinamama hao.

Alisema kikundi hicho kwa sasa kina akiba ya shilingi milioni tatu, huku SOS ikiwaingizia Sh. milioni 26 kwa ajili ya kutekeleza miradi yao.

Kwa upande wake mwenyekiti wa kamati inayoshughulikia watoto wanaoishi katika mazingira magumu Shehia ya Maziwang'ombe, Khamis Abdalla Hassan, aliipongeza SOS kwa kubuni mradi huo ambao una lengo la kuwakomboa watoto.

"Naipongeza SOS kwa kuwawezesha wanawake na kuwasaidia kubadili maisha yao na ya familia zao," alisema.

# Wanaoanza kampeni waonywa kuishia pabaya

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Kaskazini Unguja, Iddi Ali Ame, amewaonya viongozi ndani ya chama hicho wale wenye nia ya kugombea nafasi za uongozi mwaka 2020 kuacha kufanya kampeni mapema kwani mwenendo huo unaweza ukawaweka pabaya.

Aliyasema hayo huko Mahonda katika ukumbi wa Ofisi za CCM Mkoa wa Kaskazini Unguja wakati alipokuwa akifungua mkutano wa maadhimisho ya wiki ya wazazi mkoani humo.

Alisema muda wa kampeni bado haujafika kwa hivyo ni vyema kila mmoja kupitia jumuiya yake na chama kwa ujumla wakafanya kazi ya kukiimarisha chama na kuhakikisha wanakiletea ushindi katika uchaguzi wa 2020.

Alisema kuwa mtu yoyote atakaye bainika anapiga kampeni mapema kabla muda haujafika atamchukulia hatua za kinidhamu na mtu huyo anaweza kupoteza sifa za kugombea kwa mujibu wa taratibu za Chama Cha Mapinduzi. Alieleza kuwa wakati wa kampeni utakapofika kila mtu ambae anasifa za kugombea hatozuwiwa kwa kuwa ni haki yake ya msingi na kidemokrasia.

"Hivi sasa wakati wake bado haujafika tuwaachie viongozi waliopo madarakani wamalize muda wao na kama wananchi watakuamini watakuchagua tu yanini kufanya kampeni muda huu," alisema.

Akizungumzia kuhusu vitendo vya udhalilishaji wa watoto mwenyekiti huyo, aliitaka Jumuiya ya Wazazi kutoa elimu kwa walimu wa shule na madrasa ili waweza kuwafahamisha watoto mbinu za kuepukana na vitendo hivyo.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Kaskazini Unguja, Haji Sheha Machano, aliwataka viongozi wa CCM Mkoa na Wilaya kuwashajihisha vijana kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Mpigakura ili waweze kukipatia ushindi wa kishindo chama hicho. Alisema ni vyema vijana waeleweshwe mapema umuhimu wa kujiandikisha katika Daftari la Wapigakura na hatimaye kupata fursa ya kukipigia kura Chama Cha Mapinduzi wakati ukifika.

Kwa upande wao wajumbe wa jumuiya hiyo wameutaka uongozi wa CCM Mkoa na Taifa kwa ujumla kufuatilia, kuzisimamia na kuzitatua changamoto mbalimbali zilizopo katika mkoa wao hasa zile zinazojitokeza kipindi cha uchaguzi.

Wakizitaja baadhi ya changamoto hizo walisema ni pamoja na uhaba wa walimu, vikalio madarasani, baadhi ya walimu kutokuwa na ari ya kusomesha kutokana na shauku za kisasa, baadhi ya watendaji kukiuka majukumu yao wakiwamo askari wakati wa uchaguzi, ukosefu wa vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi na ucheleweshaji wa vitambulisho kwa mawakala wa kusimamia kura.

## Jangili auawa na tembo, aliwa na simba

**JOHANESSBURG,** Afrika Kusini

MTU mmoja ambaye jina lake halijafahamika aliyeshukiwa kuwa jangili wa wanyama aina ya faru amekanyagwa na tembo na kuliwa na simba katika Hifadhi ya Taifa ya Kruger, nchini Afrika Kusini.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa familia ya mtu huyo ilipewa taarifa kuwa kijana wao aliuawa na tembo siku ya Jumanne baada ya kufanyika kwa msako, hatimaye fuvu la kichwa chake kilipatikana na suruali siku ya Alhamisi.

Mkurugenzi wa hifadhi hiyo alitoa salamu za rambirambi kwa familia.

"Kuingia kwenye mbuga ya Kruger kinyume cha sheria na kwa miguu si jambo jema, ni mbuga yenye hatari nyingi na tukio hili linadhihirisha hayo," alisema mkurugenzi huyo.

Hifadhi ya Kruger imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya uwindaji haramu kutokana na uhitaji mkubwa wa pembe za faru kwenye nchi za Bara la Asia.

Siku ya Jumamosi, mamlaka za kiwanja cha ndege Hong Kong zilikamata mzigo mkubwa wa pembe za faru, mkubwa zaidi kuwahi kukamatwa katika kipindi cha miaka mitano wenye thamani ya pauni milioni 1.6. **BBC**

## Aenda jela kwa wivu wa mapenzi

**DUBAI,** Falme za Kiarabu

MWANAMKE mmoja raia wa Uingereza anakabiliwa na kifungo cha miaka miwili gerezani mjini Dubai kwa kumuita 'farasi' mke wa mtalaka wake katika mtandao wa kijamii wa Facebook.

Laleh Shahravesh, (55), alikamatwa baada ya kutua katika Uwanja wa Ndege wa Dubai kuhudhuria mazishi ya mume wake wa zamani.

Ameshtakiwa kutokana na maneno aliyoyachapisha katika mtandao huo baada ya mtalaka wake kuoa tena mwaka 2016. Shahravesh alikuwa kwenye ndoa kwa miaka 18 na aliwahi kuishi Dubai kwa miezi 18, kwa mujibu wa mamlaka mji huo.

Baada ya kurejea nchini Uingereza na binti yake, mtalaka wake alisalia Dubai na kuoa mke mwingine.

Sharavesh alifahamu kuhusu hatua ya mtalaka wake kuoa tena baada ya kuona picha ya wanandoa hao katika mtandao wa kijamii wa Facebook.

Aliandika maneno ya matusi kwa lugha ya Kiajemi na kuongeza kuwa mtalaka wake ni mjinga na kumuita farasi mke wake mpya. Chini ya sheria ya mtandao ya Falme za Kiarabu, mtu anaweza kufungwa jela au kutozwa faini kwa kutoa kauli za chuki mtandaoni.

Maofisa mjini Dubai wanasema kuwa Shahravesh huenda akafungwa jela miaka miwili au kutozwa faini ya pauni 50,000, licha ya kuchapisha maneno hayo akiwa nchini Uingereza. **BBC**

# Waziri wa Usalama wa Ndani Marekani ajiuzulu

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ametangaza kujiuzulu kwa Waziri wa Usalama wa Ndani, Kirstjen Nielsen, hatua inayosisitiza nia yake ya kuimarisha sera ya uhamiaji.

Kujiuzulu kwa Nielsen kunahitimisha uhusiano magumu na Rais Trump, ambaye alisema kutokufarishwa na utendaji kazi wake licha ya utiifu mkubwa kwake.

Wakati wa uongozi wake wa miezi 18 katika wizara hiyo yenye nguvu, Nielsen mwenye umri wa miaka 46, alitambulika kwa utaratibu wenye utata wa kuwatenganisha watoto na wazazi wao, hali iliyomsababishia mara kwa mara kuandamwa na makundi ya haki za binadamu na chama cha upinzani cha Democratic, ambapo walimtaka ajiuzulu.

Jana Rais Trump kupitia kwenye ukurasa wake wa kijamii wa Twitter aliandika kuwa Waziri wa Usalama wa Ndani, Kirstjen Nielsen, ataachia wadhifa huo na akamshukuru kwa kazi yake.

**Makadirio ya doria za mpakani yanaonyesha kuwa idadi ya wahamiaji wanaopita kwenye mpaka wa Mexico ilkuwa zaidi ya 100,000 mwezi Machi, wengi wao kutoka El Savador, Honduras na Guatemala.**

Aliongeza kuwa Kamishna wa Forodha na Ulinzi wa Mipaka wa Marekani, Kevin McAleenan atakuwa kaimu waziri kuchukua nafasi ya Nielsen.

McAleenan ni ofisa wa muda mrefu wa ulinzi wa mipaka nchini Marekani ambaye anaheshimiwa sana na wabunge. Kwenye barua yake ya kujiuzulu, Nielsen alisema kuwa: "Licha ya hatua zilizochukuliwa katika kuufanyia mageuzi usalama wa ndani, umefikia wakati wa mimi kujiuzulu".

Kujiuzulu kwa Kirstjen kumekuja zikiwa zimepita siku mbili baada ya yeye na Rais Trump kuzuru kwa pamoja eneo la mpaka wa Mexico, Jimbo la California, ambapo Rais Trump alitoa ujumbe mkali kwa wanaopanga kuwa wahamiaji haramu na waomba hifadhi akisema kuwa Marekani imejaa.

Licha ya onyo la kutokea madhara makubwa ya kiuchumi alilopewa na viongozi wakuu wa chama chake cha Republican, Rais Trump mara kwa mara ametishia kuufunga mpaka wa Marekani na Mexico, akilitaka Bunge la Marekani na serikali za nchi za Amerika ya Kati kuchukua hatua za kudhibiti wahamiaji.

Makadirio ya doria za mpakani yanaonyesha kuwa idadi ya wahamiaji wanaopita kwenye mpaka wa Mexico ilkuwa zaidi ya 100,000 mwezi Machi, wengi wao kutoka El Savador, Honduras na Guatemala.

Kwa mujibu wa Nielsen, hiyo ni idadi kubwa kabisa kuwahi kusajiliwa kwa mwezi katika muda wa muongo mmoja.

Rais Trump alipunguza msaada katika nchi hizo tatu mwezi uliopita kutokana na idadi kubwa ya wahamiaji kuingia Marekani. **VOA**



Wanajeshi watiifu wa kamanda Khalifa Haftar, wakitoka nje ya mji wa Benghazi kuongeza nguvu ya vikosi vinavyofanya mashambulizi kuingia Tripoli, Libya. **PICHA: REUTERS**

## Utawala wa Kagame waendelea kukosolewa

**KIGALI,** Rwanda

WAKATI Rwanda ikiadhimisha kumbukumbu ya miaka 25 ya mauaji ya kimbari, ambapo Watutsi na Wahutu 800,000 waliuawa mnamo mwaka 1994, utawala wa Rais Paul Kagame umeendelea kukosolewa na wapinzani wake.

Upinzani nchini humo umedai kuwa Rais Kagame tangu aingie madarakani amewakandamiza viongozi wa upinzani.

Miaka miwili iliyopita, Kagame alichaguliwa tena kuwa Rais wa Rwanda kwa kupata kura asilimia 98 kwa kipindi cha muhula wa tatu, dhidi ya wapinzani wa kisiasa kutoka jamii ya Wahutu walio wengi. Mwezi uliopita, Rais Kagame alitoa kauli iliyozua utata kwa kusema kuwa mauaji ya mmoja wa wapinzani wake, Seth Sendashonga, zaidi ya miaka 20 iliyopita, aliuawa kwa sababu alikuwa amevuka mstari mwekundu.

Sendashonga ambaye alikuwa Waziri wa zamani wa Mambo ya Ndani, alihitilafiana na Rais Kagame na kulazimika kutoroka nchi, aliuawa nchini Kenya, ambako alikuwa amekimbilia.

Familia ya Sendashonga imeendelea kushutumu serikali ya Rais Kagame kuhusika katika mauaji yake.

Tangu kumalizika kwa mauaji ya kimbari, wengi wa wapinzani walifanyiwa vitisho, wengine waliuawa nchini Kenya, Uganda, Ubelgiji, Uingereza na Afrika Kusini.

Miaka mitano iliyopita, uhusiano kati ya Afrika Kusini na Rwanda ulikuwa umedorora baada ya viongozi wa Afrika Kusini kukasirishwa na mauaji ya mshirika wa zamani wa Rais Kagame jijini Johannesburg. Kanali Patrick Karegeya, Mkuu wa zamani wa Idara ya Ujasusi ya Rwanda, ambaye pia alihitilafiana na Rais Kagame, alikutwa ameuawa katika chumba kimoja cha hoteli jijini Johannesburg, Afrika Kusini.

Hata hivyo, serikali ya Rwanda imeendelea kufutilia mbali madai ya kuhusika kwake katika mauaji na vitisho kwa wapinzani wake wa kisiasa.

Lakini kwa mara kadhaa Rais Kagame amekuwa akitoa kauli zisizoridhisha wapinzani wake, amewahi kusema kuwa: "Mtu yeyote atakayefanya uhaini dhidi ya nchi hii atajutia," alisema Kagame siku chache baadaye baada ya mauaji ya Patrick Karegeya. **RFI**

# JPM awaonya mawaziri

INATOKA UK. 3

Alisema juzi akiwa Newala alipita katika viwanda vya korosho viwili vilivyojengwa na Mwalimu Julius Nyerere vya kuboresha korosho zaidi ya tani 10,000 ambavyo hata hivyo viliuzwa kwa Sh. milioni 75 na havifanyi kazi.

Kwa mujibu wa Rais, waliovinunua walivitumia kukopa fedha benki Sh. bilioni mbili na kuviacha bila kufanya kazi na kwamba kama viwanda hivyo vingekuwa vinafanya kazi, asingekuwa anahangaika kutafuta fedha za serikali kulipa wananchi.

**JESHI MIRADI YA DHARURA**

Rais Magufuli aliwapa maelekezo mawaziri na sekta mbalimbali kulipa kipaumbele jeshi kwenye miradi ya dharura ili kupunguza gharama na kuharakisha mradi na kupunguza mlolongo na ukiritimba wa kutangaza zabuni.

"Kwa mfano Waziri wa Nishati upo hapa kama kuna kijiji unataka ukipeleke umeme halafu unataka mtu akasimike nguzo pale, waite wanajeshi wakachimbe haraka kuliko kutangaza zabuni. Hata hivyo fedha hizo zitasaidia kununua buti," alisema.

Alilitaka jeshi hilo liendelee kupanua viwanda ili kuweza kutoa ajira kwa vijana wanaohitimu mafunzo ya JKT ambao wameiva maeneo yote.

URAIS 2015

Rais Magufuli alisema hakujua kama kazi ya urais ni mateso na amewashangaa wanaoupenda.

"Hata mimi sikujua, nilivyoona wanaombaomba wengi 42, wengine wala hawafai kabisa nikaona ngoja ni bipu nilivyobipu ikakatalia simu ikapiga, lakini sikujua mzigo wenyewe, ndio maana nasema kipindi changu kikiisha sitaki niongezewe hata saa moja," alisema.

Alisema anataka katika kipindi chake ahakikishe anatekeleza yale Watanzania wanayopenda.

"Nikabadilishe yanayokwamisha nchi kwenda mbele, nikanyamazishe dhuluma na mateso, Watanzania wamekuwa wakiyapata kwa sababu ya watu wachache wanaopenda fedha za haraka. Nina uhakika asilimia 100 siku moja Watanzania watanikumbuka," alisema.

Rais Magufuli alisema katika nchi ambazo hazina amani mambo mengi ya uchumi yamekwama.

"Huwezi kulima wakati pale kuna vurugu, hata mbegu hutaweza kuzipata, nimeona masista wengi hapa huwezi kwenda kuomba kanisani katika kipindi cha kwaresma wakati mabomu yanalia pembeni mwa kanisa," alisema.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Hussein Mwinyi, alisema wanao mpango wa jeshi wa miaka 15 ambao unamadhumuni ya kuhakikisha wanajikita katika maeneo manne makuu.

"Maeneo hayo ni kuboresha zana za kijeshi ambapo tupo vizuri kamandi zote tatu jeshi la nchi kavu, maji na anga tunakwenda kwenye sera ya nchi ya kuwa na jeshi dogo lenye ueledi na zana za kisasa, eneo lingine ni kujenga miundombinu tumeshajenga nyumba za makazi ya askari 6,000.

"Eneo lingine ni mafunzo na mazoezi ambalo wanajeshi wetu wapo vizuri na mwisho ni maslahi ya wanajeshi. Pia kila mwaka JKT inaingiza vijana wa kujitolea na wale wa kufuata sheria, kwa mwaka jana tulikuwa na vijana 12,000 na wale wa kufuata sheria walikuwa 20,000," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akibadilishana mawazo na Rais mstaafu wa Nigeria, Olusegun Obasanjo, walipokutana jijini Kigali juzi, katika kumbukumbu ya miaka 25 ya mauaji ya Kimbari yaliyotokea 1994. Waziri Mkuu alimwakilisha Rais John Magufuli. **PICHA: OWM**

# IGP aonya maandamano ya ACT

**Na Mary Mosha,** SIHA

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Simon Sirro, amesema vijana wanaojiandaa kufanya maandamano ya kupinga uamuzi wa Bunge kutofanya kazi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, wafuate taratibu za kupata kibali, la sivyo watashughulikiwa kama wahalifu wengine.

Sirro alitoa onyo hilo jana alipoongozana na Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola, kushuhudia mafunzo ya askari zaidi ya 800 katika uwanja wa medani za kivita wa Kilele Pori katika Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro.

"Wanaotarajia kuandamana niwaombe wafuate sheria na taratibu za maandamano tofauti na hapo watakuwa wanavunja sheria za nchi na sisi tutawashughulikia kama wahalifu wengine wa hapa nchini, niwaombe kufuata sheria," alisema Sirro.

Jana, ngome ya vijana ACT- Wazalendo walitangaza nia yao ya kutaka kufanya maandamano leo jijini Dodoma yenye lengo la kulishinikiza Bunge kufuta azimio lake la kutofanya kazi na CAG Assad.

Katibu wa Mawasiliano Ngome ya Vijana, ACT - Wazalendo, Karama Kaila, alinukuliwa juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari Aprili 7, 2019 katika ofisi za Makao Makuu ya Chama cha ACT-Wazalendo, Kijitonyama jijini Dar es Salaam, akisema watafanya maandamano ya amani.

Kaila pia alisema kwamba dhumuni la maandamano hayo ni kulishinikiza Bunge kuweka kwenye shughuli zake (Order Paper ) upokeaji wa taarifa ya CAG ikiwa na saini ya Prof. Assad ifikapo Aprili 10, 2019 saa tatu asubuhi.

Alisema wao kama vijana wa ACT-Wazalendo kwa niaba ya mabaraza, jumuiya na ngome za vijana wa vyama vya siasa vya NCCR Mageuzi, CHAUMA, UPDP na vyama vingine vitatu ambavyo vitaungana nao baada ya uamuzi wa vikao vyao vya ndani, watafanya maandamano hayo ya amani mkoani Dodoma siku hiyo.

"Tumefikia uamuzi huu baada ya kujiridhisha kwamba uamuzi wa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Job Ndugai na Bunge kwa ujumla wake kusitisha kufanya kazi na CAG ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imeanzisha Mamlaka ya CAG na kuzuia kabisa kuingiliwa katika majukumu yake na kwamba ni wajibu wa kila raia kuilinda Katiba," alisema Kaila.

Amesema kwa Mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Polisi (police ordinance) ambayo inataka kutoa taarifa kwa saa 48 kabla ya muda wa maandamano, umma ufahamu kuwa tayari wamekwisha toa taarifa ya kufanyika kwa maandamano hayo kwa OCD-Dodoma.

Alibainisha kuwa maandamano hayo yatafanyika leo, Jumanne, saa 3:00 asubuhi na kwamba yataanzia Nyerere Square jijini Dodoma kupitia Barabara ya Jamatini na kuingia Barabara ya Bunge hadi jengo la Bunge jijini Dodoma.

Kaila aliongeza kuwa wamemwomba Spika wa Bunge au Naibu Spika apokee maandamano hayo ya amani.

# Waziri awa mbogo ujenzi wa hospitali

**Na George Tarimo,** MUFINDI

SERIKALI imetoa mwezi mmoja kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa kuhakikisha ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo unaanza mara moja.

Agizo hilo limetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, wakati akikagua ujenzi wa hospitali hiyo na kusema kuwa anasikitishwa na hajaridhishwa hata kidogo na kasi ndogo ya ujenzi huo ambao unajengwa eneo la Igowole.

Kufuatia kusuasua huko, Waziri Jafo alisema hajaridhishwa na ujenzi huo kutokana kwa kuwa ulianza muda mrefu, lakini hadi sasa upo hatua ya msingi na kuutaka uongozi huo kuhakikisha wananyanyua kwa haraka kuta za majengo yote hadi kufikia usawa wa lenta, laa sivyo waliosababisha uzembe huo watachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwamo kushushwa cheo.

Ziara ya Waziri Jafo ambayo ilikuwa ni ya kushtukiza wilayani humo na alikuta ujenzi huo upo hatua ya msingi, huku saruji zikiwa chache, mawe yameisha na tofali hazitoshi. Katika ujenzi huo, serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 1.5.

"Hapa kuna uzembe wa hali ya juu na adhabu yake inakuja, wananchi wasiokuwa na hatia wanataka hospitali ikamilike, nataka hadi Mei 8 hospitali iwe katika usawa wa lenta na nikikuta uzembe hatohamishwa mtu bali atashushwa cheo kwa sababu huwezi kuzungumzia mradi mkubwa kama huu wakati stoo kuna mifuko 200 ya saruji," alisema Jafo.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO KISESA (W) MAGU**
**SHAURI LA MADAI NA. 17/2019**

**HAMADI MBINZAGULILE.........................MDAI**
**DHIDI YA**
**RENATUS MAELO MAGESA..............MDAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**
**KWA: RENATUS MAELO MAGESA**
**POPOTE ALIPO, SIMU- 0742-181 856 / 0682-954 357**
**(TANZANIA).**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai ambayo maelezo ya Mdai mameelezwa katika nakala ya Madai ambazo zinapatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajika kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au Mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa siku ya tarehe 24/4/2019 saa 2:30 asubuhi, mbele ya Mh. Mwakisu.

Angalia kama hukuhudhuria siku hiyo tajwa hapo juu na Mahakama ikathibitisha kuwa umepokea kuitwa shaurini inaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa mbele yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 03 mwezi 04 mwaka 2019.

215164902


Kwa Habari Motomoto usikose

Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO




# COSTA ANUKIA 'JELA' MECHI 12

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid, Diego Costa, anaweza kukumbana na adhabu ya kufungiwa hadi mechi 12 kwa sababu ya kadi nyekundu aliyoonyeshwa kwenye mchezo wa Jumamosi wa kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Barcelona.

Costa alitolewa nje kwa kadi nyekundu baada ya kumtukana mwamuzi wa mchezo huo, Gil Manzano, katika dakika ya 28 ya mchezo huo. Na matokeo hayo, Gazeti la AS limesema kwamba, Costa anaweza kufungiwa mechi 12 kama akikutwa na hatia ya kuvunja sheria ya kifungu cha 94 cha La Liga cha nidhamu, ambacho kinasema mchezaji ataadhibiwa moja kwa moja akikutwa na hatia ya kumtukana mwamuzi au ofisa yeyote wa mchezo.

Hata hivyo, anaweza kupata adhabu ndogo ya kufungiwa mechi mbili au tatu kama maofisa wa La Liga wakiamua kutumia kifungu cha 117, ambacho kinatoa tafsiri ya maneno ya mchezaji kwa mwamuzi.

Aidha, Costa pia anakabiliwa na adhabu nyingine wakati akifanyiwa uchunguzi zaidi kwa kile alichokifanya dhidi ya mwamuzi Manzano.

Mwamuzi huyo alisema kwamba Costa alirudia mara kadhaa kwa kumsukuma na kumtukana baada ya kuwaonyesha kadi wachezaji wenzake, Diego Godin na Jose Gimenez, ambapo pia adhabu yake ni kukosa mechi 12. Costa kama akifungiwa mechi 12 maana yake atakosa mechi zote zilizobaki za Ligi Kuu ya Hispania msimu huu.

# Klopp: Nitakaa Liver kwa muda mrefu

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amebainisha kwamba anaweza kubakia kwenye dimba la Anfield kwa miaka mingi wakati 'Wekundu' hao wakiwa kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Raia huyo wa Ujerumani amekuwa akihusishwa na kurudi kwa miamba wa soka wa Ujerumani, Bundesliga, mapeka wiki hii, huku mabingwa Bayern Munich wakitajwa kumnyatia.

Liverpool kwa sasa wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu ya England kwa tofauti ya pointi mbili, ingawa Manchester City wanawakimbiza wakiwa na mchezo mmoja mkononi.

Katika mahojiano na Gazeti la Ujerumani, Die Welt kocha huyo wa zamani wa Borussia Dortmund alipoulizwa anajiona atakuwa kocha wapi kwa siku za usoni na kama kuna uwezekano wa kutua Bayern.

Akijibu swali hilo pamoja na mipango yake, Klopp alisema: "Nina mkataba na Liverpool hadi mwaka 2022 na hakuna yeyote kati yetu ambaye anafikiria kukatisha mkataba kabla ya muda wake.

"Sijui lini nitaondoka Anfield. Kuna muda mrefu wa kukaa hapa. Kwa kawaida soka ni kama hivi: Kuwa kwenye nafasi nzuri, kwa muda muafaka.

"Lakini nina furaha ya kuendelea kucheza hapa na sihisi kama nimemaliza kukaa hapa. Timu yangu ni nzuri na tunaweza kuendelea kuwa hapa kwa pamoja."



# Busquets akumbushia Barca ilivyoichapa Utd




**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa Barcelona, Sergio Busquets, ameelezea ushindi wao wa 3-1 dhidi ya Manchester United kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2011 kama ni wakati bora zaidi katika mafanikio ya kihistoria ya klabu hiyo.

Chini ya kocha wa sasa wa Manchester City, Pep Guardiola, Barcelona ilifurahia mafanikio makubwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2011.

Mabao kutoka kwa Pedro, Lionel Messi na David Villa yaliiwezesha Barcelona kutwaa taji hilo kwa mara ya pili katika misimu mitatu, kuisaidia kupata heshima ya kuwa klabu kubwa zaidi duniani.

Akizungumza na Daily Mail kuelekea kwenye mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya timu hizo, Busquets alikumbushia mafanikio waliyoyapata Barcelona dhidi ya United.

Alisema: "Nilikuwa sehemu ya kila mafanikio tuliyopata kwa wakati huo. Ulikuwa muda wa mabao, mafanikio yetu yalikuwa kwenye kilele kizuri.

"Wazo lilikuwa ni namna gani tulivyocheza na kuwa kwenye kiwango cha juu na sasa tunaendelea kucheza kwa kiwango cha juu.

"Muda mwingine unaweza kuhisi kwamba wakati ukiwa kileleni ni wakati wa kuendelea kuwa nafasi hiyo hiyo.

"Tulijiandaa vizuri na tulikuwa kwenye kiwango cha juu zaidi, kiasi kwamba ule ulikuwa ni wakati mzuri zaidi kwenye mafanikio yetu na nina imani kubwa ya kuwa tutarudia tena mafanikio yale."

Barcelona imesafiri kwenda katika dimba la Old Trafford na itashuka dimbani Jumatano katika mchezo wa kwanza, kabla ya kurudiana siku sita baadaye katika dimba la Camp Nou.

HABARI MICHEZO

# EMERY: NNE BORA BADO MIKONONI MWA ARSENAL



**LONDON,** England

UNAI Emery amebainisha kwamba Arsenal ilikosa nafasi kubwa wakati wakifungwa bao 1-0 na Everton, lakini bado kuna nafasi ya kumaliza kwenye nne bora ya Ligi Kuu ya England msimu huu.

Bao la Phil Jagielka la dakika ya 10 katika dimba la Goodison Park juzi Jumapili liliifanya Arsenal kupoteza mchezo wake wa kwanza kati ya saba zilizopita kwenye Ligi Kuu.

Pointi moja ingewatosha Arsenal kuipiku Tottenham na kutwaa nafasi ya tatu kama wangepata hata sare kwenye mchezo huo.


"Tulijua kwamba ungekuwa mchezo mgumu kwetu na tunakwenda kuangalia nafasi kama ya leo (juzi)," alisema Emery.

"Tulipoteza nafasi kubwa leo (juzi) kushindwa kupata pointi tatu. Tutakuwa na nafasi kwenye mechi zijazo. Itategemea na sisi na pia timu nyingine.

"Tunahitaji kucheza kwa kiwango kile kile kwa mechi 38, lakini tulipoteza kiwango chetu kwenye mchezo dhidi ya Everton. Tunahitaji kubadilika na kurudisha kiwango chetu kwenye mchezo unaofuata ili tuweze kushinda.

"Tunaweza kujichukulia kwa mtazamo hasi kwa sababu tumepoteza pointi tatu, lakini bado nafasi ipo mikononi mwetu ya kuitafuta nafasi ya nne bora."

# Pacquiao afuata nyayo za Mayweather



**MANILA,** Ufilipino

BONDIA Manny Pacquiao amefuata nyayo za Floyd Mayweather Jr kwa kusaini mkataba na Kampuni ya Rizin ya Japan.

Rizin ni kampuni ya kupigana pamoja na Karate ['Martial Arts'] ambapo ilimsajili Mayweather na kumtengenezea pambano la Kickboxer dhidi ya Tenshin Nasukawa jijini Tokyo mwaka 2018.

Mayweather alimpiga kirahisi Nasukawa katika raundi ya kwanza na sasa Pacquiao anaweza kuzichapa na bondia huyo chini ya mkataba wake mpya na Kampuni ya Rizin.

Ofisa Mtendaji wa Kampuni ya Rizin, Nobuyuki Sakakibara, alitangaza Jumatano na kuweka picha ya bondia huyo mwenye umri wa miaka 40 kwenye ukurasa wa Twitter.

"Nipo hapa Ufilipino," aliandika Sakakibara.

"RIZIN.15 watakuwa na mtu huyu kwa njia yoyote. Tutakuwa tayari kuja tena Japan!"

Hakubainisha wazi kwamba Pacquiao atakuwa kwenye tukio la Aprili 21, mwaka huu.

Pambano la mwisho la Pacquiao lilikuwa lenye matokeo ya utata dhidi ya bondia Mmarekani, Adrien Broner Januari.

Mayweather, ambaye alimpiga Pacquiao mwaka 2015, alirudi ulingoni baada ya kustaafu kwa muda na kumchapa Nasukawa.

# *Madrid kumsajili Hazard kwa pauni milioni 100*



**MADRID,** Hispania

REAL Madrid wamejiongezea imani ya kumsajili, Eden Hazard, kipindi cha majira ya joto kinachokuja, Sky Sports imebainisha.

Hata hivyo, Chelsea inataka kiasi cha pauni milioni 100 licha ya kwamba, Hazard akiwa amebakiza mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake.

Chelsea ambayo kwa sasa imepigwa marufuku ya kutokusajili kwa misimu miwili ikianza na kipindi cha majira ya joto kinachokuja, kuondoka kwa wachezaji wake nyota kutawaweka kwenye wakati mgumu zaidi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji mapema mwanzoni mwa msimu huu, alisema amekuwa akisita kusaini mkataba mpya hapo Stamford Bridge kwa sababu ya ndoto zake za kwenda kule Bernabeu.

"Kila nikiamka asubuhi kichwani mwangu nafikiri kwamba nataka kuondoka," alisema Oktoba mwaka jana. "Kuna wakati nafikiri nataka kubaki hapa. Ni maamuzi magumu. Lakini ni majaliwa yangu ya baadaye, lazima niamue sasa."

Hazard pia alizungumzia uamuzi wa kutaka kuondoka na kwenda kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Hispania baada ya Kombe la Dunia mwaka jana nchini Urusi, akiamini kwamba anahitaji kwenda sehemu nyingine ili kuimarisha zaidi kipaji chake.

"Ndio maana nilizungumza baada ya Kombe la Dunia nilisema huu ni wakati wa kubadilika, kwa sababu nilikuwa na wakati mzuri kwenye michuano ya Kombe la Dunia," alisema.

"Kwa hakika nipo kwenye mchezo ninaoupenda, nacheza soka zuri kwa wakati huu. Real Madrid ni klabu kubwa duniani. Siwezi kudanganya leo hii."

Hazard, ambaye amefikisha umri wa miaka 28 Januari mwaka huu, alisajiliwa Chelsea kwa pauni milioni 32 akitokea Klabu ya Ufaransa ya Lille mwaka 2012 na amefunga mabao 106 katika mechi 341.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DE BRUYNE: SPURS ITAFIA UWANJA MPYA

●●● Sijali kuhusu uwanja, ninajali kuhusu timu tunayocheza nayo, kila mmoja ana uwanja na kila mmoja...

**Manchester,** England

KIUNGO wa Manchester City, Kevin De Bruyne, hafikirii kuwapo kwa Tottenham katika uwanja wao mpya kutakuwa na athari kubwa kwao katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya robo fainali.

**Kikosi hicho cha Pep Guardiola kitashuka katika Uwanja wa Tottenham Hotspur baada ya Spurs kuchelewa kwa muda mrefu kuufungua uwanja wao unaochukua watazamaji 62,000, na kisha kuufunga kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Crystal Palace.**

City inatarajia kukutana na mashabiki wengi wa kushangaza katika mechi hiyo ya mkondo wa kwanza itakapowafuata leo wababe hao wa kaskazini mwa London, lakini De Bruyne anafikiria zaidi ubora wa wachezaji kama Harry Kane, Christian Eriksen na Dele Alli kuwa ndio unaoweza kuipaisha Tottenham.

"Sijali kuhusu uwanja," nilisema. "Ninajali kuhusu timu tunayocheza nayo.

"Kila mmoja anazungumza kuhusu uwanja kama ni kitu cha kipekee. Kila mmoja ana uwanja. Kila mmoja ana mashabiki. Itakuwa ni juu yao kwa hilo.

"Sidhani kama kutakuwa na tofauti yoyote. Pengine watakuwa na msisimko kidogo, lakini mwishoni ni uwanja na mashabiki.

"Kama watakwenda Uwanja wa Wembley na mashabiki 80,000 ama wakiwa na 62,000, itakuwa kitu kile kile. Itakuwa mechi ngumu lakini nadhani tutakuwa vizuri."

City iliichapa Brighton and Hove Albion kwa bao 1-0 kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA Jumamosi na itavaana sasa na Watford wakati itakaporudi Wembley mwezi ujao.

De Bruyne na wachezaji wenzake waliichapa Chelsea kwa changamoto ya mikwaju ya penalti na kutwaa Kombe la Ligi (EFL Cup) Februari mwaka huu na sasa wamebakiza vita nyingine ya ubingwa wa Ligi Kuu England dhidi ya Liverpool.

Guardiola anadhani City kumaliza ikiwa imetwaa mataji manne ni jambo linalobaki kuwa "gumu" na De Bruyne anaona ugumu wa ratiba wanaoujadili unapaswa kutambuliwa.

"Hakuna pointi ya kulifikiri hili. Unajua ni kwa namna gani ratiba ilivyo ngumu?" De Bruyne alihoji.

"Nadhani watu wanadharau jinsi ratiba inafika haraka. Huwezi kufikiri kuhusu hili. Hata hatuna muda wa kupumzisha wenyewe, hivyo tunawezaje kufikiri kuhusu nini kitakwenda kutokea ndani ya wiki nne?

"Tunakwenda tu kucheza Jumanne na kisha kutumai kucheza mchezo mzuri."

## ZISIKUPITE

### KUMPISHA POCHETTINO

AC Milan inamtaka kocha wa Tottenham, Mauricio Pochettino, kurithi mikoba ya Gennaro Gattuso na itampa pauni milioni 300 za kufanya usajili. ***(Mirror)***

### AACHIWA KAZI KWA POGBA

REAL Madrid inatumai wakala wa Paul Pogba, Mino Raiola anaweza kufanikisha kiungo huyo wa Manchester United na Ufaransa mwenye umri wa miaka 26 kutua Bernabeu. ***(Marca)***

### PELLEGRINI, DZEKO KUUNGANA

KOCHA wa West Ham, Manuel Pellegrini, anataka kumsajili mshambuliaji wa Roma, Edin Dzeko, ambaye alicheza chini yake wakiwa Manchester City. ***(Express)***

### KLOPP AZIDI KUNOGEWA LIVER

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema anataka kubaki katika klabu hiyo angalau kwa kipindi kingine cha miaka mitatu. ***(Times)***

### HAZARD AANDALIWA DAU REAL

REAL Madrid inapanga kutoa ofa mpya kwa kiungo wa Chelsea na Ubelgiji, Eden Hazard, 28, licha ya 'Blues' hao kusubiri pauni milioni 100. ***(Telegraph)***

### CHELSEA YAMGEUKIA BRUNO

CHELSEA inataka kumsajili kiungo wa Athletico Paranaense, Mbrazil Bruno Guimaraes, 21, endapo itaepuka kifungo cha usajili. ***(Mail)***

### SARRI GIROUD KUBAKI CHELSEA

KOCHA Maurizio Sarri anatarajia kumwona straika Olivier Giroud, akibaki Chelsea msimu ujao. ***(Mail)***

### COUTINHO AKATAA KURUDI EPL

KIUNGO wa zamani wa Liverpool, Philippe Coutinho, ambaye kwa sasa yupo Barcelona, amesema hana mpango wa kurudi tena Ligi Kuu England, epl. Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 26, alijiunga na Barca Januari 2018. ***(Mirror)***

### ORIGI KUULA TENA LIVERPOOL

LIVERPOOL ipo tayari kumpa mkataba mpya mshambuliaji Mbelgiji Divock Origi, 23. ***(Football Insider)***

### VAN DER SAR AIOTA TENA UTD

KIPA wa zamani wa Uholanzi, Edwin van der Sar, amesema labda "siku moja" anaweza kurudi Manchester United. Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 48, ambaye kwa sasa ni mkurugenzi wa soka wa Ajax, alitumikia Old Trafford kwa kipindi cha miaka sita. ***(Times)***

### ABRAHAM MBADALA WA WERNER

RB Leipzig inaandaa ofa ya pauni milioni 30 kwa straika Tammy Abraham, 21, anayecheza kwa mkopo Aston Villa akitokea Chelsea, ikitaka akawe mbadala wa Mjerumani Timo Werner, 23. ***(Football Insider)***

### HAYDEN KUSEPA NEWCASTLE

KIUNGO wa Newcastle, Isaac Hayden, 24, ameiambia klabu yake anataka kuchapa mwendo majira haya ya joto. West Brom imeripotiwa kuvutiwa na mchezaji huyo. ***(Newcastle Chronicle)***

# SERENGETI BOYS, KELVIN KAMILI KUANZA AFCON

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitembelea kambi ya Timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 17 'Serengeti Boys' na kuwaeleza waongeze bidii kwa kuwa Watanzania wanamatumaini makubwa kwao,

**Kocha Mkuu wa timu hiyo, Oscar Mirambo, amesema kupona kwa straika wao, Kelvin John kunakifanya kikosi chake kuwa kamili na tayari kwa michuano ya Afrika (Afcon U-17), ambayo itafanyika jijini Dar es Salaam kuanzia Jumapili Aprili 14 hadi 28, mwaka huu.**

Majaliwa alitembelea kambi ya Serengeti Boys iliyokuwa jijini Kigali, Rwanda wakati akiwa nchini humo Jumapili kumuwakilisha Rais John Magufuli kwenye kumbukizi ya miaka 25 ya mauaji ya Kimbari.

Akizungumza na wachezaji hao, Waziri Mkuu aliwataka wahakikishe wanafanya mazoezi ya kutosha ili waweze kushinda mechi zinazofuata.

"Watanzania wanamatumaini makubwa kwenu, nasi tunazidi kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu muweze kuibuka na ushindi katika michezo yenu [ya Afcon U-17] itakayowawezesha kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia."

Kadhalika, Waziri Mkuu alitumia fursa hiyo kuipongeza Serengeti Boys kwa namna wanavyoitangaza nchi kimataifa kupitia kwenye mashindano mbalimbali wanayoshiriki na kuibuka na ushindi.

Kwa upande wao, wachezaji na uongozi wa timu ya Serengeti Boys walimkabidhi Waziri Mkuu kombe walilolitwaa baada ya kuichapa Cameroon mabao 2-1 na kisha kutoka sare ya 3-3 na Rwanda katika mashindano maalumu kwa ajili ya kujiandaa na Afcon U-17.

Aidha, kocha wa timu hiyo, Mirambo, jana aliliambia Nipashe kuwa wanatarajia kurejea leo wakiwa tayari wameiva kwa ajili ya michuano hiyo ambayo Tanzania ni wenyeji, itakayofanyika jijini Dar es Salaam kuanzia Jumapili Aprili 14 hadi 28, mwaka huu.

Mirambo alisema kikosi chake kimepata maandalizi mazuri, ambayo yamesaidia kuwaimarisha na kuwajenga wachezaji wake na anaamini watawapa Watanzania furaha ambayo wanaisubiri.

Alimtaja mshambuliaji wake tegemeo, Kelvin ambaye aliumia mguu katika mechi ya kwanza dhidi ya Cameroon kuwa anaendelea vema na atakuwa tayari kucheza kwenye mechi ya kwanza ya ufunguzi dhidi ya Nigeria, itakayochezwa Jumapili.

"Mungu mkubwa tunaendelea vizuri hapa Rwanda, tumepata muda mzuri na kurekebisha makosa tuliyoyaona katika mechi hizi za mwisho za kirafiki tulizocheza, pia napenda kuwaondoa hofu Watanzania kuhusu Kelvin, ameshapona na anafanya mazoezi ya pamoja na wenzake," alisema Mirambo.

Serengeti Boys ambayo mlezi wake ni Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, imepangwa Kundi A ikiwa na Nigeria, Uganda na Angola wakati Kundi B linaundwa na Guinea, Cameroon, Morocco na Senegal. Mshindi wa kwanza na wa pili katika kila kundi atafuzu moja kwa moja fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika nchini Brazil Oktoba mwaka huu.



Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia (kulia), akipokea cheti cha shukrani kutoka kwa Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa, Tarimba Abbas, kufuatia shirikisho hilo kuonyesha ushiriki mzuri na kufanikisha michuano ya SportPesa Cup 2019. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Twiga Stars kibaruani Congo

**Na Mwandishi Wetu**

VITANI! Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Soka ya Wanawake (Twiga Stars), Bakari Shime, amesema wamejipanga kupambana ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na hatimaye wanasonga mbele katika mbio za kusaka tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki hapo mwakani.

DRC inatarajiwa kuwakaribisha Twiga Stars katika mchezo wa marudiano wa kuwania tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Stade de Martyrs ulioko mjini Kinshasa kuanzia saa 12:00 jioni kwa saa za Tanzania. Akizungumza na gazeti hili, Shime, alisema wako Kinshasa kwa kazi moja ya kusaka ushindi na mechi hiyo kwake ameifananisha na "vita".

Shime alisema kuwa wachezaji wote walioko Congo wako katika hali nzuri na amewaandaa wachezaji wake kutosikiliza kelele na vurugu za nje ya uwanja.

"Tuko tayari kwa mchezo, jana (juzi) jioni tulifanya mazoezi kwenye uwanja tutakaoutumia, na leo (jana) pia tutaenda kumalizia pale tulipoachia, naamini kama tutaendelea pale tulipoishia nyumbani, tunanafasi kubwa ya kusonga mbele," alisema Shime.

Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Wanawake Tanzania (TWFA) na Mkuu wa Msafara wa timu hiyo, Amina Karuma, alisema jana kuwa kila kitu kiko vizuri na wanachosubiri ni muda wa mchezo kufika.

## Maafande KVZ, JKU washushana

**Na Hawa Abdallah**, ZANZIBAR

TIMU ya Maafande wa KVZ imefanikiwa kuwashusha kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, Maafande wenzao wa JKU baada ya kuwachapa mabao 2-0 katika mechi ya mfululizo wa ligi hiyo iliyopigwa juzi katika dimba la Mau ze Dong majira ya saa kumi alasiri.

Kabla ya mechi hiyo, JKU ilikuwa kileleni mwa ligi hiyo ikiongoza kwa tofauti tu ya mabao ya kufunga na kufungwa, lakini kwa pointi ikilingana na KVZ. Ushindi wa KVZ unaipeleka kileleni mwa ligi hiyo baada ya kufikisha alama 70, huku nafasi ya pili ikishikwa na Maafande wa JKU wenye alama 67.

Katika mchezo huo wa juzi, Maafande wa KVZ walipata bao la kwanza kupitia Amour Bakari katika dakika ya 74, huku bao la pili likipachikwa na mtokea benchi Ayoub Kassim katika dakika ya 90, aliyeingia kuchukua nafasi ya Abdul Ramadhani.

# *Lipuli FC yachangiwa mamilioni kuiua Yanga*

**Na Friday Simbaya, IRINGA**

WADAU mbalimbali wameichangia Lipuli FC 'Wanapaluhengo', kiasi cha Sh. milioni 74 ili ziweze kuwasaidia kufanya vizuri katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA hususan kuelekea mchezo wa nusu fainali dhidi ya Yanga, imeelezwa.

Kiasi hicho cha fedha kilipatikana katika harambee maalumu iliyofanyika juzi kwenye Ukumbi wa Kichangani mkoani hapa na kuhudhuriwa na Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda ambaye alishirikiana vema na Mkuu wa Mkoa, Ally Hapi.

Katika harambee hiyo ambayo haikuhudhuriwa na watu wengi, kiasi cha Sh. milioni 9.3 kilipatikana hapo hapo na kilichobakia kilikuwa ni ahadi kutoka kwa wadau ambao walithibitisha wataichangia timu hiyo.

Akisoma risala mbele ya mgeni rasmi, Katibu wa Chama cha Mpira Iringa (IRFA), Ally Ngalla, alisema Lipuli inakabiliwa na tatizo la fedha za kujiendesha na kulipa mishahara ya wachezaji wake na watendaji muhimu wa timu hiyo.

"Wachezaji hawajalipwa mishahara ya miezi miwili, tunapenda kuwashukuru wadau wote waliojitoa kwa moyo kuichangia timu hii hasa Kampuni ya ASAS iliyoko chini ya Mkurugenzi wake, Salim Abri ambaye ameahidi kuichangia Lipuli Sh. milioni 10," alisema Ngalla.

Alisema ASAS wao wamekuwa wakiisaidia timu hiyo pia kwenye mchakato wa kusajili wachezaji na mambo mengine bila ya kusaini mkataba wowote.

Wadau wengine waliochanga fedha katika harambee hiyo ni pamoja na Jesca Msambatavangu ambaye pia aliwahi kuwa rais wa timu hiyo alichangia Sh. milioni tano, wabunge wa mkoa wa Iringa kupitia CCM walichangia kila mmoja shilingi milioni moja huku Waziri Mkuu mstaafu, Pinda akiichangia Sh. milioni tano.

Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah, Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Jamhuri William, Mkuu wa Wilaya ya Iringa Mjini, Richard Kasesela na Famari Store.

# Michezo

Jumanne Aprili 9, 2019

Nipashe



De Bruyne: Spurs itafia uwanja mpya UKURASA 30



Sergio Aguero akiwa na wachezaji wenzake wa Manchester City katika mazoezi kuelekea mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya robo fainali dhidi ya Spurs itakayopigwa leo katika Uwanja wa Tottenham Hotspur. **HABARI UK. 30**

# Mazembe, Simba marefa kimenuka

## ●●● Caf yawabadili Waethiopia yapanga Wazambia, Wekundu wa Msimbazi washtuka, wapinga, wasema...

**Na Mwandishi Wetu**

WINGU jeusi limetanda kuelekea mchezo wa marudiano wa hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya wenyeji, TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) dhidi ya Simba ya jijini Dar es Salaam baada ya waamuzi wa awali ambao walipangwa kuchezesha mechi hiyo kubadilishwa.

**Awali, Shirikisho la Soka Afrika (Caf), lilitangaza mechi hiyo itakayochezwa Jumamosi mjini Lubumbashi, itachezeshwa na waamuzi kutoka Ethiopia ambao ni Bamlak Tessema Weyesa, Temesgin Samuel Atango na Gilbert Cheruiyot kutoka Ethiopia huku mwamuzi wa akiba akiwa ni Mkenya, Peter Waweru.**

Waamuzi wapya ambao Caf imewatangaza jana ni pamoja na Janny Sikazwe ambaye atasaidiwa na Romeo Kasengele, Audrick Nkole wote kutoka Zambia huku mwamuzi msaidizi namba moja akiwa ni Berhe Tesfagiorgis O'michael wa Eritrea.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema jana kuwa wameandika barua ya malalamiko kwa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kuiarifu Caf wakipinga mabadiliko hayo ambayo yameelezwa yametokana na sababu za kiufundi.

Magori alisema katika taarifa yake kuwa wanaomba Caf ibatilishe uamuzi waliofanya na kurejesha waamuzi waliowapanga awali na kutaja sababu ya kuwateua waamuzi wapya kutoka Zambia inatokana na ukaribu na Lubumbashi isiwe kigezo kikubwa. Kiongozi huyo alisema pia jambo hilo la kubadilisha waamuzi ambalo limefanywa jana na Caf si la kawaida hasa baada ya kumalizika kwa mchezo wa kwanza wa hatua hiyo ya robo fainali.

"Tunaiomba ofisi yake iweze kubadilisha uamuzi huu na kuwaacha waamuzi waliooteuliwa awali kuendelea kuchezesha ili haki iweze kutendeka," ilisema sehemu ya barua hiyo.

Katika taarifa ambazo si rasmi, Simba inadai kuwa mabadiliko hayo ya waamuzi yametokana na shinikizo kutoka kwa Makamu wa Rais wa Caf, Costantine Omar ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

### SIMBA KUKODI NDEGE

Kikosi cha watu 30 cha Wekundu wa Msimbazi kitasafiri kwa ndege maalumu kwenda Lubumbashi.

Hata hivyo, hadi jana mchana bado ilikuwa haijaamuliwa timu hiyo itasafiri lini kwa ajili ya kuwafuata wenyeji wao, TP Mazembe.

"Siku kamili ya safari tutajua leo (jana) jioni," alisema kwa kifupi Magori. Naye Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, aliliambia gazeti hili kuwa jana jioni ndio walianza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo huo wa marudiano baada ya kupewa mapumziko ya siku mbili.

# Yanga, Makambo wazidi kukimbiza

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili kupitia kwa straika Mkongomani Heritier Makambo, yameiwezesha Yanga kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya African Lyon iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza jana, lakini pia yakimwongezea kasi ya mbio za Kiatu cha Dhahabu msimu huu.

Mabao hayo yanamfanya Makambo kucheka na nyavu mara 14 akimzidi bao moja straika wa Simba, Mnyarwanda Meddie Kagere, huku wote hao wakiongozwa na Mtanzania Salum Aiyee wa Mwadui FC mwenye mabao 16 mpaka sasa.

Katika mchezo huo wa jana ambao uliifanya Yanga kufikisha pointi 71 baada ya mechi 30 kama ilivyo kwa Azam yenye alama 63 ikiwa nafasi ya pili, iliwachukua dakika tano tu vijana hao wa kocha Mwinyi Zahera kuandikisha bao la kwanza.

Mpira mrefu wa juu kutoka nyuma uliopigwa na Kelvin Yondani ulimkuta Makambo akiwa anafukuzwa na mabeki wawili, lakini kosa lililofanywa na kipa wa Lyon, Douglas Kisembo, kwa kutoka golini lilimfanya kuuweka nyavuni kirahisi.

Dakika ya 31, Makambo alifunga bao la pili kwa kichwa akiunganisha kimyani mpira wa faulo uliopigwa na Haruna Moshi 'Boban'.

Yanga ambayo inaendelea kutesa kileleni, inaizidi Simba kwa pointi 14, lakini watani zao hao wa jadi wakiwa nyuma kwa michezo nane.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >